# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Sita – Tarehe 10 Septemba, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu:-

(a) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi; na

(b) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu:-

(a) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi; na

(b) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

**MHE. CATHERINE N. RUGE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu:-

(a) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi; na

(b) Azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki *(Minamata Convention on Mercury).*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki *(Minamata Convention on Mercury)*.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki *(Minamata Convention on Mercury)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI**:

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 69

**Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kifungu cha 31(1) cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 kinatekelezwa ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo tafadhali Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremia Komanya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu utoaji wa nafasi ya ajira kwa watu wenye ulemavu waliokidhi vigezo vya msingi vya nafasi zilizo wazi. Sharti hili la sheria ni kwa waajiri wote yaani Serikali na waajiri binafsi. Sharti hili la sheria

ni kwa sababu Serikali inatambua kwamba kazi ni muhimu katika maendeleo ya watu wenye ulemavu inayowawezesha kujitegemea na kuondokana na hali ya kuombaomba. Pia inaleta heshima na hali ya kujiamini katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya Serikali ya kuhakikisha kifungu hiki kinatekelezwa ipasavyo ni kama ifuatvyo:-

i. Serikali imeanzisha kanzidata ya wahitimu wenye ulemavu wenye fani mbalimbali ambao wanazo sifa za kupatiwa ajira kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

ii. Lakini pia tumekuwa tukifanya kaguzi za kazi kupitia Sheria ya Taasisi za Kazi kifungu cha 45A kinachompa fursa Afisa Kazi kutoa adhabu za papo kwa papo.

iii. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya uhamasishaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu kwa njia mbalimbali zikiwemo warsha, mikutano, makongamano, vipindi vya redio pamoja na runinga.

iv. Kwa kushirikiana na Chama cha Waajiri Tanzania tumekuwa tukitoa tuzo kwa mwajiri bora ambaye ameajiri watu wenye ulemavu na kuwawekea mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

v. Tumekuwa tukitumia programu ya ukuzaji ujuzi kwa kukuza ajira kwa kutoa mafunzo ya kitalu nyumba kwa vijana wakiwemo wenye ulemavu katika Halmashauri mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri wao wenyewe lakini pia kuajiri wenzao na pia kuweza kuajiriwa.

vi. La mwisho tumekuwa tukitoa mafunzo kupitia vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu vya Yombo - Dar es Salaam na Sabasaba -Singida ambavyo mafunzo haya ambayo yamekuwa yanawawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna anavyozifikia Halmashauri zetu na kutoa maelekezo namna ya kuitekeleza mahitaji ya watu wenye ulemavu. Nilikuwa nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkakati wa kuanzisha kanzidata nilitaka kufahamu ni utaratibu gani unaotumika kuwapata wahitimu wenye ulemavu ili waweze kuingizwa katika kanzidata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili katika Halmashauri zetu kuna vikundi vya wajasiriamali wenye ulemavu wakiwepo mafundi selamala, lakini wameshindwa kupata masoko katika ofisi za umma. Nilitaka kufahamu Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia kupata masoko ili waweze kukuza mitaji yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Leah Komanya Mbunge wa Viti Maalum, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Leah kwa jinsi ambavyo amekuwa akihakikisha kwamba watu wenye ulemavu Mkoani Simiyu wanaenda vizuri. Nilienda ziara Mkoani Simiyu tulikuwa naye na kuna mambo niliahidi na niliweza kutekeleza pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza ameuliza kwamba ni utaratibu gani ambao Serikali tunautumia kuwapata wahitimu hao wenye ulemavu na kuweza kuwaingiza kwenye kanzidata yetu.

Awali ya yote tuliweza kuviandikia vyuo vyote vya elimu ya juu pamoja na vyuo vingine ambavyo vinatoa mafunzo kwamba watu wenye ulemavu wanapohitimu basi

Ofisi ya Waziri Mkuu kuna kanzidata ambayo tunawaingiza na kuweza kuwapatia ajira. Lakini njia nyingine ambayo tumekuwa tukiitumia ni watu wenye ulemavu mara nyingi wamekuwa wakipiga simu na wakija ofisini wao wenyewe *physically* kwa ajili ya kutafuta ajira. Kwa hiyo, wanapokuja pale ofisini tunapata zile *details* zao na kuweza kuwaingiza kwenye kanzidata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiongee tu kwa kifupi kwamba kanzidata hii imekuwa na manufaa makubwa, hata mwaka jana tuliweza kupata walimu ambao waliajiriwa pale nafasi za ajira zilipotangazwa kupitia kanzidata hii. lakini pia sasa hivi tuna programy ya *internship* kwa vijana na tunaposema vijana ni pamoja na vijana wenye ulemavu na tunaposema vijana ni pamoja na vijana wenye ulemavu. Kupitia kanzidata hii tumepata wahitimu wenye ulemavu zaidi ya 100 ambao watanufaika nah ii program ya *internship*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza kwamba ni kwa jinsi gani Serikali inafanya kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata masoko ya bidhaa zao, tumekwisha kuzielekeza Halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya biashara za watu wenye ulemavu, lakini pia masoko ambayo yamekuwa yakiandaliwa sasa hivi tumesisitiza kwamba miundombinu ni lazima iwe rafiki kwa watu wenye ulemavu, lakini pia ndani ya hayo masoko wahakikishe kwamba kunakuwa na maeneo ambayo ni maalum kwa ajili ya watu wenye ulamavu. Mikakati ya Serikali iko migni lakini kwa ufupi ni hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Ruge.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali na hasa katika sekta ya elimu imefanikiwa kuajiri walimu wengi wenye mahitaji maalum, lakini changamoto kwa walimu hawa wanaoajiriwa tatizo kubwa ni vifaa

maalum ambavyo vinawasaidia hasa walimu wasiioona, changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha kwamba walimu hawa wanaoajiriwa kwanza wanapelekwa katika shule zenye miundombinu rafiki, lakini pia vifaa hivyo kwamba wanawasaidia ili waweze kufanya kazi zao kwa ufasaha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa kifupi kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mwongozo wa watumishi wenye ulemavu na mwongozo huu tumekuwa tukiutumia kuhakikisha kwamba mtumishi yeyote mwenye ulemavu anapata mahitaji yake ya msingi kwa mujibu wa yale ambayo yameelekezwa ndani ya mwongozo.

Kwa upande wa walimu wenye ulemavu tumekuwa tukielekeza ama mtu mwenye ulemavu yeyote si walimu peke yake, lakini mtu mwenye ulemavu yoyote anapokuwa anafika mahali akaajiriwa basi yeye ni wajibu wake na ndio mwongozo unavyosema kwamba ni wajibu wake kuweza kueleza mahitaji yake kwa mwajiri wake kwamba ili aweze kutekeleza majukumu yake basi mahitaji yake ya msingi ni nini na pale ambapo mwajiriwa huyu anapeleka mahitaji yake kwa mwajiri sisi kama Serikali tumekuwa tukifanya ni sawa na ambavyo tulikuja hapa Bungeni tulikaa na uongozi pia wa Bunge tukiwa Wabunge tukaeleza kwamba kama Wabunge wenye ulemavu tuna mahitaji gani na ili ufanisi wetu katika kazi uweze kwenda vizuri basi Bunge lifanye nini ili tuweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndani ya Serikali haya yamekuwa yakifanyika, walemavu wa viungo wamekuwa wakipatiwa usafiri, lakini pia na wengine kulingana na mahitaji yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, haya Mheshimiwa Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 kifungu cha 31 kinataka waajiriwa waajiri wote kuajiri angalau asilimia tatu ya watu wenye ulemavu. Ni nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Bunge ambalo ndio chombo kinachotunga sheria kinatimiza matakwa haya ili kutoa mfano kwa waajiri wengine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza Bunge kama nimemuelewa vizuri ameuliza kwamba ni nini sasa kwamba Bunge ili lioneshe mfano nadhani sasa hilo ni suala uongozi wa Bunge kwamba ni kwa jinsi gani sasa Bunge litafanya ili kuonesha mfano kwa kuajiri watumishi wenye ulemavu kwa kuzingatia sheria kwamba asilimia tatu ni lazima iwe ni watu wenye ulamavu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutendea haki sana kiti chake na kujibu maswali mazuri yaliyoulizwa kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kupitia Tume ya Huduma za Bunge ambayo ndio yenye Mamlaka ya Ajira katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ajira kwa watu wenye ulemavu pia zimekuwa zikizingatiwa na kama Waheshimiwa Wabunge mtaona mnapishana na watumishi wengine baadhi ya watumishi kwenye Ofisi ya Bunge wakiwa wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kuweza kupitia hizo *quota* na viwango vinavyotakiwa kisheria yako mambo mengi ambayo pia yanatakiwa kuzingatiwa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma. Hata hivyo Tume ya Utumishi wa Bunge itaendelea kuzingatia sheria nyingine pamoja na sheria hii ya mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu ili kuhakikisha kwamba kadri watu wenye ulemavu wanavyoweza kutoa huduma na kuajirwa katika taasisi za Serikali na sekta binafsi waendelee kupewa nafasi na haki sawa kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Na. 70

**Hitaji la Walimu Wenye Taaluma ya Watoto Wenye Mahitaji Maalum - Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** Aliuliza:-

Shule ya Msingi Kambarage ni shule pekee katika Wilaya ya Liwale inayochukua watoto wenye mahitaji maalum (walemavu); lakini shule hiyo haina walimu wenye taaluma hizo na vilevile miundombinu ya shule hiyo sio rafiki kwa watoto wenye ulemavu.

(a) Je, ni lini shule hiyo itapatiwa walimu wenye taaluma husika ili kukidhi mahitaji ya shule?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya shule hiyo ili iweze kukidhi mahitaji ya watoto hao?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kambarage ina wanafunzi 1,283 wavulana wakiwa 636 na wasichana 647. Shule inatoa elimu changamani ambapo wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia wapo 10, wenye ulemavu wa akili kwa maana ya mtindio wa ubongo wapo watano na wenye ulemavu wa ngozi wapo watatu. Uwiano wa walimu na mwanafunzi unatofautiana kulingana na aina ya ulemavu wa wanafunzi. Ulemavu wa akili mwalimu mmoja kwa wanafunzi watano, ulemavu wa kusikia mwalimu mmoja kwa wanafunzi tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kambarage ina walimu watatu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia na mwalimu mmoja kwa wenye ulemavu wa akili. Kwa uwiano huo walimu na wanafunzi ni wazi kuwa hakuna upungufu wa walimu kwa wanafunzi kwenye mahitaji maalum katika shule hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathimini ya miundombinu katika Shule ya Msingi Kambarage na kubaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 50 kinahitajika kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu kwenye Shule ya Msingi Kambarage. Naielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kutenga fedha hizo kwenye bajeti zake zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Vilevile napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa

Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya msingi niliyosema shule hii ni shule pekee katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, shule pekee yenye inawachukuwa watu wenye mahitaji maalum, kwa takwimu hiyo utaona kabisa kwamba bado kuna tatizo la miundombinu, shule hii inahitaji mabweni na ndiyo maana inakuwa na takwimu ndogo ya walemavu kwa sababu walemavu wengi kutoka vijijini wanashindwa kumudu kuandikishwa kwenye shule hii kwa sababu ya ukosefu wa mabweni, lakini siyo hivyo hata wale walimu hao anaowataja...

**MWENYEKITI:** Uliza swali basi Mheshimiwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja; je, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa kujenga mabweni kwenye shule hii ili watoto wanaotoka nje ya Halmashauri hii waweze kumudu kuingia shuleni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa sababu ya mahitaji ya wanafunzi hawa wanatakiwa wafuatiliwe kule wanapokaa manyumbani kwa sababu hawakai bweni kwahiyo panahitajika usafiri wa walimu hao kuwafuatilia kule wanapoishi kuona maendeleo yao namna gani wanavyo *catch* yale masomo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwanunulia vifaa kama vile mapikipiki hawa walimu watatu waliobaki ili waweze kumudu kuwafuatilia hawa watoto manjumbani kwao?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege, kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwanza tunaunga jitihada za Mheshimiwa Mbunge

katika kuhakikisha kwamba hawa wanafunzi wenye uhitaji maalum wanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge jana nilipata fursa ya kuongea na mkurugenzi na tukakubaliana kwamba hicho kiasi cha shilingi milioni 50 itatengwa kuanzia mwezi Desemba wakati tutakapokuwa wanafanya *review* ya bajeti yao kwa sababu na wanaona ni jambo la muhimu sana kuhakikisha watoto hawa wanakuwa katika mazingira yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali lake la pili anaongelea swala zima la usafiri ili walimu waweze kwenda kupata fursa kwenda kuwabaini hata wanafunzi wengine ambao wanashindwa kujiunga kutokana na adha iliyoko huko, naomba ni muhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni azma ya Serikali, siyo walimu peke yao ni pamoja watumishi wote ikiwepo wale wa Ustawi wa Jamii kuhakikisha kwamba tunawabaini watoto wetu wote bila kujali hali zao ili waweze kupelekwa katika maeneo ya kuweza kujufunza sawa na watoto wengine ambao hawana ulemavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pale jimboni Kondoa tunazo shule mbili, Shule ya Iboni na Shule ya Ubembeni ambazo zinavitengo vya watoto wenye mahitaji maalum zote ziko kata moja ya Chemchem ambayo ni kata ya katikati kabisa katika jimbo zima. Hali ya mapato yetu ya ndani ya Halmashauri ni ndogo sana ambayo imetupelekea mpaka mimi mfuko wa jimbo kuweza kusaidia miundombinu stahiki kwa ajili ya wale watoto pamoja na choo, walimu pia hatuna.

Je, Waziri ni lini unaweza ukafanya utaratibu wa kutuupa uzito na kuja kufanya tathimini ya kina ili tuweze kuweka miundombinu stahiki na walimu wa kututosheleza ukizingatia watoto hao wenye mahitaji maalum wanaendelea kuongezeka siku hadi siku?

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Sannda kwa jitihada zake kwa kutumia mfuko wa Jimbo ili kuhakikisha kwamba miundombinu wezeshwi inajengwa katika shule hizo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba watoto wote wenye uhitaji maalum hawaachwi nyuma na suala zima la uhitaji wa walimu ambao wanatakiwa waajiriwe naomba nimuhakikishie kama sisi Serikali tutazingatia maombi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukya.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Shule ya Msingi ya Uhuru iliyoko Arusha ni shule pia yenye watoto walemavu, shule hii inashida pia ya miundombinu, vyoo vyake havifai ukizingatia kuwa walemavu wengi au baadhi ya walemavu ni wale ambao wanatambaa, ukiangalia vile vyoo ni vichafu, havifanyi kazi vizuri maji mpaka yanatitirika nje na tunavyoelewa ukiongelea swala zima la vyoo ni afya.

Je, Serikali itarekebisha lini miundombinu ile ya vyoo katika hile shule ya Uhuru ya Arusha Mjini ili kuwasaidia walemavua hawa watoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba nichukuwe fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Arusha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi nikimuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri

ya Liwale naomba nitumie fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Jiji Arusha kwa sababu nina uhakika wanavyanzo vya mapato vya kutosha, atizame namna gani wataweza kuboresha miundombinu ili wanafunzi wetu wenye uhitaji maalum wasome katika mazingira yaliyo bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea bado tupo Ofisi ya Rais - TAMISEMI, swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba.

Na. 71

**Ujenzi wa Madaraja kata na Vijiji vya Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** Aliuliza:-

Jimbo la Mlimba lina mito mingi mikubwa inayotenganisha kata pamoja na vijiji.

Je, ni lini *TARURA* itajenga madaraja ya kudumu katika Kata ya Mbingu na Kijiji cha Chiwachiwa, Kata ya Igima na Kijiji cha Mpofu, Kijiji cha Ngajengwa (kwa Mtwanga), Kata ya Mchombe na Kijiji cha Igia, Kata ya Mofu na Kijiji cha Ikwambi, Kata ya Mbingu, Kata ya Utengule na Kijiji cha Ipugasa, Kata ya Kamwene na Kata ya Uchindile, Kata ya Msagati Kijiji cha Taweta na Kijiji cha Tanga, Kata ya Kalengakelu na Merela, Kata ya Mlimba - Sokoni na Kata ya Idete – Barabara ya Itikinyu?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imeanza kushughulikia ujenzi wa vivuko katika Halmashauri ya Kilombero hususani Jimbo la Mlimba. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilinunua na kuweka daraja la chuma katika Mto Kihansi linalounganisha Vijiji vya Chita, Idunda na Melera kwa gharama ya shilingi milioni 717.62. Kazi hiyo tayari imekamilika ikiwa ni hatua ya awali ya kuunganisha Kata za Chita na Kalengakele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2019/2020 *TARURA* imetenga kiasi cha shilingi milioni 127.94 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja/makalvati katika barabara za Miembeni - Vigaeni, Kichangani katika Kata za Mbingu, Namwawala - Mofu katika Kata ya Mofu, Iduindembo - Utengule katika Kata ya Utengule, Manyasini katika Kata ya Mlimba, Ngwasi - Uga katika Kata ya Kalengakelu na Uchindile.

Aidha, *TARURA* kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* imeweza kutenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la mita 25 katika barabara ya Kisegese - Chiwachiwa - Lavena ambapo kwa sasa lipo katika hatua za upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha na kujenga barabara, madaraja na makalvati kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu haya ingawa wamekosea sana majina ya vijiji vyangu na kata zangu na pale napenda kutoa marekebisho kwamba pale Taweta ni Kijiji cha Tanganyika siyo Tanga, sisi kwetu hatuna Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali lakini jimbo la Mrimba lina changamoto kubwa sana

ukizingatia sisi ni wakulima kama asilimia 99 kwa hiyo madaraja haya yasipojengwa kwa wakati kwa hiyo mazao mengi yanashindwa kufika sokoni na wakulima kuwa maskini miaka yote.

Je, pamoja na bajeti hii imetengwa, Serikali haioni kwamba iliangalie Jimbo la Mlimba kwa akina ya pekee kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata miundombinu hii ukizingatia mito mingi mikubwa kwa mfano hii Tanganyika kuna huo Mto Kilombero ndiyo unapita huko, chini kuna mamba wengi lini mtafanya na kunatakiwa daraja kubwa.

Je, Waziri mara nyingi naongea na wewe upo tayari sasa kutembelea hilo Jimbo la Mlimba hivi uone hali halisi na uone kwamba kunajitihada za kujenga haya madaraja uone wananchi wanavyoteseka na mara nyingi nakuomba lakini hutaki kwenda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nenda tu kamtembelee huyu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza atuwie radhi kwa kukosea majina ya vijiji vyake hatukukusudia hilo, lakini na yeye mwenyewe amekiri kwamba tumetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuanza kujenga hilo daraja ambalo ni kubwa lakini kiasi cha shilingi 127; naomba Mheshimiwa Mbunge aridhike na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kwamba ni azma yetu kuhakikisha kwamba wananchi wa Mlimba wanapata madaraja na barabara za uhakika katika kipindi chote na mimi nashukuru, leo ameongea hajalia na sisi tunamhakikishia haitatokea kulia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Susan amesema amekuwa akiniomba twende Mlimba naomba nimhakikishie nipo tayara ilikuwa ni swala tu la muda tupange na yeye mwenyewe tumewasiliana kunapindi fulani akasema

kipindi hiki mvua zinanyesha sana hatuwezi kwenda, niko tayari.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la makorongo na mahitaji ya madaraja katika majibo ya vijijini imekuwa kubwa sana na kwa kuwa maeneo haya yanatatiza na kuzuia huduma za jamii nyakati za masika, katika Jimbo la Mbulu Mji kuna Daraja la Gunyoda linalounganisha Halmashauri ya Mbulu Mjini na Halmashauri ya Mbulu Vijijini; mahitaji ya ujenzi wa daraja lile ni zaidi shilingi milioni 600 na kwakuwa fedha tunazopata kutoka *TARURA* kwenye jimbo la Mbulu Mji ni shilingi milioni 600 na hazitaweza kusaidia ujenzi wa daraja hilo pamoja na maeneo mengine nchini. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka mpango mkakati kwa kuainisha baadhi ya maeneo hayo ili tuweze kutatua tatizo hili linalokwaza jamii katika kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Ahsante, jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema katika swali lake kuna maeneo ambayo yanauhitaji maalum na kiasi cha fedha ambacho kinatakiwa kitumike kingi na yeye mwenyewe katika swali lake anasema kiasi ambacho *TARURA* Wilayani kwake wanapangiwa kiasi kidogo, ni vizuri tuendelee kushirikiana tuone maeneo hayo ili tuwe na mpango mahususi katika kuhakikisha sehemu ambazo inahitajika fedha nyingi ili kuwe na andiko maalumu kwa ajili ya kutatua maeneo yenye matatizo makubwa kama hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo yaliyopo Jimbo la Mlimba yanafanana na matatizo yaliyoko katika Jimbo la Kavuu na kwa kuwa nilikwisha omba maombi maalumu kwa ajili ya matengenezo ya daraja linalounganisha Kata ya Chamalemu D na Mwamwamapuli. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kupeleka pesa kwa ajili ya kutengeneza daraja hilo hili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma za afya katika Kata ya Kibaoni badala ya kuzunguka Kata ya Mbede?

**MWENYEKITI:** Ahsante, jibu la kwa swali hilo Mhesimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaondolea adha wananchi ili wasilazimike kuzunguka umbali mrefu wakati ingewezekana kujenga daraja ili wananchi wasitembee umbali mrefu. Naomba nimhaikikishie Mheshimiwa Mbunge ni vizuri baada ya Bunge hili, baada ya kipindi hiki tuwasiliane na *coordinator* wa Mkoa tujue uwalisia na uhitaji kwa ajili ya daraja hilo ambalo linaweza likajenga ili wananchi wasilazimike kutembea umbali mrefu wakiwa wanafuata huduma ya afya ambayo na yeye mwenyewe anaridhika jinsi ambavyo huduma hii inatolewa kwa karibu, lakini adha imekuwa ni hilo daraja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea sasa tunaamia Wizara ya Kilimo na swali linaulizwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini.

Na. 72

**Kutafuta Masoko ya Vitunguu Saumu**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** Aliuliza:-

Wakulima wa vitunguu saumu wanayo changamoto ya soko la kuuzia zao hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la vitunguu saumu nje ya nchi?

**MWENYEKITI:**Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitunguu saumu vinavyozalishwa nchini hutumika ndani ya nchi na vilevile huuzwa nje ya nchi vikiwa ghafi. Aidha, baadhi ya mataifa ambayo hununua vitunguu saumu vinavyozalishwa nchini ni Shelisheli, Visiwa vya Comoro, Msumbiji, Zambia, Mauritania, Kenya, Uganda na Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo ikiwemo vitunguu swaumu, Serikali inakamilisha upatikanaji wa simbomilia *(barcode)* na kiwango cha ubora wa bidhaa zinazotokana na vitunguu saumu kutoka Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).*

Aidha, Wizara imeanzisha Kitengo cha Masoko chenye jukumu la kutafuata mahitaji ya masoko ya wakulima ndani na nje ya nchi ikiwemo vitunguu swaumu kwa kufahamu kiwango kinachohitajika, ubora, bei na muda wa unaohitajika sokoni wa mazao na bidhaa hizo sokoni ili kutoa taarifa kwa wakulima na hivyo kuzalisha mazao yanayokidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO)* ilivijengea uwezo vikundi vya wakulima katika

Bonde la Bashay na kuwawezesha kusindika vitunguu saumu na kuwa katika bidhaa mbalimbali zikiwemo mafuta na unga wa vitunguu saumu. Jitihada hizo zimesaidia kuongeza thamani ya zao la vitunguu saumu muda wa kuhifadhi bila kuharibika ubora wake na kuimarisha soko la bidhaa hiyo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima na wasindikaji wa vitunguu saumu wa Mbulu huwezeshwa kushirki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam kila mwaka ili kutangaza na kutafuta masoko ya viunguu saumu na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Serikali kwa kushirikiana na Asasi Isiyo ya Kiserikali ya *Global Communities* iliandaa Kongamano la Vitunguu Saumu lililofanyika katika Bonde la Bashay tarehe 16 Aprili, 2019 katika *AMCOS* ya *DIDIHAMA* ambapo wafanyabiashara kutoka sehemu mbalimbali za nchi walialikwa lengo likiwa ni kutafuta soko la vitunguu saumu.

Aidha, Serikali inaendelea kudhibiti uuzaji holela wa vitunguu saumu kwa kutumia magunia ya lumbesa, mabeseni na ndoo ili mizani itumike katika minada ambayo hufanyika katika ghala la vitunguu saumu Bashay Wilayani Mbulu na hivyo kuratibu soko na bei ili kumnufaisha mkulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bashay tunazalisha vitunguu na tunasindika pale pale kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tunasindika kwa kutumia mashine ile na kwakuwa tuna rojo na *oil* na tuna *powder;* je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba sasa umefika wakati wewe mwenyewe kuja Bashay kuwasaidia wakulima kwa changamoto hii ya uuzwaji wa vitunguu saumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kwa kuwa kuna wanunuzi na walanguzi ambao hawafuati taratibu kama alivyosema kwenye jibu la msingi; je, aoni yeye mwenyewe hataisaidiaje *AMCOS* ya Bashay kuondokana na uchuuzi huo ambao haufuati vigezo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mgumba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kwamba Serikali tufike pale ili kuona changamoto hii na kuona namna ya kuwasaidia wakulima hawa, kwamba nikimaliza ziara ya Mikoa ya Katavi na Rukwa basi mkoa utakaofuata ni Mkoa wa Manyara pamoja na kufika Mbulu Vijijini kuangalia hali halisi ya wakulima wetu wa vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua kwa sababu sasa hivi ni chama kimoja tu cha msingi kinanunua mazao haya ya vitunguu kutoka kwa wakulima na wanapitia watu mbalimbali kwa ajili ya ununuzi huo, nitafika wakati huo huko kwa ajili ya kuona utaratibu huo wa ununuzi unaofanyika, hasa hawa waliosema kwamba ni madalali ambao sisi tunawaita kwamba ni wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo. Lengo kwamba tutaweza kuunganisha na kuweka mfumo rasmi kwamba kila kijiji wafungue vyama vya msingi vya ushirika ili viweze kukusanya mazao kutoka kwa wanachama wao na wakulima, baadae hawa wanunuzi wadogo wa kutoka ndani na nje ya nchi wakija watumie vyama hivi vya msingi kununua mazao kutoka kwa wakulima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa sababu ya muda tunaendelea. Swali linalofuata bado Wizara ya Kilimo, linaulizwa na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 73

**Ushirika wa Mazao na Wa Akiba na Mikopo**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** Aliuliza:-

Vyama vya Ushirika ndio mkombozi wa wakulima na wafugaji.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vyama hivyo vinaimarika na kuleta tija kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 22 kifungu (f), (g) na (h) kuwa ushirika ndiyo suluhu pekee inayoweza kumkwamua mkulima mdogo kupitia kuungana na kutengeneza chombo imara cha kuwatetea.

Aidha, Wizara inatambua mapungufu yaliyomo sasa katika mfumo wa vyama vya ushirika wa mazao mbalimbali ikiwemo pamba, kahawa, miwa, ufuta ambapo baadhi ya viongozi ambao sio waaminifu wamekuwa wakifanya vitendo visivyofaa ikiwemo ubadhirifu wa rasilimali za ushirika, hali iliyopelekea ushirika kutoaminika miongoni mwa wanachama walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume imeendelea kuimarisha misingi ya utawala bora na uwajibikaji

katika Vyama vya Ushirika kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara mara mbili kwa mwaka na kaguzi za mwisho wa mwaka, kusimamia chaguzi za viongozi na mikutano mikuu ya vyama vya ushirika na kufuatilia utekelezaji wa hoja zinazotokana na matokeo ya ukaguzi na uchunguzi. Aidha, Wizara inafanya tathmini kupitia mfumo mzima wa ushirika kwa kuangalia muundo wake, uendeshaji, usimamizi wa rasilimali zake na fedha za wanachama ili kuleta tija na kufanya uwe wa kibiashara zaidi kuliko udalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine ni pamoja na kuhamasisha wadau mbalimbali hususan vijana, wanawake na vikundi vyenye mwelekeo wa ushirika kujiunga au kuanzisha vyama vya ushirika ili kuongeza idadi ya wanachama, kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo yaani *SACCOS* kwenye vyama vya ushirika vya kilimo na masoko yaani *AMCOS* ili kuwajengea wakulima tabia ya kuweka akiba na kupata mikopo yenye masharti nafuu. Aidha, Wizara kwa sasa inahuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002, kuandaa mkakati wa utekelezaji pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Sheria ya Ukaguzi ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1985 ili kuongeza ufanisi katika ushirika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya kwa ajili ya kuimarisha ushirika, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huko nyuma tulikuwa na *Mara Corp,* tulikuwa na *SHIRECU,* tulikuwa na Nyanza, tulikuwa na *KCU.* Viongozi wake walikuwa na nguvu, weledi na uwezo, lakini vyama vile vya ushirika vilikuwa na mitaji kiasi kwamba vile vyama vya ushirika ndiyo vilivyonunua mazao ya wakulima na siyo kununua peke yake, hata kusindika na mfano ni Mkoa wa Mara, tulikuwa na Kiwanda

cha *Mwatex* na Mwanza walikuwa na *Mutex* na Mwanza, lakini tulikuwa na *Mgango Ginnery,* tulikuwa na *Ushashi Ginnery,* tulikuwa na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusindika mazao ya wakulima. Sasa ushirika huu umeanza, viongozi wake hawana weledi, hawana mafunzo, lakini ushirika hawana mitaji na viwanda vile vya kusindika mazao vingi vimekufa.

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inapatia ushirika mitaji ili vyama hivi viweze kujiendesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa tulianzisha Benki ya Kilimo kwa ajili ya kuwakomboa wananchi na hasa wanawake na kwa kuwa vipo vikundi vingi vya wanawake vilivyoanzishwa kwenye *SACCOS* kwa ajili ya kilimo, ningependa kujua Benki ya Kilimo itafika lini kwa ajili ya kuwakopesha wanawake vijijini katika ushirika wao wa kilimo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumo wa ushirika wa *SHIRECU* na vyama vingine vya ushirika wakati ambao anaongelea Mheshimiwa Mbunge, mfumo wa uchumi ambao nchi ilikuwa inaenda nao ulikuwa ni mfumo hodhi. Kwa hiyo mfumo ule wa ushirika wa wakati ule ulikuwa ni *compatible* na zama zile na wakati ule. Sasa hivi ni mfumo wa soko, hatuwezi kurudi katika mfumo uliokuwepo wakati wa nyuma. Lakini tunachokifanya sisi kama Serikali sasa hivi ni kupitia upya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2002 wakati huohuo kupitia Sheria ya Ukaguzi ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1985 na kupitia mfumo mzima wa uendeshaji wa ushirika ili vyama vya ushirika viweze kuwa vya kibiashara na vijiendeshe kibiashara zaidi na kuwa *competitive* katika soko

ambalo ni soko huria linaloruhusu watu binafsi kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala la ushirika kupewa mitaji na Serikali; hili jambo haliwezekani. Kisera ya kiuchumi hatuwezi Serikali kuwapelekea vyama vya ushirika kupewa mitaji ya kujiendesha, lakini Serikali inachoweza kukifanya ni kuvifanya vyama vya ushirika kuwa *strong* na viweze kukopesheka na viweze kufanya biashara ili viwe vina sura ya kuendesha na kutengeneza faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Benki ya *TADB; TADB* ni *development bank* na wala siyo *commercial bank* kama benki zingine, haiwezi kufungua matawi nchi nzima, lakini pale ambapo ama chama cha ushirika au wananchi ambao wanaendesha miradi ya kilimo ya kimkakati wana *business plan* wanaweza kwenda ku-*access* mikopo katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili tuweze kuendeleza *infrastructure* ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakaelewa, *Tanzania Agricultural Development Bank* ni *development bank* na siyo *commercial bank,* haiwezi kufanya kazi za *commercial bank,* inafanya kazi za kuwekeza kwa miradi ya muda mrefu kwenye sekta ya kilimo. Kwa hiyo hawawezi kwenda kufungua matawi katika wilaya na mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu akina mama; akina mama *Tanzania Women Bank* imeunganishwa na *Postal Bank* na *facilities* za akina mama kuweza kukopeshwa mikopo midogo midogo inapatikana kupitia Benki ya Posta kwa akaunti maalum ambayo imeanzishwa kama *product* kupitia benki ile.

Kwa hiyo, ninataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge watusubiri wakati tunapitia Sheria ya Ushirika na kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa ushirika ili uweze kuendana na mahitaji ya sasa na kuwajengea imani wananchi. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa muda wetu siyo rafiki, naendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, linaelekezwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 74

**Mtaji wa Benki ya Kilimo Nchini**

**MHE. ORAN M. NJEZA** Aliuliza:-

Ili kuboresha kilimo na ujasiriamali inahitajika elimu kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuwa na vyanzo vya uhakika vya mtaji.

(a) Je, Benki ya Kilimo ina mtaji kiasi gani?

(b) Je, Benki ya Kilimo ina mkakati gani wa kuwafikia wakulima wadogo wa Wilaya ya Mbeya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipatiwa mtaji wa shilingi bilioni 60 mwezi Novemba, 2014. Aidha, tangu ilipoanza rasmi shughuli zake mwaka 2015, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefanikiwa kujiendesha na kukuza mtaji wake hadi kufikia shilingi bilioni 67.5 zilizorekodiwa mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo inakuwa na fedha za kutosha kwa ajili

ya kutoa mikopo na hivyo kufikia malengo ya kuanzishwa kwake, Serikali imeipatia benki hii kiasi cha shilingi bilioni 103 kupitia mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Aidha, kwa sasa benki inaendelea na mchakato wa kukamilisha masharti ya kupatiwa awamu ya pili ya mkopo wa shilingi bilioni 103 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imefikisha huduma zake Mkoani Mbeya na kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kutoka shilingi milioni 799.9 mwezi Desemba, 2017 hadi shilingi bilioni 2.54 kwa taarifa ya mwisho wa mwezi Aprili, 2019. Mikopo hiyo imetolewa kwa miradi saba ya kilimo na kuwanufaisha wakulima 509 wa Wilaya za Mbozi, Momba na Mbarali.

Napenda pia kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefanikiwa kufungua ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mkoani Mbeya. Malengo ya ufunguzi wa ofisi hiyo ni kuhakikisha kwamba benki inasogeza huduma zake karibu zaidi na wateja wake ambao ni wakulima wote wa Nyanda za Juu Kusini ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo wa Wilaya ya Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kuwahimiza wadau wote wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na wakulima wa Wilaya ya Mbeya Vijijini, kuwasiliana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili waweze kupata maelekezo sahihi ya uandaaji wa miradi itakayokidhi vigezo vya kupatiwa mikopo na benki yao na pia kupatiwa maelezo ya fursa nyinginezo zinazopatikana katika benki yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, na inavyoonesha Benki ya Kilimo bado ina mahitaji ya mtaji mkubwa hasa ukizingatia kuwa kilimo kwa nchi yetu ndiyo tunakitegemea kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi. Sasa ukiangalia katika jibu kwa Mkoa wa Mbeya ambayo imeoneshwa kuwa zimepelekwa shilingi milioni 700

lakini na hizi Wilaya alizozitaja Mheshimiwa Waziri siyo za Mkoa wa Mbeya ni za Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo kwa jibu hilo inaelekea kabisa Mkoa wa Mbeya haujanufaika na mikopo ya Benki ya Kilimo.

Sasa swali langu; je, ni kwa kiasi gani Serikali imeweza kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya mtaji wa Benki ya Kilimo? Na je, mtaji huo utapelekwa Benki ya Kilimo ukiondolea mbali hiyo mikopo ya *ADB* utapelekwa lini huo mtaji kwa Benki ya Kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kiasi kikubwa ukiwapa wakulima mikopo *risk* kubwa iko kwenye bei kwa sababu bei za mazao hazieleweki, kuna *risk* sana kwenye bei. Sasa kwa kiasi gani Benki ya Kilimo kwa kutumia *instruments* za kibenki na vilevile kwa kusaidiana na taasisi zingine kama *commodity exchange (TMX)* zimeweza kutengeneza utaratibu wa kuondoa hiyo *risk,* wa ku-*manage* hiyo *risk* ambayo inatokana na changamoto za bei za mazao yetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa ufupi tu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza lenye (a) na (b), tathmini ya mtaji na utapelekwa lini; tathmini ya mtaji ilishafanyika na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tunaangalia njia nyingine za ku-*finance* benki yetu ya kilimo ili iweze kuwa na uwezo wa kuwakopesha wateja wake ambao ni wakulima wadogo, wa kati pamoja na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Bunge lako tukufu likafahamu kwamba mabenki yote hayakopeshi kupitia mtaji, yanakopesha kupitia njia nyingine, *co-financing agreement,* ndiyo maana Serikali ilitafuta mkopo wa bei nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na ikaipatia Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Kwa hiyo, hilo naomba Waheshimiwa Wabunge tulifahamu; hakuna benki yoyote inayokopesha kupitia mtaji wake, inakopesha kupitia amana

na njia nyingine za utafutaji wa fedha ili iweze kuwahudumia wateja wake. Serikali ipo tayari kabisa kuiwezesha benki yetu kupitia mipango mingine ili ipate fedha za kutosha za kuwahudumia wakulima wetu ambao ndio lengo kubwa la uanzishwaji wa benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *risk* ya masoko; *TMX* ambalo ni Soko la Bidhaa Tanzania, limeanza kazi vizuri mwaka huu na tayari tumeona baadhi ya mazao kwa mfano ufuta ambao umetafutiwa soko zuri na Soko letu la Bidhaa Tanzania wameweza kutafuta masoko na sasa tunaendelea kutafuta masoko mengine kupitia Soko la Bidhaa Tanzania kwa ajili ya mazao yaliyobaki ili kuwasaidia wakulima wetu kuondokana na vihatarishi vya ukosefu wa bei au bei isiyoeleweka kwenye masoko yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na linaulizwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 75

**Viongozi wa Nje Wanaokuja na Kuahidi Kusaidia Miradi**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO** Aliuliza:-

Je, Serikali ina maelezo gani juu ya viongozi kutoka nje ya nchi wanaokuja Tanzania na kutembelea baadhi ya maeneo na kisha wanapokuta miradi ya wananchi huahidi kusaidia na baadae kushindwa kutimiza ahadi zao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ikipokea viongozi wageni kutoka nje ya nchi na makundi aina mbili yaani wa Kiserikali na wasio wa Kiserikali. Viongozi hao hutembelea Tanzania kwa ziara za kikazi na binafsi ambapo hupata fursa ya kuona miradi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kuratibu na kusimamia ziara za kikazi za viongozi wa Serikali kutoka mataifa ya kigeni ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali zinazotolewa na viongozi hao kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na taasisi za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ambazo hutolewa na baadaye kushindwa kutimizwa, Wizara huratibu vikao vya majadiliano vinavyoshirikisha wahusika pamoja na Wizara za kisekta na taasisi za Kiserikali ili kupata mwafaka juu ya suala husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wetu kuweza kuirudisha ndege yetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza litakuwa moja; je, Waziri anaweza kutuambia ni njia gani zinazotumika kwa viongozi wa Wilaya na Mikoa kufuatilia

ahadi zinazotolewa na viongozi hawa wanapokuja nchini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Tauhida kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kule Zanzibar akiwakilisha wananchi. Amefanya mambo mengi, ametoa kompyuta na kujenga madarasa ya kompyuta na amekuwa akijulikana kama ni rafiki wa wanawake na watoto. Swali lake ni ushahidi tosha kwamba anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Zanzibar inashirikiana kwa karibu kabisa na viongozi wa Wilaya na Mkoa pamoja na Ofisi ya Rais kule Zanzibar, katika kufanya vikao vya mashauriano ili kuona kwamba ahadi ambazo zimetolewa na hazijatekelezwa zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niwashauri Mheshimiwa Tauhida tuendelee kushirikiana kupitia viongozi wa Wilaya, Mkoa, Wizara za Kisekta, Ofisi ya Rais Zanzibar pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kuhakikisha kwamba ahadi zote zinatekelezwa. Kama kuna ahadi sugu ambayo haijatekelezwa nitamuomba tuonane ili tuweze kuitekeleza haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, tunahamia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi.

Na. 76

## Matukio ya Watoto Kuokota Mabomu na Kulipukiwa

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** Aliuliza:-

Kumekuwa na matukio ya watoto kuokota mabomu wakidhani ni vyuma chakavu na kisha kuwalipukia na kusababisha madhara makubwa ikiwemo vifo. Hivi karibuni watoto watano wamepoteza maisha na zaidi ya watoto 40 kujeruhiwa katika Shule ya Msingi Kihanga iliyopo Ngara Mkoani Kagera.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti na kukomesha tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi duniani yanakabiliwa na changamoto ya kutapakaa kwa kwa silaha ndogo ndogo yakiwemo mabomu ya kutupwa kwa mkono. Pamoja na Tanzania kuwa ni nchi yenye amani, baadhi ya nchi zinazotuzunguka zimejikuta zikitumbukia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hali hiyo imesababisha baadhi ya wakimbizi kukimbia na silaha yakiwemo mabomu ya kutupwa kwa mkono na kuyatekeleza baada ya kujiona wapo salama au kuwauzia wahalifu jambo ambalo limechangia kuwepo kwa mabomu hayo katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vita vya Kagera, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilitoa elimu kwa

wananchi kutookota vitu vinavyong'ara, vifaa vya chuma na pindi wanapoona vitu hivyo watoe taarifa Vituo vya Polisi au kwenye Kambi za Jeshi iliyo karibu. Kwa maeneo yaliyotiliwa mashaka wananchi walipewa tahadhari ya kutolima, kutopita au kulisha mifugo. Aidha, Jeshi la Wananchi lilipeleka Wahandisi wa Medani kukagua maeneo hayo na kujiridhisha kama yapo salama kwa wananchi kuendelea na shughuli zao za kawaida. Hivyo, inashauriwa wananchi katika mkoa huo na mingine kuendelea kuchukua tahadhari wanapoona vitu vyenye asili ya chuma.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri anakiri katika masuala yake kwamba elimu ilitolewa baada ya vita vya Kagera, lakini waathirika wakubwa katika kadhia hii ya mabomu ni watoto wadogo hasa wanafunzi wa shule za msingi. Inaonekana kabisa kwamba elimu hawajapatiwa ya kutosha au hata kama inapelekwa haiwafikii. Sasa swali langu lipo hapa; je, Serikali iko tayari kuingiza kipindi maalum katika masomo yao wanafunzi wa shule za msingi ili wapatiwe elimu ya kujikinga na mabomu na athari zake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, umiliki na udhibiti wa silaha za mabomu pamoja na silaha nyingine ni jukumu la vyombo vya ulinzi na usalama. Kwa hiyo, kutapakaa hovyo kwa mabomu kumepelekea wanafunzi wa Shule ya Kihanga, Ngara, Kagera kupoteza maisha na wengine wengi wao kujeruhiwa. Je, Serikali iko tayari kuwalipa fidia wale waliopata janga hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwanza kwamba Serikali iwe tayari kuingiza somo maalum katika mitaala ya shule za misingi, hili ni wazo zuri na linazungumzika na sisi tutaendelea kuzungumza na wenzetu wa Wizara zinazohusika na elimu ili kuweza kuona uwezekano wake. Wakati hayo yanaendelea, elimu imekuwa ikitolewa katika maeneo hususan yale maeneo ambayo yanaonekana yana matatizo na lengo ni kuwapa elimu wahusika na wao waweze kupeleka katika shule zinazopatikana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la kwamba inapotokea kwamba mtu amepata tatizo linalohusiana na mabomu au silaha nyingine mbalimbali basi walipwe fidia, niseme tu kwamba kwa kiwango kikubwa ili kuweza kuondoa tatizo hili, ni muhimu kuhakikisha kwamba elimu inatolewa. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba wahandisi wetu wa medani mara zote wamekuwa tayari kwenda katika maeneo yenye mashaka, yenye matatizo ili kuweza kuondoa mabomu haya ili kuepuka athari badala ya kujikita katika suala la kusubiri watu wapate matatizo halafu fidia zitolewe. Hata hivyo, ikithibitika kwamba aliyepata madhara haya yametokana na mabomu ya kutupwa kwa mkono ambayo hayakuweza kuondolewa kwa wakati, basi kwa kawaida fidia huwa zinatolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimwia Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea athari ya vifo au majeruhi kwa wananchi waliopata milipuko ya mabomu au kuokota mabomu, Serikali mara nyingi huwa wanatoa fidia kama kule Mbagala na Gongo la Mboto. Mheshimiwa Waziri utakumbuka kwamba kule Tunguu kuna watoto waliokota mabomu na walifariki wawili na wananchi wengine walipata majeruhi. Narudia hili kwa Mheshimiwa kwamba wale watu

wataweza kupewa fidia. Ni kwa nini basi hadi leo wale watoto wawili au na majeruhi kule Tunguu ambao walipata athari hii hawajapata fidia? Na ni lini watapata fidia yao?

**MWENYEKITI:** Jibu swali moja tu Mheshimiwa. Karibu Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea tatizo hili lililotokea Tunguu, nitamuomba Mheshimiwa Mbunge anipe uhakika wa suala lenyewe kwa maandishi ili liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 77

**Wananchi Waliopisha Barabara ya Mchepuo Tumaini – Iringa**

**MHE. RITTA E. KABATI** Aliuliza:-

Wananchi waliopisha ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Tumaini kuchepusha magari makubwa kupita katikati ya Mji wa Iringa walilipwa fidia zao baada ya muda mrefu sana kufanyiwa tathmini.

(a) Je, sheria inasemaje?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwapatia nyongeza ya fidia zao?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwongozo wa uthamini wa fidia wa mwaka 2016 na Kanuni ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2001, malipo ya fidia yanapaswa kufanyika kwa wakati ndani ya muda wa miezi sita. Endapo hayatafanyika ndani ya muda huo, malipo hayo yanapaswa kulipwa pamoja na riba. Serikali inatambua kuwa waathirika 188 wa Kata ya Igumbilo na Kihesa na makaburi 43 yalihamishwa ili kupisha ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Tumaini – Iringa. Jumla ya shilingi 4,623,369,257.11 zimetumika kulipa fidia waathirika wa mradi huo. Aidha, shilingi 14,550,500 zimetumika kuhamisha makaburi kutoka katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itawalipa wananchi riba kwa mujibu wa sheria mara fedha itakapotolewa na Hazina.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili. Kwanza nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana ambazo wamekuwa wakizifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze sana Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwa ujenzi wa mtandao wa barabara katika Mkoa wetu wa Iringa, wamefanya kazi nzuri sana. Pia kuwalipa wananchi hao fidia kwa hiyo barabara ambayo imetajwa hapo.

Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wananchi hao wanatakiwa walipwe fidia na riba,

sasa nimuombe Waziri anijulishe. Je, ni lini? Na wanalipwa bila usumbufu kwa sababu kwa kweli kwanza walitumia karibu miaka mitano kutolipwa baada ya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa changamoto ya kupitisha magari makubwa katikati ya Mji wa Iringa kumesababisha wafanyabiashara hasa wenye maduka, hoteli, migahawa kupata shida sana na wale wananchi wanaofuata huduma kwa sababu magari yao yanafungwa, kwa hiyo wanasababisha kutofanya biashara vizuri. Vilevile kumesababisha Serikali kutopata kodi ya uhakika na vilevile kuna ajali kubwa sana itakuja kutokea kwa sababu magari makubwa ya mafuta yanapita barabarani.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa leo hii uniambie na uwaambie wananchi wa Iringa ile barabara ya mchepuo kwa sababu tumeshapata ahadi nyingi sana. Kila siku, nimeuliza kama maswali matano, lini sasa mtaijenga ili kuondoa hiyo changamoto ambayo imekuwa ni tatizo kubwa mno katika Mkoa wa Iringa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu kwa maswali hayo. Ooh! Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la riba ni *commitment* ya Serikali kwamba riba hiyo kwa wananchi italipwa baada ya fedha kutolewa kwa sababu tuko mwezi wa tisa na kwa mujibu wa sheria za kifedha, mwezi wa tisa ndiyo fedha zinaanza kutolewa. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba fedha hiyo ya riba italipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usumbufu mwingine uliousema Serikali ilishaona, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba kuna umuhimu wa kuweka barabara ya mchepuo ili kuweza kuondoa hivyo vikwazo ambavyo mwenyewe umevitaja kwa wananchi. Kwa hiyo, nikuhakikishie, usanifu umekamilika na kama hatua tayari fidia tumeshalipa bado riba. Kwa hiyo sasa hivi taratibu za Kiserikali zinaendelea ili kuhakikisha barabara hiyo inajengwa haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa muda wangu mnauona, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi bado linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nikuombe tu kabla sijaomba swali langu lijibiwe kufanyike marekebisho ya jina la kijiji badala ya kusomeka Lupajo, isomeke Lupaso.

Na. 78

**Ahadi ya Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano – Lulindi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** Aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga minara ya mawasiliano ya simu katika Kata za Sindano, Lupaso, Lipumburu, Mchauru na Mapili (Chikolopola) ambazo zipo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo lisomeke Kulupaso, Kulupaso?

**MBUNGE FULANI:** Lupaso.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kuandikwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliviainisha vijiji vya Kata ya Sindano, Lipumburu, Namtona, Mchauru na Chikolopola (Mapili) na kuviiingiza vijiji vya Kata za Mchauru katika mradi uonatekelezwa na Kampuni ya Simu ya *MIC* (Tigo) ambapo vibali vya ujenzi kutoka *NEMC* vimekwisha patikana. Kata za Sindano na Lipumburu ziliingizwa katika mradi wa awamu ya tatu ambayo ilitiwa saini tarehe 15 Desemba, 2018 ambapo utekelezaji wake unategemewa kukamilika mnamo mwezi Desemba, 2019 ambapo Kata ya Sindano inafikishiwa huduma na Kampuni ya Vodacom wakati Lipumburu itafikishiwa huduma na *TTCL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vijiji vya Kata za Lupaso na Chikolopola vimeingizwa katika orodha ya miradi ya zabuni iliyotengwa mwezi Julai, 2019. Utekelezaji wa mradi unategemea kuanza mwezi Oktoba, 2019.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina maswali ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri.

Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Mapili na Namyomyo, Chikolopola, Lupaso pamoja na maeneo ya Lipumburu wamekuwa wakipata shida ya mawasiliano kwa muda mrefu sana. Ahadi ya Serikali ni kwamba kipaumbele cha kwanza ni kuhakikisha minara inajengwa hasa maeneo ya kandokando mwa vijiji vilivyomo mipakani mwa nchi yetu na nchi jirani. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la ucheleweshaji wa kupatikana vibali vya ujenzi iliyopelekea

hata kwenye jibu la msingi, kwamba mradi mmoja unasainiwa mwezi Desemba, 2018 lakini unakuja kumalizika kutekelezwa Desemba, 2019.

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inaondoa tatizo la urasimu wa upatikanaji wa vibali ili minara ijengwe kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuahidi kwamba katika Bunge lililopita kwamba atatembelea vijiji hivi vilivyopo mpakani mwa Tanzania, Msumbiji ili kuzungumza na wananchi. Je, yupo tayari sasa baada ya Bunge hili kutembelea vijiji hivyo pamoja na Kijiji cha Lupaso ambacho Kiongozi Mkuu wa nchi mstaafu ndiyo nyumbani kwake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Aah Waziri mwenyewe *Engineer* Isack Kamwelwe.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru Bunge lako tukufu ambalo lilitunga Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Mfuko huu utahakikisha kwamba sasa nchi nzima inakuwa na mawasiliano. Ijumaa nilikuwa na mkutano na watoa huduma wote wa mawasiliano tukizungumzia miradi ya kata 521. Tumekubaliana baada ya wiki mbili tunakutana, kwa hiyo, hayo majibu ya msingi yaliyotolewa Mheshimiwa Bwanausi, vijiji vyote hivyo vyote vitapata mawasiliano na hiyo ndiyo ahadi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili la vibali, suala la vibali sasa hivi halina mgogoro tena, *NEMC* wamejiandaa vizuri tukiomba vibali tunavipata haraka. Ufumbuzi wa kutoka vibali haraka ulitokana na mradi wa makaa ya mawe pale

Mtwara, Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba sasa vibali vinatakiwa vitoke haraka na sasa vibali vinatoka haraka hakuna kikwazo tena cha kutoka vibali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge naendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 79

**Fidia kwa Wananchi wa Kipunguni**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** Aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mchakato wa kulipa fidia kwa wananchi wa Kipunguni waliotakiwa kusitisha kuendeleza maeneo yao ili kupisha upanuzi wa kiwanja cha ndege?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (ELIAS J. KWANDIKWA)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonist, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa wananchi 1,182 eneo la Kipunguni yaani wananchi 381 Kipunguni Mashariki na wananchi 801 Kipunguni A ambao maeneo yao yalifanyiwa uthamini kwa ajili ya kulipwa fidia baada ya maeneo hayo kuwekwa kwenye mpango wa kutwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* kufuatia mradi wa maboresho ya miundombinu na

usalama wa Kiwanda cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam yanayoendelea kufanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao maeneo yao yapo kwenye eneo la mradi kuwa Serikali itawalipa fidia pale itakapotenga fedha kwa ajili ya mradi husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Anatropia Theonist.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitoe masikitiko kwamba leo ni mara ya nne ninauliza swali kuhusu kulipwa fidia kwa wananchi wa Kipunguni. Leo najibiwa kwa mara ya nne, mara ya tatu majibu yalibadilika nikaambiwa wangelipwa kwa mwaka wa fedha ulioisha, lakini kwa jibu la leo naona tumerudi nyuma. Serikali inasema watalipwa pale itakapopata fedha, sio sahihi kabisa hawa wananchi wamezuiwa kuendeleza maeneo yao kwa muda mrefu. Wananchi wengi wanakufa, wengine wanashindwa kujiletea maendeleo ni changamoto kubwa sana. Sasa swali langu halijajibiwa ni lini hawa wananchi watalipwa fidia kwa kuwa tuliambiwa wangelipwa mwaka jana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili zaidi ya wananchi 322 walienda mahakamani baada ya kutoridhishwa na mchakato ambao ulikuwa ni pamoja na kutolipwa viwango stahili na kutokubalina na tathimini.

Sasa Serikali ipo tayari kurudi na kuongea na wananchi hawa waondoe kesi mahakamani wafanyiwe tadhimini upya ili walipwe stahili zao sambamba na tathimini ya sasa ili wapate faida ya maeneo yao? Naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali haya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwele.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mbunge Anatropia kuhusiana na fidia ya Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitajibu swali la mwisho, suala la mahakamani kwa sababu wao wameenda mahakamani hatuwezi kulizungumza humu Bungeni. Niombe Mheshimiwa Mbunge tuache hatua za kimahakama ziendelee, *ruling* inatakapokuwa imekuja basi sisi ndio tutaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu fidia ndio utaratibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalipa fidia pale ambapo inatekeleza mradi. Awamu ya kwanza tulikuwa tunajenga *Terminal III* tulilipa fidia kupata lile eneo na ukuta tumejenga. Tutakapohitaji kufanya maendelezo ya ule mradi tena kama ambavyo jibu la msingi limesema basi tutaendelea, tutachukua hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli kwamba tumezuia wananchi wasifanye maendelezo katika eneo ambalo tumeli-*earmark* kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Na hilo sio kwenye uwanja tu hata kwenye barabara. Kwa hiyo, tunafanya hivyo ili serikali pia isiingie gharama kubwa wakati wa ujenzi wa barabara wakati wa fidia.

Kwa hiyo, nikujibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo makini itahakikisha kwamba pale ambapo inatekeleza mradi watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba yake. Yupo? Oooh Maria karibu.

Na. 80

**Hitaji la Maji Vijiji vya Mwanza Kupitia Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** Aliuliza:-

Kumekuwa na mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuelekea Mikoa ya Shinyanga na Tabora vyenye mitambo yake chanzo cha maji kule Ihelele Wilayani Misungwi, aidha maeneo yanayozunguka mitambo hiyo na yanayopitiwa na mabomba ya mradi huo hayana maji safi na salama.

Je, nini mpango wa Serikali kusambaza maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria kwa wananchi wa vijiji vya Mkoa wa Mwanza hususan maeneo yanayopitiwa na bomba hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo linaelekezwa kwa Wizara ya Maji Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa wa Victoria, Serikali ililenga kufikisha maji katika miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji vyote vilivyopo kando ya bomba kuu la kusafisha maji. Kwa wakati huo vijiji vilivyokidhi na kuingizwa katika mradi huu vilikuwa ni vijiji vilivyopo umbali usiozidi kilometa tano kwa kila upande wa bomba kuu. Hivyo, jumla ya vijiji 39 vikiwemo vijiji vitano vya Mawile, Ilalambogo, Lubili, Isenengeja na Ibinza vya Wilaya ya Misungwi katika Mkoa wa Mwanza viliunganishwa na vilianza kupata huduma a maji tangu uendeshaji wa mradi ulipoanza mwezi Februari, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha maji na mitambo ya kusafisha maji kwa mradi wa Kahama - Shinyanga iko katika kijiji cha Nyang'ohomango. Aidha, eneo hilo pia linapakana na vijiji vya Lubili, Isesa, Igenge na Mbalika. Kwa kutambua umuhimu wa maeneo haya kuwa na huduma ya majisafi na salama kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilianza ujenzi wamradi wa maji vijiji vya Nyang'ohomango, Isesa, Igenge na Mbalika kwa gharama ya shilingi bilioni 6.1.

Aidha, fedha za kutekeleza mradi huu zinatolewa kwa asilimia mia moja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inatarajiwa kuwa baada ya ujenzi huo kukamilika, jumla ya wananchi 14,606 wa vijiji hivyo na mifugo yao watanufaika na huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huu kutawezesha pia kuunganishwa kwa mradi wa maji unaoanzia kwenye kijiji cha Mbalika kwenda katika mji wa Misasi katika Wilaya ya Misungwi ambao pia utahudumia ziadi ya vijiji kumi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nianze kwa kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo inaonesha jitihada ya kusambaza maji ndani ya Mkoa wa Mwanza. Pamoja na majibu hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji alivyokuja Misungwi aliahidi kukamilisha malipo ya mkandarasi mradi huu tajwa hapa wenye gharama ya shilingi bilioni 6.1. Lakini mpaka sasa hivi kwa taarifa niliyonayo ni kwamba kuna sintohamu nyingi, mimi ombi langu moja ningependa kujua ni lini Waziri atapata muda wa kuambatana na mimi pamoja na Mbunge wa Jimbo ili tuende tukae na makandarasi na wananchi ili tupate jibu sahihi ya lini watapata maji safi na salama?

(ii) Mara ya Mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotembelea Misungwi aliahidi mradi wa maji wa Misungwi pamoja na Igokelo kukamilishwa na kukabidhiwa mwezi wa tano. Ikasogezwa ikawa ni mwezi wa nane, leo hii tunavyongea ni mwezi wa tisa. Ningependa kujua ni nini mpango wa Serikali wa kukamilisha mradi huu ili wananchi wa Misungwi waweze kupata maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa ufupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli Mheshimiwa Maria Kangoye ni Mbunge king'anga'nizi katika kutetea wananchi wake. Lakini niungane pamoja na Mheshimiwa Kitwanga kwa kazi kubwa wanaifanya katika Jimbo la Misungwi kubwa ambalo ninachotaka kusema utekelezaji wa mradi wa maji unategemea na fedha nataka nimhakikishie mkandarasi anayetekeleza mradi ule shilingi bilioni 6.1 sisi kama Wizara ya maji hatutakuwa kikwanzo na Mheshimiwa Mbunge na kuhakikishia *certificate* ile na mradi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kuhusu utekelezaji wa mradi pale Misungwi tuna mradi takribani shilingi bilioni 12 kutokana na kilio cha Mheshimiwa Mbunge Mzee wangu Kitwanga. Wiki ijayo tunakwenda kukabidhi mradi ule ili wananchi waweze kupata maji, na ninataka kumtia moyo Mheshimiwa Kangoye na Mheshimiwa Kitwanga unapotembea na kuzuru wengine naomba usinipite mwokozi, sitowapita nitakuja mwenye Misungwi kushuhudia namna gani wananchi wanaenda kupata maji wiki ijayo. Ahsante sana Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kitwanga.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna mradi mwingine ambao umekuwepo kwa muda mrefu sana; mradi wa kutoa maji katika Ziwa Victoria

sehemu ya Butimba kupeleka Wilaya ya Ilemela, vilevile kuleta Usagara Wilaya ya Misungwi pamoja na Kisesa Wilaya ya Magu. Kumekuwa na muda mrefu sana tunaambiwa watasaini mkataba. Naomba basi nifahamu leo hii ni lini mkataba utasainiwa na mradi huo uanze haraka iwezekanavyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso ni lini mradi huu utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli Mheshimiwa Kitwanga ni miongoni mwa Wabunge ambao ni wafuatiliaji ususani mambo yanayohusu wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Mheshimiwa Kitwanga sio mara moja analizunguzia hili jambo, nataka nimhakikishie serikali ya awamu ya tano ni serikali ya matokeo sio serikali ya mchakato. Na kwa kuwa sisi tupo karibu sana na Wizara Fedha nikuombe Mheshimiwa Mbunge nikuombe hebu tukutane leo ili tukae na wenzetu wa Wizara ya Fedha hili jambo tuweze kukalisha na wananchi wako waweze kupata huduma hii muhimu sana safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kiza Mayeye, Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Bupe.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona naomba kuliza swali kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Kigoma Vijiji ina vijiji cha Mwandiga, Kiganza, Bitale, Mkongoro na Msimba ambavyo mpaka sasa wananchi wanateseka kwa kukosa maji, kipundupindu ni cha kwao, lakini kina mama hata ndoa zao zinakwenda kuhatarika.

Ni lini sasa mradi wa Ziwa Tanganyika na ule wa Kigoma Manispaa utafika katika vijiji hivi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Maji kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kubwa tunapozungumzia maji, maji ni uhai na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatupo tayari kupoteza uhai wa wana Mwandiga. Mheshimiwa Mbunge nilivyokuja ziara katika yetu Peter Serukamba alipiga kelele sana kuhusu suala la kupelekewa fedha ili tutekeleze maji na Mheshimiwa Waziri ametuma fedha tayari na ile kazi itatekelezwa na watalaamu wetu wa ndani katika kuhakikisha wana Mwandiga wananufaika na mradi wa uwepo wa Ziwa Tanganyika kati eneo hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chegeni Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanatia matumaini mazuri. Napenda kufahamu mradi wa maji wa kutoka Bukabile katika Wilaya ya Busega kwenda katika Wilaya za Bariadi Itilima, Meatu na Maswa ni lini mradi huu utaanza kutelezwa, licha kwamba fedha zilishapatikana na mpaka sasa hivi tuliambiwa mwezi wa tisa tutasaini mkataba lakini mpaka sasa hivi hatujasaini mkataba wowote. Nataka kujua ni lini mradi huu sasa utaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi kubwa sana. Lakini pia napenda nimfahamishe kwamba mkataba tumekwisha kusaini mradi ule na nikuombe Mheshimiwa

Mbunge kutokana na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri ambayo ameitupia jicho katika Mkoa ule wa Simiyu ni kuombe tuweze kukutana tuweze kupeana *update* lini tutaweza kuutekeleza ili wananchi wako waweze kupata huduma ya maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Shida iliyopo Mwanza ni sawa na shida iliyopo Mkoani Rukwa, Wilaya Sumbawanga Vijijini Kata ya Kaengesa katika vijiji vya Mkunda, Kaengesa B, Kaengesa A na Italima na vijiji vyote vya wilaya Sumbawanga vijiji.

Ni lini sasa Wizara itapeleka maji katika vijiji hivyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante ni lini sasa mtapeleka maji katika vijiji hivyo Kaengesa na kwingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake, lakini kubwa ambacho ninachotaka kusema jukumu la wananchi kupata maji ni jukumu letu sisi Wizara ya Maji na nilishasema si mara moja si mara mbili, sisi ni Wizara maji si Wizara ya ukame tumepata fedha ambazo tumetengewa zaidi ya shilingi bilioni 301 na uwanzaishaji huu wa wakala wa maji vijiji kwa maana ya *RUWASA* tumejipanga miradi mingi katika kuhakikisha tunaitekeleza kutumia wataalamu wetu wandani, nimhakikishie Mheshimiwa Bupe sisi kama Wizara ya maji vijiji ambavyo ameainisha tunajipanga kuhakikisha tunavitatua ili wananchi wake waweze kupata huduma maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea Waheshmiwa Wabunge swali linalofuata bado linaelekezwa Wizara hii ya Maji linaulizwa na Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini.

Na. 81

**Mradi wa Maji katika Jimbo la Morogoro Mjini**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** Aliuliza:-

Serikali iliahidi kuleta mradi wa maji katika Jimbo la Morogoro Mjini ambao utamaliza kero ya maji katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kihonda, Tungi, Lukombe na Mkundi katika Kata ya Mindu.

(a) Je, ni lini mradi huo utaanza?

(b) Je, mradi huo unategemewa kugharimu kiasi gani?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi kutekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Morogoro Mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro *(MORUWASA)* imeandaa mipango ya muda mfupi na mrefu. Katika mipango ya muda mfupi katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Kata za Kihonda na Mkundi. Mradi huo umegharimu kiasi cha shilinigi bilioni 1.9 na umewanufaisha wakazi wapatao 17,000 wanaoishi maeneo ya Kihonda, Kilimanjaro, Kiyegea na Kihonda Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupita Shirika lake la Maendeleo la *AFD* itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji safi katika Manispaa ya Morogoro. Kazi zitakazotekelezwa ni kuongeza kina cha Bwawa la Mindu, ujenzi wa mtambo wenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji, upanuzi wa matandao wa kusambazi maji, ukarabati wa mabwawa ya majitaka. Gharama ya mradi huo ni Euro milioni 70. Taratibu zakusaini mkataba wa kifedha zinaendelea na zitakapokamika utekelezaji wa mradi utaanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Abood.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza nilitaka kujua mradi wa maji wa Kihonda na Mkundi ambao unaunganisha Mitaa ya Yespa, Kilimanjaro umeshaanza; tunataka kujua ni lini utakamika kwa sababu umechukua muda mrefu mpaka sasa haujakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mradi wa Maji wa *AFD* ambao utagharimu Euro milioni 70 Morogoro kama unavyojua kuna kero kubwa za maji; sasa nilitaka kujua ni lini utasainiwa ili uanze kazi uwakombe wananchi wa Morogoro Mjini?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji nimpongeze Mheshimiwa Abood ni miongoni mwa Wabunge ambao wachapakazi na amekuwa ni mfuatiliaji mkubwa sana hususan changamoto zinazohusina na wananchi wake, lakini kubwa ambacho ninachotaka kusema pamoja na

changamoto zipo jitihada ambazo sisi kama Serikali tunazozifanya katika Mkoa ule kwa maana ya Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa Kilimanyari Yespa mradi takribani milioni 715 ambazo tunatekeleza nimwagize Meneja kwa maana Mkurugenzi wa *MORUWASA* kuhakikisha mradi ule unakamilika kwa mujibu wa mkataba ili wananchi wale waweze kupata huduma ya maji. Na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Abood baada ya Bunge nitafika eneo lile kujionea utekelezaji wa mradi ule. Lakini kikubwa kuhusu la huu mradi huu mkubwa kwa maana kuondoa tatizo la maji Morogoro wa Euro milioni 70 ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ukiona giza linatanda ujue kuna kucha.

Mheshimiwa Abood jana sisi tumefungua *tender document* kwa maana ya kuwapata wataalam wa ushauri ili kuhakikisha mradi ule unaweza kuanza na wananchi wako wanapata maji. Ahsante sana

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru, ninaomba niulize swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo kwenye hatari kubwa la kupoteza fedha takribani shilingi bilioni moja na milioni 600 kutokana na mkandarasi wa Mradi wa Mbuta kuvunja mkataba, lakini vilevile mkandarasi wa Mwakijembe kuamua kusimama kufanya kazi kwa sababu ya uchelewashaji wa fedha.

Ni lini Serikali itachukua hatua za haraka kuhakikisha inaokoa fedha hizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Dastan Kitandula kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika jimbo lake pale Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti sisi kama Wizara ya Maji tulishasema kwamba hatukuwa na kisingizio chochote, kwamba sasa hivi mmetupa rungu kwa maana uazishwaji wa *RUWASA* kwa maana Wakala wa Maji Vijijini na tumejipanga vizuri kwa maana agizo la Mheshimiwa Waziri kwa maana baadhi ya miradi ya tutaifanya kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumhakikishi katika Mkandarasi yule aliyeondoka *site* hatuna nafasi tena ya kubembelezana ile kazi tutaifanya kupitia wakala wetu wa maji kwa maana ya Uchimbaji wa Maji Visima *(DDCA)* nawaagiza waende kuifanya kazi ile mara moja ili wananchi waweze kupata maji. Lakini kuhusu mkandarasi ambaye ametekeleza mradi hajalipwa *certificate,* nataka nimhakikishie ndani ya mwezi huu wa tisa tutamuweka katika orodha ili kuhakikisha kwamba tunamlipa ili wananchi waendelee kutekelezewa mradi wa maji, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza, Mheshimiwa Semuguruka na Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana katika Manispaa ya Mtwara Mikindani yaani Jimbo la Mtwara Mjini kumekuwa na tatizo kubwa la maji kutoka yenye tope jingi kwa muda mrefu na maji hayo yanapita katika mita za wananchi kuwasababishia kulipa bili wakati maji wanayoyapata ni machafu. Pamoja na mambo mengine chanzo kikubwa ni kukosekana kwa chujio katika chanzo cha maji cha Mtawanya.

Swali langu, ni lini Serikali itanunua chujio kubwa la uhakika kwa ajili ya kuchuja maji katika chanzo cha Mtawanya ili kusudi wananchi wanaoishi Mtwara Mikindani wapate maji safi na salama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji niseme kwa ufupi sana ni wajibu na ni haki ya mwananchi kupatiwa maji, si maji tu kwa maana yamaji safi na salama na yenye ubora. Nimefika Mtwara lakini moja ya changamoto kubwa pale ni chujio na nitumie nafasi hii kumwagiza Katibu Mkuu wa Wizara yetu ya Maji kuhakikisha mchakato ule unakamika haraka kwa ajili ya ujenzi wa chujio na wananchi wa Mtwara waweze kupata maji safi salama na yenye ubora. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Semuguruka, Mheshimiwa Mangungu, Mheshmiwa Masala.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupatikana Mkandarasi wa Mradi wa Lwakajunju katika Jimbo la Karagwe lakini bado wananchi wa Karagwe hawajajua ni lini mkandarasi huyo atakwenda kuanza. Je, ni lini utekelezaji wa Mkandarasi wa maji wa Lwakajunju utaanza ili kuwatua ndoo wakina mama?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Lini? Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa jasiri, mpambanaji kwa wanawake wenzake kwa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusema sisi kama Wizara ya Maji na kupitia Mheshimiwa Rais tunamshukuru sana tumepata fedha zaidi ya dola milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa miradi katika miji 28 lakini tunashukuru

jitihada kubwa ambazo zimefanyw ana Waziri wetu kwa maana ya Mheshimiwa Mbarawa kuhakikisha Mhandisi Mshauri amepatikana kwa haraka na ameshapita katika miji yote sasa hivi tunakamilisha *document* kwa maana ya kupata kibali ili kumpata mkandarasi na ujenzi wa mradi ule uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kaka yangu Bashungwa siis Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha mkandarasi anapatikana kwa wakati na utekelezaji wa mradi wa maji kwa maana ya kumtua mwanamama ndoo kichwani unaanza mara moja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri ulitembelea Jimbo la Mbagala kwenye mradi wa Mgembaki pamoja na Kiwika na ulitoa maagizo kwa sababu miradi hiyo inaendeshwa kiufanisi, wananchi ambao walichangia miradi ile pamoja na Wizara pamoja na watu wa *DAWASA* wakae pamoja ili waangalie jinsi ya kuiendesha kwa ufanisi, lakini cha ajabu watu wa *DAWASA* wameingia kule na wanataka kuchukua vyanzo vile bila kushirikisha Kamati zile za wananchi na kuacha kabisa maagizo uliyoyatoa.

Je, utakuwa tayari sasa turudi tena kwa wananchi wale na *DAWASA* ili tuweze kuangalia jinsi gani ya kuendesha miradi ile kwa maridhiano?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mbunge unafanyakazi kubwa na sisi kama Wizara ya Maji

hatuwezi kuwa kikwazo, nipo tayari kuongozana na wewe. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri moja ya ziara ambazo umezifanya Jimbo la Nachingwea ni katika Kata ya Mbondo, Kijiji cha Chimbendenga. Sasa hivi ni takribani miezi minane toka uondoke ule mradi mpaka sasa hivi haujakamilika. Naomba kufahamu *commitment* ya Wizara juu ya kukamilisha mradi wa maji Chimbendenga?

**MWENYEKITI:** Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kiukweli nimefika Nachingwea nimejionea kazi kubwa ambazo anazozifanya siyo katika maji tu hata katika maeneo mengine, lakini kikubwa ambacho ninachotaka kusema moja ya changamoto kubwa sana katika sekta yetu ya maji kulikuwa na wakandarasi wengi wababaishaji lakini hata hao wanaotekeleza wamekuwa katika kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuna nafasi kama Wizara ya Maji kubembeleza watu. Tunawaomba Wakandarasi wafanyekezi kwa wakati na sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuwalipa fedha zao katika kuhakikisha wanakamilisha miradi ya maji. Ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutafanya mawasiliano na wenzetu wa Nachingwea, tukiona mkandarasi anafanyakazi kwa kusuasua tutamnyang'anya kazi tutaifanya kwa wataalam wetu wa ndani ili mradi wetu uweze kukamilika na wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea muda umekwenda sana. Swali linalofuata linaliulizwa na Mheshimiwa Lijualikali, Mbunge wa Kilombero.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Lijualikali...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Wewe acha hiyo biashara.

**MBUNGE FULANI:** Hamna toka zako.

Na. 82

**Ujenzi wa Gereza Wilaya ya Kilombero**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA (K.n.y. MHE. PETER A. LIJUALIKALI)** Aliuliza:-

Jeshi la Magereza lilikuwa na mpango wa ujenzi wa Gereza Kitongoji cha Nakato na Kijiji cha Kibaoni, Wilaya ya Kilombero.

Je, mpango huu umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilombero ni miongoni mwa Wilaya 51 nchini ambazo hazina magereza. Mpango wa kuwa na magereza katika kila Wilaya una lengo la kupunguza tatizo la msongamano kwenye baadhi ya magereza yanayopokea wahalifu kutoka Wilaya zisizokuwa na magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuwa na magereza kila Wilaya utarahisisha usikilizwaji wa kesi,

wafungwa na mahabusu wataweza kupata huduma kwa urahisi kutoka kwa mawakili wao na pia kupunguza gharama za usafiri kwa ndugu zao wanapowatembelea magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Magareza ina mpango wa kujenga magereza kwa Wilaya ambazo hazina magereza nchini ikiwemo Wilaya ya Kilombero. Aidha, mpango huu utatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa na msongamano mkubwa sana kwenye magereza mbalimbali hapa nchini na hasa ukiangalia kwa mfano kama Gereza letu la Ilembo pale Vwawa wafungwa wanaotakiwa kukaa pale pamoja na mahabusu ni 120; lakini mpaka sasa hivi kuna mahabusu pamoja na wafungwa zaidi ya 400 na hili limekuwa ni tatizo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua haya magereza kutokana na mrundikano huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwa na matatizo makubwa sana katika magereza haya, hakuna zahanati katika magereza yetu na kumekuw ana tatizo kubwa sana la wafungwa kutolewa kwenye haya magereza na kupelekwa kwenda kutibiwa katika hospitali mbalimbali hapa nchini wakati huo magereza hawana magari.

Serikali ina mpango gani wa kujenga zahanti katika magereza yetu yote hapa nchini ili wafungwa na mahabusu katika maeneo haya wawe wanatibiwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna utaratibu wa kujenga magereza mapya, kuongeza mabweni na kupanua kadri ya hali ya fedha inavyoruhusu. Kwa mfano, katika kipindi cha karibuni tumekamilisha ujenzi wa Gereza la Ruangwa, Gereza la Chato lakini pia na kufanya uongezaji wa mabweni katika magareza kadhaa nchini, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo hali itaruhusu na Gereza la Vwawa vilevile nalo tutafanya upanuzi wa gereza hilo ingawa upanuzi wa magereza siyo njia pekee ya kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka hivi karibuni, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kutokana na dhamira yake ya dhati ya kuwatumikia wananchi wa nchi hii hususani wanyonge na hasa pale katika jitihada zake za kuona kwamba wanyonge wa nchi hii hawaonewi, alivyofanya ziara katika Gereza la Butimba hivi karibuni alitoa maelekezo nchi nzima ambayo yameshaanzakufanyiwakazi na yamesaidia sana kupunguza idadi ya mahabusu ambayo kimsingi msongamano huu kwa kiwango kikubwa unasababisha na mahabusu ambao ni wengi wakati mwingine wanapita hata idadi ya wafungwa.

Kwa hiyo, baada ya maelekezo yale na hatua ambazo mbalimbali zimechukuliwa sasa idadi ya mahabusu imeendelea kupungua nchini na hivyo kupunguza msongamano.

Lakini kwenye eneo hili la pili la zahanati, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna utaratibu katika magereza yetu yote kuwa na madakrati pamoja na zahanati.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba katika maeneo ambayo tunaona labda kuna upungufu wa nguvukazi ya madaktari pamoja na madawa tufanye jitihada za kuongeza ili tuweze kukabiliana na changamoto ya wafungwa wetu na mahabusu ambao wanahitaji matibabu katika magereza. Kwa hiyo, hii kama katika Gereza la Vwawa ni changamoto nitalichukua na nifuatilie ni la ukubwa kiasi gani na tuweze kuchukua hatua stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni Waheshimiwa tunaendelea. Swali letu la mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini na linaelekezwa kwa Waziri wa Nishati.

Na. 83

**Utekelezaji wa Mradi wa REA III (1) Jimbo la Tabora Kaskazini**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** Aliuliza:-

Mradi wa *REA III(1)* unatekelezwa katika Jimbo la Tabora Kaskazini kwa kasi ndogo na mpaka sasa ni vijiji vitatu tu kati ya vijiji 82 ndiyo vimewashwa umeme.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kumfanya mkandarasi akamilishe kuwasha umeme katika vijiji vyote 18 vya *REA III(1)?*

(b) Kwa vile kwa makosa Mradi wa *REA III(1)* unarudiwa kupelekwa katika Kijiji cha Upuge, Kata ya Upuge ambako umeme ulishapelekwa na *REA III.* Je, ni lini sasa umeme utapelekwa katika Kata ya Ikongolo ambako ni Kata jirani na Kata ya Upuge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almasi Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatekeleza mradi wa kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini vikiwemo vijiji vya Jimbo la Tabora Kaskazini. Katika Jimbo la Tabora Kaskazini, Vijiji 18 vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III(1)* unaoendelea kutekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya *JV Pomy Engineering Company Limited, Intercity Builders Limited* na *Octopus Engineering Limited.* Ili kuhakikisha mkandarasi anakamilisha kazi za kuwasha umeme katika vijiji 18 vinavyofanyiwa kazi, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* pamoja na *TANESCO* wameimarisha usimamizi wa kazi za kila siku za mkandarasi na kumtaka mkandarasi kuwa na vifaa kwa ajili ye ujenzi wa mradi kutoka ndani ya nchi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Kata ya Ikongolo vinavyojumuisha Kanyenye, Kiwembe na Majengo vitapelekewa umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa *REA III(2)* utakaoanza mwezi Januari, 2020. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vya kata hizo utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *kilovolt 33* yenye urefu wa kilometa 36.14, njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 20.28, ufunguaji wa transfoma tisa za *KVA 50* na *KVA 100* pamoja na kuwanungnishia umeme wateja wa awali 614 na gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 2.29.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na juhudi kubwa inayofanywa na Waziri wa Nishati ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa vile katika mradi huu wa *REA III* uliokuwa na vijiji 18 katika Jimbo langu ni vijiji vinne tu ndiyo vimepata umeme mpaka sasa. Je, ni lini vijiji vyote 18 vitapata umeme?

(ii) Kwa kuwa Jimbo langu lote la Tabora Kaskazini lenye vijiji 82 ni vijiji saba tu ndiyo vimepata umeme. Napata wasiwasi kama kweli umeme utaenea karibu vijiji vyite 82. Je, Serikali inawahakikishia wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwamba vijiji vyite 82 vitapata umeme?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:**Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Endelea.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi la Mheshimiwa Almas Maige, lakini zaidi nimpongeze sana Mheshimiwa Maige anavyofuatilia masuala ya umeme katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mwaka 2015 Jimbo zima la Tabora Kaskazini halikuwa na kijiji chochote chenye umeme lakini kwa juhudi kubwa alizofanya Mheshimiwa Maige kufuatilia upatikanaji wa umeme hadi sasa tuna zaidi ya vijiji saba vina umeme. Kwa hiyo, nipende kumpongeza Mheshimiwa Maige lakini niwaombe wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini wawe na imani na Serikali kwa sababu vijiji vyote 82 vitapelekewa umeme ifikapo mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake mawili ya nyongeza kuhusiana na vijiji 18 ni lini vitapate umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mkandarasi anaendelea na vijiji vingine pamoja na kwamba ameshawasha vijiji saba alivyotaja Mheshimiwa Mbunge lakini tarehe 25 mwezi huu, mkandarasi atawasha vijiji vingine vine ikiwemo Kijiji cha Ibushi, Kagera ya Nsimbo, Majengo ambako Mheshimiwa Mbunge unatoka kwenye Kata ya Ikongolo pamoja na Mputi navyo vitawashwa umeme tarehe 25 mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 15 mwezi ujao vijiji vingine vitawashwa umeme ikiwemo Kijiji cha Mkalya, Mpenge pamoja na Ngokoro. Kwa hiyo niwape taarifa wananchi ambavyo Mheshimiwa Mbunge anavyofanya kazi vijiji vyote vya Tabora Kaskazini vitapelekewa umeme ifikapo Juni mwaka 2020/2021.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote napenda niipongeze Wizara ya Nishati hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kuifanya Tanzania inayomeremeta. Umeme ni maendeleo, umeme ni uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini kwenye Kata ya Kitumbikwela ambapo kuna Kijiji cha Sinde na Mnali itapatiwa umeme wa *REA* na maeneo mengine yote yaliyosalia hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa mama yangu Salma Kikwete, Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Kwanza nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya kutokana na heshima aliyopewa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli katika Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Pwani, lakini swali lake limejielekeza kuulizia Kata ya Kitumbikwela, Vijiji vya Sinde na Mnali ni lini vitapata mradi wa *REA.* Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mama Salma, natambua hii ni changamoto ambayo aliwasilishiwa alipofanya ziara lakini tumefanya mawasiliano na *TANESCO* kwa kuwa tuliwapa maelekezo ya kubaini maeneo ambayo yanaweza yakapelekewa miundombinu ya umeme kupitia kwao *TANESCO* na wamebaini maeneo 754. Moja ya maeneo ambayo wamebaini ni eneo la Kitumbikwela na kwa bajeti

ya *TANESCO* ya mwaka 2019/2020 eneo hilo na vijiji ambavyo amevitaja ikiwemo Mnali vitapatiwa umeme katika kipindi hiki.

Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na maeneo ambayo Lindi yamesalia kati ya vijiji 150, Mkandarasi *State Grid* anaendelea na kazi na tutaratajia ifikapo Disemba, 2019 kazi itakamilika. Kwa hiyo niwape moyo Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Waheshimiwa Wabunge wote akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwamba kazi ya mkandarasi inaendelea na tutamsimamia vizuri ili akamilishe. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninakiri kutambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii kuhakikisha kwamba maeneo mengi yanapata umeme na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni dogo tu, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa nguzo kwa wateja wapya hasa kwenye Jimbo la Nyamagana, lakini pia ni lini sasa Serikali itahakikisha Nyamagana ambayo inajengeka kwa kasi kubwa sana kwenye maeneo yote kuanzia Kishiri, Fumagira, Rwanima, Bwigoma na Maina watapata umeme wa uhakika kabla hatujafika kwenye mwisho wa mwaka tuliokusudia? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi tu Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:**...napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Ni kweli, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nyamagana mwaka jana tulifanyakazi kubwa sana kuhakikisha wananchi wa mitaa yote ya Nyamagana wanapata umeme na hivi sasa tunavyoendelea kuzungumza vijiji na maeneo ya Kishiri, Fumagira, Buhongwa pamoja na Nyamagana yote kuna wakandarasi wanne wanaofanyakazi na nguzo zaidi ya 2000 zitaondoka tarehe 18 mwezi huu kwenda kufanyakazi Nyamagana. Niwaondoe wasiwasi wananchi na wakandarasi nguzo zipo za kutosha hapa Nchini kuliko hata mahitaji yetu. Kwa hiyo kazi zitafanyika na Nyamagana nzima itapata umeme. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumekula sana muda wetu. Niendelee kushauri bahati mbaya majibu yameanza kuwa marefu tena sasa sitaki kutaja Wizara, lakini *Chief Whip* wa Serikali naomba mliangalie tena hili. Tulikuwa tumeanza vizuri sana, lakini unajua ziko Wizara kama tatu ambazo ndiyo zimetusaidia kubeba kuwapa nafasi Wabunge wengi kuuliza maswali, lakini kuna Wizara kama tatu zimetumalizia sana muda wetu, tuzingatie hilo.

Wageni tulionao Bungeni leo; wageni wa Mheshimiwa Spika leo ambao ni kwenye *Speaker's Gallery* ni Dkt. Edmund Mndolwa, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazai Tanzania CCM ambaye pia Dkt. Mndolwa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Posta Nchini, karibu sana Dkt. Mndolwa. Huyo ni mtaalam sana wa mahesabu, mhasibu wa siku nyingi sana, *auditor* wa siku nyingi sana. Karibu sana Mheshimiwa Mndolwa. *(Makofi)*

Katika timu yake ameambatana na Ndugu Ngaita Edward, Msaidizi wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Bwana Sabasaba Moshingi, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Posta, Ndugu Nesika Mapunga Ngongi, Mkurugenzi wa Sheria na Katiba Benki ya Posta na pia Ndugu Henry Bwogi, Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya Posta. Karibuni sana. Benki hii inatanuka vizuri, itumieni Waheshimiwa Wabunge na wananchi wetu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 12 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mbunge) Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka *St. Christina Girls School* iliyoko Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu William Sungura. Karibuni sana. Mmependeza kweli kweli, someni vizuri kwa weledi, umakini na kwa nidhamu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa George Simbachawene (Mbunge) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kutoka Mpwapwa wakiongozwa na Ndugu Wilfred Munogecha, wageni wa kutoka Kibakwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni viongozi wa kikundi cha *Mkulima Smart Initiative,* Tanzania toka Jijini Dodoma. *Smart Initiative,* karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Pascal Haonga, Mbunge kutoka Mlowa, Mbozi Mkoa wa Songwe ambao ni Ndugu Mosses Krom na Ndugu Rosina Kalupande, karibuni sana. *(Makofi*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Najma Giga kutoka Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Ndugu Bashiri Kambarage, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Amina Mollel (Mbunge) ambao ni viongozi wa watu wenye ulemavu kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ndugu Ndekira Pallangyo. Arusha karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Martin Msuha (Mbunge) ambao ni ndugu zake kutoka Mbinga, Mkoa wa Ruvuma Ndugu Bononi Komba na Ndugu Musa Sita, karibuni sana ndugu zetu kutoka Ruvuma. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Salum Rehani (Mbunge) ambao ni wapiga kura na viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Uzini, Mkoa wa Kusini Unguja wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo Ndugu Haji Waziri, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Wanu Hafidh (Mbunge) ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar, Ndugu Ibrahim Mohamed na Ndugu Samia Abdallah, karibuni. Someni na ninyi mtakuwa Wabunge siku moja. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Joseph Michael (Mbunge) ambao ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa UVCCM kutoka Mkoa wa Mwanza Ndugu Jamal Magesa. Jamal Magesa karibu. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Edwin Sannda (Mbunge) ambao ni watoto wake kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. Mheshimiwa Sannda, naona timu nzuri sana hii. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Seif Gulamali (Mbunge) ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na bibi yake mzaa mama, Ndugu Amina Ganaim. *(Makofi)*

Sasa ngoja niseme kidogo hapa, kuna bahati sana kwa familia hii, Mheshimiwa Gulamali ni Mbunge wetu wa Manonga, marehemu babu yake alifariki mwaka 1990 akaacha watoto 30 na wajukuu sasa 60. Miongoni mwa wajukuu hao Gulamali pamoja na Mbunge wetu wa Nyang'hwale Mheshimiwa Amar. Kwa hiyo mnaona mzee yule alikuwa shughuli. Karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sabrina Sungura (Mbunge) ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mbunge wa Kiteto ambao ni wakulima kutoka Kiteto Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Christopher Hamelk. Wakulima wetu stadi karibuni sana, mimi nilikuwa jirani yenu huko, siku hizi silimi huko. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba (Mbunge) ambao ni kwaya ya Efatha kutoka Kanisa la Efatha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lubatuka Japhet. Kwaya yetu, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 34 wa Mheshimiwa Ritta Kabati (Mbunge) ambao ni wanamaombi kutoka Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 48 wa Mheshimiwa Fred Mwakibete (Mbunge) ambao ni kwaya ya *Emmanuel Academy* ya Ukonga Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mlezi wa kwaya hiyo Ndugu Stanley Ngosi. Karibuni sana, mmependeza sana. Watatuimbia baadae huko. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa William Qambalo (Mbunge) ambao ni Diwani wa kata ya Buga kutoka Karatu Mkoani Manyara, Mheshimiwa Emmanuel Tiatso. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Tuna wanafunzi 100 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Christina ya Jijini Tanga. Wamekuja kwenye mafunzo hawa, ndiyo timu ya kwanza tuliyotambulishwa. *(Makofi)*

Kwenye *gallery* ya Spika kuna wageni wengine; tuna mgeni mashuhuri ambaye pia kwenye ibada ya leo atahubiri, Mtume na Nabii Josephat Mwingira, karibu sana na timu yako lakini ameongozana na mke wake Ewakwada Mwingira na Mchungaji Frida Nyito, karibuni sana. *(Makofi)*

Nije kwenye matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo

tarehe 10 Septembe saa tisa mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ukumbi namba 9 Jengo la Utawala. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa *TWPG* Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kuwa leo tarehe 10 Septemba kutakuwa na semina kwenye ukumbi wa St. Gasper mara tu baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge saa saba mchana.

Mheshimiwa Rweikiza, Katibu wa *caucus* ya CCM anawatangazia Wabunge wote wa CCM mara baada ya kikao hiki kutakuwa na kikao kifupi sana ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada wa *Chapel* yetu ya Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katiak eneo la wazi la *basement* leo siku ya Jumanne tarehe 10 Septemba mara tu baada ya shughui za Bunge kusitishwa mchana. Katika ibada hiyo mtumishi wa Mungu, Mtume na Nabii, Josephat Mwingira atahudumu katika ibada hiyo. Wote mnakaribishwa na Mheshimiwa Masoud unakaribishwa. *(Makofi)*

Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**NDUGU. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba Kigosi Kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi

### Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji wa Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Igalla Kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla

**na**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki *(Minamata Convention on Mercury)***

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Leo sichukui Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dharura. Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Hapana, nimeshasema.

**MBUNGE FULANI:** Hali ya hatari Mheshimiwa.

**MWENYEITI:** Mheshimiwa Waziri, *take your position.*

**WABUNGE FULANI:** Hali ya hatari.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa jukumu la kusimamia rasilimali za wanyamapori, misitu, malikale na uendelezaji wa utalii. Usimamizi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori unajumuisha Hifadhi za Taifa 19, Mapori ya Akiba 23, Mapori Tengefu 42, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 22 zilizosajiliwa na 16 ambazo zipo katika hatua mbalimbai za usajili. Aidha, tofauti ya msingi ya maeneo haya ni aina ya matumizi yanayoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Wizara ya Maliasili na Utalii iliwasilisha maombi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba sehemu ya Pori la Akiba Ugalla na Hifadhi ya Msitu wa *Ugalla North* zibadilishwe hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla pia Pori la Akiba Kigosi libadilishwe hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya maombi hayo ni kuimarisha ulinzi wa maliasili na kuongeza wigo wa utalii katika maeneo hayo kwa lengo la kuongeza mapato ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliridhia maombi haya ya Wizara mnamo tarehe 25 Agosti, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maombi yaliyoridhiwa na Mheshimiwa Rais, Mapori ya Akiba na Hifadhi za Misitu zinazopendekezwa kubadilishwa hadhi ni zifuatazo; Pori la Akiba Kigosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 lililoanzishwa kwa tangazo la Serikali Namba 68 la mwaka 1983 na sehemu ya Pori la Akiba Ugalla lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1811 kati ya 5,000 lililoanzishwa kwa tangazo la Serikali Namba 281 la mwaka 1965 na sehemu ya Msitu wa Hifadhi *Ugalla North* wenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,054.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza maelekezo na ridhaa ya Mheshimiwa Rais ya kubadilisha hadhi mapori tajwa na hifadhi ya msitu kuwa Hifadhi za Taifa, Sheria ya Hifadhi za Tafa Sura 282 katika kifungu cha 3 na cha 4 inaelekeza utaratibu wa kuzingatia kama ifuatavyo na ninaomba kunukuu; *Section 3, "The President may with the consent of the National Assembly by proclamation publishing the gazette declare any area of land to be a Nat ional Park for the purposes of this Act."*

*Section 4* inasema; *"Notwithstanding anything contained in the interpretation of Laws Act, no proclamation made under the provision of section 3 of this Act shall be amended, veried or revoked except under the authority of an Act of Parliament provided that the President may with the consent of the National Assembly by Proclamation Publish in the gazette alter the boundaries of any area declared to be a National Park under the provisions of Section 3."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo haya ya Mheshimiwa Rais, Wizara inapendekeza yafuatayo; moja, Pori la Akiba Kigosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 libadilishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na mbili, sehemu ya Pori la Akiba Ugalla na Hifadhi ya Msitu

wa *Ugalla North* zenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,865 zibadilishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mapendekezo haya kwa wakati utawezesha kuunganisha mfumo wa ikolojia wa Malagarasi Muyowosi ambao ni ardhi oevu yenye umuhimu wa kimataifa pia kuongeza Pato la Taifa kutokana na ongezeko la idadi ya watalii, kuwezesha jamii, kunufaika na fursa za utalii na kuimaisha uhifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha hoja ya kuwa Bunge lako tukufu ili kupata ridhaa ya kubadilisha hadi ya maeneo haya yafuatayo basi pori la akiba Kigosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 libadilishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi. Pili, sehemu ya Pori la Akiba Ugalla na Hifadhi ya Msitu wa *Ugalla North* zenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,865 zibadilishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono. Sasa soma Azimio. Endelea halafu utakuja kuitoa hoja tena.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa Azimio la Bunge la kuridhia ubadilishaji hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi.

KWA KUWA Sera ya Wanyampori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda baioanuai katika mtandao wa hifadhi za Taifa, mapori ya akiba na mapori tengefu;

NA KWA KUWA Sera ya Utalii ni kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii, unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi;

NA KWA KUWA Pori la Akiba Kigosi lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 568 la mwaka 1983 ambapo imekusudiwa tangazo hilo lifutwe ili kubadilisha hadhi ya sehemu ya pori hilo kuwa Hifadhi ya Taifa;

KWA KUWA kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 kinampa Rais kwa idhini ya Bunge kwa Tangazo la Rais litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali mamlaka ya kutangaza eneo la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa kwa madhumuni ya sheria hiyo;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 ili kuanzisha Hifadhi ya Taifa ni sharti kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA kubadilisha hadhi ya uhifadhi kwa sehemu ya eneo la Pori la Akiba Kigosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi kutaimarisha uhifadhi wa baioanuai hususan za wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuongeza utalii wa ndani, kukuza uchumi wa jamii inayozunguka hifadhi, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hiyo;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Azimio hilo, Taifa litapata manufaa yafuatayo.

(a) Kuimarisha na kuendeleza uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa kwenye maji; na

(b) Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa pori hilo utasababisha hifadhi hiyo kuwa kivutio cha utalii.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya utangazaji wa hifadhi tajwa ya Taifa ninaomba sasa Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita na kwa mujibu wa masharti ya kifungu 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 niridhie Azimio la ubadilishaji hadhi sehemu ya Pori la Akiba Kigosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi. Hivyo mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Kigosi itasomeka kama inavyoainishwa katika kiambatisho cha azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya Azimio la Bunge la kuridhia ubadilishaji hadhi sehemu ya Pori la Akiba Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla.

KWA KUWA Sera ya Wanyamapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda baioanuai katika mtandao wa hifadhi za taifa, mapori ya akiba na mapori tengefu;

NA KWA KUWA Sera ya Utalii ni kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi;

NA KWA KUWA Pori la Akiba la Ugalla lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 281 la mwaka 1965 ambapo imekusudiwa tangazo hilo lifutwe ili kubadilisha hadhi ya sehemu ya pori hilo na kuwa Hifadhi za Taifa;

NA KWA KUWA kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 kinampa Rais kwa idhini ya Bunge kwa Tangazo la Rais litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali mamlaka ya kutangaza eneo la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa kwa madhumuni ya sheria hiyo;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282 ili kuanzisha Hifadhi ya Taifa ni sharti kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA kubadilisha hadhi ya uhifadhi kwa sehemu ya Pori la Akiba Ugalla lenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,865 kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kutaimarisha uhifadhi wa baioanuai hususan za wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuongeza utalii wa ndani, kukuza uchumi wa jamii inayozunguka hifadhi, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hiyo na kwa kuridhia azimio hili taifa litapata manufaa yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa kwenye maji; na

(b) Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa sehemu ya pori hilo utasababisha hifadhi hiyo kuwa kivutio cha utalii.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya utangazaji wa hifadhi tajwa ya Taifa ninaomba sasa Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita kwa mujibu wa masharti ya kifungu 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 liridhie Azimio la Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Pori la Akiba Ugalla lenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,865 kuwa Hifadhi ya Taifa

Mto Ugalla. Hivyo, mipaka ya Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla itasomeka kama inavyoainishwa katika kiambatisho cha azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati aliyechambua na kuleta mapendekezo Bungeni Mheshimiwa Kemirembe. Una muda usiozidi dakika 20. *(Makofi)*

**MHE. KEMIREMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maazimio ya Bunge ya kuridhia mapendekezo ya ubadlishaji wa sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Maazimio ya Bunge ya ubadilishaji hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio yaliyowasilishwa yanatokana na Sera ya Wanyamapori ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuai katika mtandao wa hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hii kwenye Kamati ya

Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, tarehe 9 Septemba, 2019, Kamati ilikutana na kuifanyia kazi hoja hii muhimu. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushaurikwa kuanza na manufaa ya uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa umuhimu wa kiikolojia wa Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla ambayo ni pamoja na uwepo wa mito, misitu, maeneo oevu na vyanzo vya maji.

Aidha, ubadilishaji hadhi wa mapori haya kutaimarisha uhifadhi hususan wa bioanuai za wanyamapori, mimea, nyuki, na mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuwa kivutio cha utalii wa ndani. Vilevile itachangia kukuza uchumi wa jamii inayozunguuka hifadhi hizo, itakuwa eneo la kufanyia utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali wa kuyapandisha hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla siyo tu kutaimarisha ulinzi, kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo bali pia kutaifungua fursa za utalii katika ukanda wa Magharibi wa nchi yetu. Aidha, kupandisha hadhi sehemu ya mapori haya kutaimarisha jitihada za Serikali za kulinda maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Kamati inapenda kumpongeza kwa dhati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa jitihada zake za kujenga miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vitakavyorahisisha ufikaji wa watalii katika maeneo haya. Uwepo wa uwanja wa ndege wa Chato, Mwanza, Kigoma na Bukoba pamoja na mtandao wa barabara za lami ni ushahidi tosha wa jitihada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya kamati; uamuzi wa kupandisha hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla kutaimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii katika ukanda wa Magharibi na kukuza pato la wananchi wa ukanda huo na Taifa kwa ujumla. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kupitisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inashauri Serikali kuhakiki mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi mpya. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kuvutia wawekezaji kujenga mahoteli ndani au karibu na hifadhi ili kuwezesha watalii wengi wa nje na ndani kuweza kutembelea hifadhi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wadau waliijulisha Kamati katika baadhi ya maeneo yanayokusudiwa kupandishwa hadhi hasa katika Pori la Akiba la Ugalla, kuna vijiji viko ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria. Aidha, wako wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika mto Ugalla na wengine wanafuga nyuki katika mapori yote mawili. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha wananchi waliomo ndani ya hifadhi hawabugudhiwi na wanawekewa utaratibu ambao hautaleta migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa wananchi hawajashirikishwa katika mchakato huu wa kubadili sehemu ya Mapori ya Akiba kuwa Hifadhi za Taifa na hivyo kutowatayarisha kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na misitu. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha wananchi juu ya dhana ya uhifadhi shirikishi ili nao waweze kutoa mchango wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyowahi kusema katika taarifa zetu za nyuma, Serikali ione uwezekano wa kulijengea Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* mazingira

wezeshi yatakayolisaidia kumudu kuzihudumia hifadhi mpya zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuiwezesha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Tunaliomba Bunge kuitaka Serikali kuharakisha kuleta Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori mapema iwezekanavyo kwani kimekuwa ni kilio cha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Katibu wa Kamati Ndugu Elihaika Mtui kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAAZIMIO YA BUNGE YA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA UBADILISHAJI WA SEHEMU ZA MAPORI YA AKIBA YA KIGOSI NA UGALLA KUWA HIFADHI ZA TAIFA ZA KIGOSI NA MTO UGALLA - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu

Maazimio ya Bunge ya ubadilishaji hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla.

## 2.0 CHIMBUKO LA MAAZIMIO

**Mheshimiwa Spika,** Maazimio yaliyowasilishwa yanatokana na Sera ya Wanyamapori ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuai katika mtandao wa hifadhi za Taifa ,Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

**Mheshimiwa Spika,** Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, tarehe 9 Septemba, 2019, Kamati ilikutana na kuifanyia kazi hoja hii muhimu. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri kwa kuanza na manufaa ya uamuzi**.**

## 3.0 MANUFAA

**Mheshimiwa Spika**, imeelezwa umuhimu wa kiikolojia wa Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla ambayo ni pamoja na uwepo wa mito, misitu, maeneo oevu na vyanzo vya maji. Aidha ubadilishaji hadhi wa Mapori haya kutaimarisha uhifadhi hususan wa bioanuai za wanyamapori,mimea, nyuki, na mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuwa kivutio cha utalii wa ndani. Vile vile itachangia kukuza uchumi wa jamii inayozunguuka hifadhi hizo , itakuwa eneo la kufanyia utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hizi.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali wa kuyapandisha hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa Hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla siyo tu kutaimarisha ulinzi, kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo

bali pia kutafungua fursa za utalii katika ukanda wa Magharibi wa nchi yetu. Aidha kupandisha hadhi sehemu ya mapori haya kutaimarisha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee Kamati inapenda kumpongeza kwa dhati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa jitihada zake za kujenga miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vitakavyorahisisha ufikaji wa watalii katika maeneo haya. Uwepo wa uwanja wa ndege wa Chato, Mwanza, kigoma na Bukoba pamoja na mtandao wa barabara za lami ni ushahidi tosha wa jitihada hizo.

## 4.0 MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa kupandisha hadhi sehemu ya Mapori ya Akiba ya Kigosi na Ugalla kuwa hifadhi za Taifa za Kigosi na Mto Ugalla kutaimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii katika ukanda wa Magharibi na kukuza pato la wananchi wa ukanda huo na Taifa kwa ujumla. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kupitisha hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro**,** Kamati inashauri Serikali kuhakiki Mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi mpya. Aidha Serikali iweke mkakati wa kuvutia wawekezaji kujenga mahoteli ndani au karibu na hifadhi ili kuwezesha watalii wengi wa nje na ndani kuweza kutembelea hifadhi hizi.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya wadau waliijulisha Kamati katika baadhi ya maeneo yanayokusudiwa kupandishwa hadhi hasa katika Pori la Akiba la Ugalla,kuna vijiji viko ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria. Aidha wako wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika mto Ugalla na wengine wanafuga nyuki katika Mapori yote mawili. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha wananchi waliomo ndani ya hifadhi

hawabugudhiwi na wanawekewa utaratibu ambao hautaleta migogoro.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa wananchi hawajashirikishwa katika mchakato huu wa kubadili sehemu ya Mapori ya Akiba kuwa hifadhi za Taifa na hivyo kutowatayarisha kushiriki katika uhifadhi wa raslimali za wanyamapori na Misitu. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha wananchi juu ya dhana ya uhifadhi shirikishi ili nao waweze kutoa mchango wao.

**Mheshimiwa Spika,** Kama tulivyowahi kusema katika taarifa zetu za nyuma, Serikali ione uwezekano wa kulijengea Shirika la Hifadhi za Taifa(TANAPA) mazingira wezeshi yatakayolisaidia kumudu kuzihudumia hifadhi mpya zilizoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuiwezesha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania(TAWA) iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Tunaliomba Bunge kuitaka Serikali kuharakisha kuleta Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori mapema iwezekanavyo kwani kimekuwa ni kilio cha muda mrefu.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spka,** baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg, Athman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg.Gerald Magili, Katibu wa Kamati Ndg Elihaika Mtui kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

**Mheshmiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Kemirembe Julius Lwota, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

10 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti kwa taarifa yako nzuri inayounga mkono. Tunaendelea Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani muda usiozidi dakika 20.

**MHE. CATHERINE N. RUGE K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Maliasili na Utalii napenda kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu azimio la kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba na Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla, pamoja na kuridhia mapendekezo ya ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (a) Pori la Akiba la Ugalla; Pori la Akiba la Ugalla ni mojawapo kati ya mapori kumi makubwa hapa nchi, lipo mkoa wa Tabora na lina ukubwa wa kilometa za mraba zipatazo 5,000 na lilianzishwa mwaka 1965. Pori la Akiba la Ugalla linapatikana takribani kilometa 191 kutoka Tabora Mjini na linatambulika kwa kuwa na uoto wa asili mbalimbali hasa miti ya miombo na ni moja ya eneo muhimu la uhifadhi wa mazingira ya makazi oevu. Viumbe hai na wanyamapori takribani 50,000 wanapatikana katika eneo hilo. Wanyamapori hawa ni kama vile simba, chui, tembo, viboko, Twiga, nyati, pala, kulo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pori hili la Ugalla ni miongoni mwa mapori ya akiba 28 yanayosimamiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Wanyapori Tanzania *(TAWA).* Kama ilivyo kwa mapori mengine ya akiba hapa nchini shughuli za uwindaji katika pori hili la akiba la wanyamapori zinaruhusiwa kwa watu wenye vibali na leseni za uwindaji baada ya kulipia gharama stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufika makao makuu ya eneo la Pori la Wanyamapori la Ugalla, itakubidi kusafiri kilometa 128 kutoka Tabora hadi Kaliua na kilometa 63 kutoka Kaliua Mjini hadi Pori la Akiba la Ugalla na hivyo kufanya umbali wote kuwa kilometa 191.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Akiba Ugalla limepakana na Wilaya ya Sikonge, Urambo na Kaliua na kwa pande mwingine lipo kwenye Mkoa wa Rukwa. Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri husika hifadhi inayoombewa kibali au ridhaa ya Bunge itakuwa na ukubwa wa kilometa za Mraba 1,811; Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata ufafanuzi eneo hilo litakatwa au litamegwa kutoka upande upi wa pori hilo ili kuangalia kama wananchi ambao wanapakana na pori hilo wanaweza kuathirika na mkakati wa kuhakikisha wananchi hawapati madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni vijiji vingapi katika kata ngapi zinazozunguka eneo la kilometa za mraba ambazo zinapandishwa kuwa Hifadhi ya Mto Ugalla. Hii ni kutokana na ukweli kuna wananchi ambao wanafanya shughuli zao karibu na maeneo hayo ya hifadhi au mapori ya akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa Mheshimiwa Rais alishasikika akisema kuwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki kuendelea kufanya hivyo na wasibughudhiwe. Kwa kuwa katika awamu hii tano ya utawala, kauli ya Mheshimiwa Rais ni sawa na sheria na wananchi waliisikia na wakatoa pongezi kwa Mheshimiwa

Rais kwa kuwajali wananchi wa hali ya chini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kuwahamisha wananchi toka kwenye Pori la Akiba la Ugalla ni kupingana na kauli ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo wadau wengi wamelitolea maoni linalohusu mamlaka tatu za Serikali kujihusisha na majukumu yanayofanana, mamlaka hizo ni *TAWA*, *TANAPA* na *NCAA*. Mamlaka hizo zote zinajihusisha na uhifadhi wa wanyamapori na kutoa huduma kwa wageni wanaokuja kwa ajili ya kutemebelea vivutio vyetu vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanyia tafakari ya kina maoni hayo ya wadau utaona ni sahihi kabisa kwani uwepo wa taasisi hizo zote ni kuongeza ukubwa wa Serikali na hivyo kuongeza mzigo wa bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau hao walikwenda mbali zaidi kwa kuonesha jinsi majirani zetu wa Kenya ambao wana taasisi moja tu inayojihusisha na utalii na wanyamapori ijulikanayo kama *Kenya Wildlife Service (KWS),* kwa Zambia inaitwa *Zambia Wildlife Authority (ZAWA)* na Uganda inaitwa *Uganda Wildlife Authority (UWA)* na mataifa hayo yote yana mapori ya akiba na mbuga za wanyama katika nchi zao. Lakini mamlaka inayosiamamia Tasisi zote ni moja na zinafanya kazi vizuri sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili linakinzana na dhana ya utawala bora na uzingatiwaji wa matumizi endelevu wa rasilimali na kodi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Akiba la Ugalla kwa sasa liko chini ya *TAWA* na linasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji mmoja, je, baada ya kuligawanya, wakati kiuhalisia kilometa za mraba bado ni zilezile na wanyama ni wale wale na biashara inayofanyika inafanana ila itakuwa na wasimamizi wakuu wawili. Maana yake ni kuwa matumizi yataongezeka. Kwa mantiki hiyo kweli tunaweza kujitanabahisha kuwa ni wapangaji wazuri katika matumizi ya rasilimali zetu ndogo tulizonazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imekuwa inasema kwamba, kuongeza hifadhi zitakazo kuwa zinahudumiwa na *TANAPA* ni kuzipunguzia uwezo wa kifedha hifadhi zingine ambazo zinaweza kujiendesha kwa faida kwa mfano Hifadhi ya Serengeti, hii inaweza kupelekea hifadhi hizo kushindwa kuwekeza zaidi ili kuvutia watalii. Uwezo huo unapungua kwa kuwa *TANAPA* inalazimika kuzisaidia hifadhi mpya zinazoanzishwa bila ya kuwa na bajeti ya kuziendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (b) Pori la Akiba la Kigosi lina ukubwa wa kilometa za mraba 7,000 ilianzishwa mwaka 1983 na linapatikana katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Shinyanga. Serikali inataka kumega sehemu ya Pori hilo kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumetoa hoja zetu hapo awali kuhusiana na kumegwa kwa sehemu ya Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla, hoja za msingi ni zile zile kwani mazingira ya utunzaji au uhifadhi wa mazingira ya mapori yetu yanafanana. Hivyo itakuwa ni muhimu kwa Serikali kutoa ufafanuzi kulingana na hoja zilizoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kulieleza Bunge bajeti ya uendeshaji wa hifadhi hizi mpya ambazo zinaombwa kuridhiwa na Bunge ipo kwenye fungu lipi na kasma namba ngapi? Uamuzi unaotolewa bila ya kuwepo wa kasma ya uendeshaji sio kama unalisaidia Taifa bali unalitia hasara Taifa, kwani inalazimika kunyang'anya fedha ambazo tayari zilikwishapangiwa matumizi kwenye bajeti na hivyo miradi hiyo inalazimika kusimama hadi uamuzi wa dharura utekelezwe, tukumbuke kuwa muda ni rasilimali, pindi unapopita hairudi tena na hiyo ni hasara ambayo haiwezi kufidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache kuhusiana na mapendekezo ya Serikali kuhusu

Bunge kuridhia ubadilishaji wa hadhi ya mapori hayo ya akiba kuwa Hifadhi za Taifa, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**AZIMIO LA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA UBADILISHAJI HADHI SEHEMU YA ENEO LA PORI LA AKIBA LA UGALLA KUWA HIFADHI YA TAIFA YA MTO UGALLA, PAMOJA NA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA UBADILISHAJI WA HADHI SEHEMU YA ENEO LA PORI LA AKIBA LA KIGOSI KUWA HIFADHI YA TAIFA YA KIGOSI - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2016)"*

**A. PORI LA UGALLA**

**Mheshimiwa Spika,** pori la akiba la wanyamapori la Ugalla ni mojawapo kati ya mapori kumi makubwa hapa nchi, lipo mkoa wa Tabora na lina ukubwa wa kilometa za mraba zipatazo 5,000 na lilianzishwa mwaka 1965. Pori la akiba la wanyamapori la Ugalla linapatikana takribani kilometa 191 kutoka Tabora mjini na linatambulika kwa kuwa na uoto wa asili mbalimbali hasa miti ya miombo na ni moja ya eneo muhimu la uhifadhi wa mazingira ya makazi Oevu. Viumbe hai na wanyamapori takribani 50,000 wanapatikana katika eneo hilo. Wanyamapori hawa ni kama vile simba, chui, Tembo, viboko, Twiga, nyati au swala, pala, kulo, Nyamera, mbwa mwitu, Ngiri na na wanyama wengineo.

**Mheshimiwa Spika**, pori hili la UGALLA ni miongoni mwa mapori ya akiba 28 yanayosimamiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Wanyapori Tanzania (TAWA), kama ilivyo kwa mapori mengine ya akiba hapa nchini, shughuli za uwindaji katika pori hili la akiba la wanyamapori zinaruhusiwa kwa watu wenye vibali na leseni za uwindaji baada ya kulipia gharama stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufika makao makuu ya eneo la pori la wanyapori la Ugalla, itakubidi kusafiri kilometa 128 kutoka Tabora mjini hadi Kaliua na kilometa 63 kutoka Kaliua mjini hadi pori la Ugalla linapoanzia na hivyo kufanya umbali wote

kuwa kilometa 191 na wakati wa kiangazi ndege ndogo zinaweza kutua katika viwanja vidogo vya Muhuba and Siri.

**Mheshimiwa Spika,** Pori la UGALLA limepakana na Wilaya ya Sikonge, Urambo na Kaliua na kwa pande mwingine ipo kwenye mkoa wa Rukwa. Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri husika Hifadhi inayoombewa kibali au ridhaa ya Bunge itakuwa na ukubwa wa Kilomita za Mraba 1,811, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata ufafanuzi eneo hilo litakatwa au litamegwa kutoka upande upi wa pori hilo, ili kuangalia kama wananchi ambao wanapakana na pori hilo wanaweza kuathirika na mkakati wa kuhakikisha wananchi hawapati madhara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni vijiji vingapi katika kata ngapi zinazozunguka eneo la kilomita za mraba 1,811 ambazo zinapandishwa kuwa hifadhi ya mto Ugalla. Hii ni kutokana ukweli kuna wananchi ambao wanafanya shughuli zao karibu na maeneo hayo ya hifadhi au mapori ya akiba.

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kuwa Mheshimiwa Rais alishasikika akisema kuwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki kuendelea kufanya hivyo na wasisumbuliwe. Kwa kuwa katika awamu hii tano ya utawala, Kauli ya Mheshimiwa Rais ni sawa na Sheria na wananchi waliisikia na wakatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwajali wananchi wa hali ya chini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kuwahamisha wananchi toka kwenye pori la UGALLA ni kupingana na kauli ya Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** kuna jambo ambalo wadau wengi wamelitolea maoni, linalohusu mamlaka tatu za Serikali kujishughulisha na majukumu yanayofanana, taasisi hizo ni TAWA, TANAPA na NCA. Mamlaka hizo zote zinajihusisha na uhifadhi wa wanyamapori na kutoa huduma kwa wageni wanaokuja kwa ajili ya kutemebelea vivutio vyetu vya asili.

**Mheshimiwa Spika,** ukifanyia tafakari ya kina maoni hayo ya wadau, utaona ni sahihi kabisa, kwani uwepo wa taasisi hizo zote ni kuongeza ukubwa wa Serikali na hivyo kuongeza mzigo wa bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya matumizi kwenye miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** wadau hao walikwenda mbali zaidi kwa kuonesha jinsi majirani zetu wa Kenya ambao wana taasisi moja tu inayojihusisha na utalii na wanyamapori ijulikanayo kama *Kenya Wildlife Service (KWS),* kwa Zambia inaitwa *Zambia Wildlife Authority (ZAWA)* na Uganda inaitwa *Uganda Wildlife Authority(UWA)* na mataifa hayo yote yana mapori ya akiba na Mbuga za wanyama katika nchi zao. Lakini mamlaka inayosiamamia Tasisi zote ni moja na zinafanya vizuri kabisa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili linakinzana na dhana ya Utawala Bora na uzingatiwaji wa matumizi endelevu wa rasilimali na kodi za watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** pori la UGALLA kwa sasa liko chini ya TAWA na linasimamiwa na mkurugenzi mtendaji mmoja, je, baada ya kuligawanya, wakati kiuhalisia kilometa za mraba bado ni zile zile na wanyama ni wale wale na biashara itakayokuwa inafanyika inafanana ila wasimamizi wakuu watakuwa wawili. Maana yake ni kuwa matumizi yanaongezeka. Kwa mantiki hiyo kweli tunaweza kujitanabahisha kuwa ni wapangaji wazuri katika matumizi ya rasilimali zetu kidogo tulizonazo?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imekuwa inasema kwamba, kuongeza hifadhi zitakazo kuwa zinahudumiwa na TANAPA ni kuzipunguzia uwezo wa kifedha hifadhi zingine ambazo zilikuwa zinaweza kujiendesha kwa faida kwa mfano Hifadhi ya Serengeti hii inaweza kupelekea hifadhi hizo kushindwa kuwekeza zaidi ili kuvutia watalii. Uwezo huo unapungua kwa kuwa TANAPA inalazimika kuzisaidia hifadhi mpya zinazoanzishwa bila ya kuwa na bajeti ya kuziendesha.

**B. PORI LA KIGOSI**

Mheshimiwa Spika, **Pori la Akiba la Kigosi** – lina ukubwa wa kilomita za mraba 7,000 ilianzishwa mwaka 1983 na linapatikana katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Shinyanga. Serikali inataka kumega sehemu ya Pori hilo kuwa hifadhi ya Taifa ya KIGOSI.

**Mheshimiwa Spika,** Kama ambavyo tumetoa hoja zetu hapo awali kuhusiana na kumegwa kwa sehemu ya Pori la Akiba la Ugalla kuwa hifadhi ya Taifa ya Mto UGALLA, hoja za msingi ni zile zile kwani mazingira ya utunzaji au uhifadhi wa mazingira ya mapori yetu yanafanana.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo itakuwa ni muhimu kwa Serikali kutoa ufafanuzi kulingana na hoja zilizoelezwa hapo juu.

**C. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inamtaka Mheshimiwa Waziri kulieleza Bunge bajeti ya uendeshaji wa hifadhi hizi mpya ambazo zinaombwa kuridhiwa na Bunge ipo kwenye fungu lipi na kasma namba ngapi? Uamuzi unaotolewa bila ya uwepo wa kasma ya uendeshaji sio kama unalisaidia Taifa bali unalitia hasara Taifa, kwani inalazimika kunyanganya fedha ambazo tayari zilikwishapangiwa matumizi kwenye bajeti, na hivyo miradi hiyo inalazimika kusimama hadi uamuzi wa dharura utekelezwe, tukumbuke kuwa muda ni Rasilimali pindi unapopita hairudi tena na hiyo ni hasara ambayo haiwezi kufidiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo Machache kuhusiana na mapendekezo ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Ubadilishaji wa hadhi ya mapori hayo ya akiba kuwa hifadhi za Taifa, naomba kuwasilisha.

Catherine Nyakao Ruge(Mb)
**Kny: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA MALIASILI NA UTALII.**
**10.9.2019**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Catherine Ruge, namuita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Simbachawene awasilishe Azimio la Serikali. Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa tangu niteuliwe kuwa Waziri, naomba nichukue nafasi ya kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini tena ili niweze kuhudumu katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo yao kwangu na kunisaidia katika kipindi chote kabla na hata baada ya kuwa katika nafasi hii. Niwashukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na ninyi Wenyeviti na Wabunge wenzangu kwa kufanya kazi pamoja wakati wote kabla na hata baada ya kuwa katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa kunivumilia na kuwa na mimi wakati wote wa magumu na mambo mazuri yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kusoma Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki *(The Minamata Convention on Mercury).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki ni makubaliano ya Jumuiya ya Kimataifa kuhusu udhibiti na usimamizi wa uchafuzi unaotokana na zebaki. Kufuatia kuongezeka kwa changamoto ya zebaki duniani Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira kupitia Azimio Namba *GC21/5* la mwaka 2001 lilielekeza kufanyika tathmini ya hali ya uchafuzi wa mazingira duniani. Matokeo ya tathmini yaliwasilishwa katika kikao cha 22 cha Baraza hilo kilichofanyika mwezi Februari, 2003 huko Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kwamba zebaki hudumu katika mazingira kwa muda mrefu, miaka miwili hadi 20 na husafiri masafa marefu kwa njia ya hewa, maji yaani mito, maziwa na bahari na udongo. Vilevile ilibainika zebaki husafiri angani umbali wa hadi kilometa 1,000 kutoka kwenye chanzo na huathiri afya ya binadamu, viumbe wengine na mazingira. Athari hizi zinajitokeza zaidi katika nchi zinazoendelea ukilinganisha na nchi zilizoendelea kutokana na nchi hizo kupunguza matumizi ya zebaki. Tathmini hiyo ilipendekeza hatua za pamoja za Jumuiya ya Kimataifa zichukuliwe bila kuchelewa ili kupunguza madhara hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia matokeo ya tathmini hiyo Baraza lilihimiza nchi kuchukua hatua za hiyari za kukabiliana na changamoto ya matumizi ya zebaki hali ambayo haikufanikiwa. Hivyo Baraza kupitia Azimio Namba *GC25/5* la mwaka 2009 liliazimia kuanzishwa kwa mkataba wa kimataifa wa kukabiliana na uchafuzi utoakano na matumizi ya zebaki. Kupitia azimio hilo Kamati ya Kimataifa ya Majadiliano ya Uanzishwaji wa Mkataba iliundwa na kuendesha majadiliano yaliyodumu kwa muda wa miaka mitatu hadi tarehe 19 Januari, 2013. Hatua hii ilifuatiwa na Mkutano wa Kidoplomasia wa Jumuiya ya Kimataifa uliofanyika katika Mji wa Minamata, Japan, terehe 10 Oktoba, 2013 na kupitishwa Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huo ulisainiwa na nchi 128 ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo kuu la mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari za uchafuzi wa mazingira unaotokana na matumizi ya zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki yanashabihiana na baadhi ya vipengele vya mikataba ambayo Tanzania imeridhia. Mikataba hiyo ni ule wa Stockholm kuhusu udhibiti wa kemikali za ki-*organic* zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu, Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji wa utupaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi, Rotterdam unaohusu

upashanaji wa habari kuhusu udhibiti wa biashara ya kimataifa ya kemikali hatarishi na viuatilifu na Mkataba wa Bamako unaozuia uingizwaji taka hatarishi katika Bara la Afrika na udhibiti wa usafirishaji baina ya nchi na nchi na usimamizi wa taka hatarishi Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Minamata unaolenga kudhibiti aina zote za zebaki katika hatua za uzalishaji, matumizi na utupaji wake kwa upande mmoja Mkataba wa Stockholm unalenga katika udhibiti wa kemikali za aina ya ki-*organic* tu ambapo baadhi ya aina ya zebaki hazina sifa hii. Mikataba ya Basel na Bamako ni mahususi katika udhibiti wa taka hatarishi ikiwemo taka za zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mikataba hii haihusishi hatua za uzalishaji, biashara na matumizi ya zebaki ambazo zinadhibitiwa na Mkataba wa Minamata na Mkataba wa Rotterdam unaohusu ubadilishwanaji taarifa za viuatilifu na kemikali za viwandani ikiwemo viambata vya zebaki kwenye viuatilifu, hata hivyo hauna mfumo moja kwa moja wa udhibiti na usimamizi wa zebaki ukilinganisha na mkataba wa minamata ambao umeweka mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sheria hapa nchini ambazo zinatoa mwongozo wa jumla kuhusu usimamizi wa zebaki. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya mwaka 2003, Sheria ya Madini ya mwaka 2010, Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 na Sheria ya Dawa na Chakula ya mwaka 2003. Sheria hizi hazihitaji marekebisho yoyote bali zitaandaliwa kanuni za usimamizi wa zebaki nchini chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ili kuwezesha utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na tafiti zilizofanyika hapa nchini inakadiriwa kuwa 25% hadi 33% ya wachimbaji wadogo wa dhahabu hapa nchini wameathiriwa na zebaki kwa kupata magonjwa yakiwemo

yale ya mifumo ya neva za fahamu, uzazi, upumuaji, figo, moyo na udhaifu wa mwili. Aidha, baadhi ya athari kwa mazingira zilizobainika ni pamoja na kudhoofika kwa ukuaji wa viumbehai wanaoishi ndani ya maji, uchafuzi wa mfumo mfuatano wa mazao ya chakula, mifugo na samaki na uchafuzi wa vyanzo vya maji, hewa na udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukubwa wa changamoto zitokanazo na matumizi ya zebaki kwa afya ya binadamu na kwa mazingira, Jumuiya ya Kimataifa iliona umuhimu wa kuanzisha Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki ili kukabiliana na changamoto hizi. Hivyo basi, ni muhimu kwa Tanzania kuridhia mkataba huu ili kukabiliana na madhara yatokanayo na zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo haya vipengele muhimu vya mkataba huu ni pamoja na hivi vifuatavyo:-

(i) Ibara ya 4, bidhaa zenye viambata vya zebaki; Ibara hii inazitaka nchi zilizoridhia mkataba huu kusitisha uzalishaji, uingizaji na usafirishaji wa bidhaa zenye viambata vya zebaki zilizoorodheshwa katika mkataba ifikapo mwaka 2020. Aidha, bidhaa zote zilizoorodheshwa katika mkataba huu tayari zina mbadala na zinapatikana katika soko.

(ii) Ibara ya 5, shughuli za uzalishaji viwandani zinazotumia zebaki; Ibara hii inazuia matumizi ya zebaki katika shughuli za uzalishaji viwandani na kuweka ukomo wa matumizi ya zebaki ifikapo mwaka 2018 kwa uzalishaji wa *acetaldehyde* na mwaka wa 2025 na *chlor-alkali.* Aidha, matumizi ya zebaki duniani katika uzalishaji bidhaa viwandani yanaendelea kuondoshwa kwa kuwa kuna teknolojia mbadala na ya gharama nafuu. Kwa ujumla hapa nchini hakuna kiwanda chochote kinachotumia zebaki katika uzalishaji wa bidhaa.

(iii) Ibara ya 6, ni maombi ya msamaha kwa nchi wanachama kuendelea kutumia zebaki; Ibara hii inaweka utaratibu wa kuomba msamaha wa kuendelea kutumia

zebaki, bidhaa zenye viambata vya zebaki baada ya kipindi cha mpito cha mwaka 2020. Msamaha huu utakuwa ni wa miaka mitano kuanzia tarehe ya kujiunga na nyongeza ya miaka mitano kwa kutegemea ridhaa ya nchi wanachama na haitazidi miaka 10 hadi mwaka 2030. Kwa ujumla ibara hii inatoa fursa kwa nchi mwanachama kutumia kipindi cha mpito na kile cha msamaha kuendelea kujipanga kutekeleza mkataba huu.

(iv) Ibara ya 7, wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu; Ibara hii inazitaka nchi wanachama zilizo na wachimbaji wadogo wanaotumia sebaki katika shughuli za uchenjuaji wa dhahabu kupunguza na pale inapowezekana kuondosha matumizi ya zebaki. Ibara hii haiweki ukomo wa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na inaelekeza kuandaliwa kutekelezwa kwa mpango kazi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. Aidha, katika kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo hapa nchini, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau imeandaa rasimu ya mpango kazi wa kitaifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ambapo utategemea kukamilika mwezi Oktoba, 2019.

(v) Ibara ya 13, inahusu vyanzo vya utaratibu wa upatikanaji wa rasilimali fedha; Ibara hii imeainisha vyanzo vya mfumo wa rasilimali fedha za kutekeleza mkataba na kuhakikisha kuwa zinakidhi mahitaji ya upatikanaji kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye mkataba. Mfumo huo unaohusisha Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environmental Facility Trust Fund)* na programu maalum ya kusaidia kukuza uwezo wa kuongeza utaalamu. Njia nyingine zilizoainishwa ni pamoja na kutenga fedha, yani bajeti ya Serikali, lakini pia washirika wa maendeleo na sekta binafsi.

(vi) Ibara ya 14, inahusu ujengaji wa uwezo, misaada ya kitaalamu na uhaulishaji wa teknolojia; Ibara hii inahimiza ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika kujenga uwezo, kutoa misaada ya kitaalamu na uhaulishaji wa tekonolojia katika kutekeleza matakwa ya mkataba. Kuridhia

mkataba huu kutawezesha nchi zinazoendelea kunufaika na fursa zilizopo, ili kutekeleza mkataba.

(vii) Ibara ya 25, inahusu usuluhishi wa migogoro; Ibara hii inaelekeza nchji wanachama kusuluhisha migogoro baina yao kwa njia ya mazungumzo au kwa namna nyingine inayofaa. Hii itasaidia kutatua mgogoro wowote miongoni mwa nchi wanachama katika utekelezaji wa mkataba huu.

(viii) Ibara ya 32, ni kuridhia pasipo pingamizi; Ibara hii imezuia nchi kuridhia kwa pinagmizi katika ibara yoyote. Hata hivyo, baada ya kufanya uchanbuzi tumejiridhisha kwa sasa hakuna Ibara ambayo inakwenda kinyume na maslahi ya nchi yetu.

(ix) Ibara ya 33, ni kuhusu kujitoa kwenye mkataba; Ibara hii inaweka utaratibu wa kujitoa katika mkataba huu kwa nchi mwanachama baada ya kupita miaka mitatu toka tarehe ya kurudhia. Hatua hii ya kujitoa itatimia baada ya mwaka mmoja tangu kuwasilisha hati ya kujitoa na hivyo, utaratibu huu huchukua jumla ya miaka minne. Utaratibu huu unatoa fursa kwa nchi mwanachama kutathmini utekelezaji wa mkataba kabla ya kuamua kujitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuridhia mkataba huu kutasaidia kuimarisha na kulinda afya za binadamu na mazingira dhidi ya athari za uchafuzi wa mazingira unaotokana na matumizi ta zebaki. Matokeo mengine mahususi ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa wataalam wenye uelewa na masuala ya zebaki katika sekta mbalimbali ikiwemo mazingira, afya, kilimo, uvuvi, mifugo, madini na elimu.

(ii) Kunufaika kwa teknolojia mbadala, rasilimali fedha na msaada wa kitaalamu kwa ajili ya kuboresha usimamizi na udhibiti wa uchafuzi utoakanao na zebaki.

(iii) Kupungua kwa matumizi ya zebaki kutokana na matumizi ya bidhaa na teknolojia mbadala na mbinu bora za uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkataba huu uweze kutekelezwa ni lazima nchi zilizosaini mkataba ziridhie. Aidha, utaratibu wa kuridhia mkataba huu umeoneshwa katika Ibara ya 30 ya Mkataba wenyewe ambao unazitaka nchi hizo kuridhia mkataba huu na kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 6 Septemba, 2019 jumla ya nchi 113 zilikuwa zimeridhia mkataba huu zikiwemo nchi 30 za Bara la Afrika na ulianza kutekelezwa tarehe 16 Agosti, 2017. Aidha, kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania, zimesaini mkataba huo, nchi ya Rwanda imeridhia tarehe 29 Juni, 2017 nchi ya Uganda imeridhia tarehe 01 Machi, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA zebaki ni miongoni mwa kemikali zinazohatarisha zaidi afya ya jamii duniani kutokana na kudumu katika mazingira kwa muda mrefu, kusafiri masafa marefu kwa njia ya hewa, maji yaani mito, maziwa na bahari na udongo na hivyo, kuathiri afya za binadamu na mazingira;

NA KWA KUWA athari kwa afya ya binadamu na mazingira kutokana na matumizi ya zebaki zinajitokeza zaidi kwa nchi zinazoendelea kuliko nchi zilizoendelea na kuhatarisha vizazi vya sasa na vijavyo;

NA KWA KUWA madhara kwa afya za mazingira kutokana na uchafuzi unaochangiwa na zebaki yamedhihirika kuwa makubwa, kuna umuhimu wa kuhakikisha usimamizi thabiti wa zebaki na kuepuka madhara katika siku zijazo;

KWA KUWA hadi hivi sasa jumla ya nchi 113 zimeridhia mkataba huu ambao ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 16 Agosti, 2017 mara baada ya nchi 50 kuridhia, kama inavyotakiwa na Ibara ya 30 ya Mkataba wa Minamata;

NA KWA KUWA baada ya kuridhia Mkataba wa Minamata Tanzania itaweza kushurikiana kikamilifu na nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata katika kukuza ushirikiano katika kupunguza uchafuzi utokanao na zebaki na hivyo, kuimarisha hifadhi ya mazingira na afya ya jamii, kujenga uwezo wa kitaalamu, kiteknolojia na kifedha ili kuimarisha udhibiti na usimamizi wa zebaki;

NA KWA KUWA Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 inahimiza kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo;

NA KWA KUWA hakutakuwa na gharama ya ziada kwa wanachama wa Mkataba wa Minamata kutokana na kuridhia mkataba huu, zaidi ya ada ya uanachama ya kila mwaka inayokadiriwa kufikia shilingi milioni tano;

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na kuridhia Mkataba wa Minamata kwa Tanzania ikiwemo haki ya kupiga kura kwenye mikutano mikuu ya nchi wanachama pamoja na shughuli nyingine. Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa mwaka 2013 *(The Minamata Convention on Mercury of 2013).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waziri tunakushukuru sana kwa wasilisho lako zuri, imetiririka vizuri na inaeleweka.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira awasilishe taarifa yake kuhusiana na Azimio hili; una muda usiozidi dakika 20.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa mwaka 2013 *(Minamata Convention on Mercury of 2013)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa mwaka 2013. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 53(6)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge yaViwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa mwaka 2013 *(Minamata Convention on Mercury of 2013)* ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge. Kamati ilijadili

na kuchambua hoja hii na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao umelenga kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna Kamati Ilivyoshughulikia hoja hii; katika kushughulikia hoja hii Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge, Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu:-

Kwanza tulianza na semina ya kuijengea uelewa Kamati juu ya Mkataba wa Minamata ambapo tarehe 1 Septemba, 2019 Kamati ilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na kupatiwa semina hiyo. Semina hii ilisaidia sana kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni kadri inavyoona inafaa. Tunawashukuru wawezeshaji wote wa semina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali juu ya pendekezo la kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki maelezo ya Serikali yaliwasilishwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira siku ya tarehe 4 Septemba, 2019 yalifafanua kwa kina nia ya Serikali kutaka kutatua changamoto za matumizi ya kemikali ya zebaki. Maelezo haya yalilenga kuishawishi Kamati na hatimaye Bunge kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa mwenyekiti, kupokea maoni ya wadau katika kutekeleza jukumu hili; Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 117(9) kuhusu utaratibu wa Kamati kuwaalika wadau ambapo wadau waliokuwa na maoni ya Mkataba huu wa Minamata walipata fursa ya kuyawasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawashukuru wadau wote waliofanikiwa kuwasilisha maoni yao kuhusu mkataba huu, maoni yao yalisaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu mkataba huu na hatimaye kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; Mkataba wa Minamata unalenga kulinda afya ya binadamu

na mazingira dhidi ya uchafuzi unaotokana na zebaki unaochangiwa na shughuli za binadamu. Zebaki ni miongoni mwa kemikali hatarishi na ina madhara ya afya ya jamii na mazingira kwa ujumla kutokana na kuwa na sifa ya kudumu na muda mrefu katika mazingira, uwezo mkubwa wa kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, uchafuzi wa mfumo wa chakula kutoka kwenye maji kwenda kwenye mmea na hatimaye kumfikia mlaji, kutoka kwenye maji kuingia kwenye viumbe vya majini na hatimaye kumfikia mlaji.

Kwa kuzingatia madhara hayo Kamati inaona kuwa umuhimu wa nchi kuridhia mkataba huu kwa lengo la kushirikiana na nchi nyingine kutafuta suluhisho la zebaki bila ya kuathiri shughuli za binadamu hususan shughuli ya uchimbaji mdogo, hivyo basi Kamati inalishauri Bunge lako kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huo wa kuridhia yapo baadhi ya maeneo ambayo Kamati imeona ni vyema yakazingatiwa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3 ya mkataba inapiga marufuku kuanzishwa kwa migodi mipya ya zebaki, kwa migodi iliyopo imepewa kipindi cha mpito cha miaka 15 tangu tarehe ya kuanza utekelezaji wa mkataba ambayo ilikuwa ni Agosti, 2017 iwe imeacha uchimbaji hatua ambayo hii inaashiria kutoweka kwa kemikali ya zebaki ambayo ni jambo jema, lakini inaashiria kupotea kwa wachimbaji wadogo pia kama jitihada za dhati hazitachukuliwa kupata mbadala wa zebaki kamati inashauri Serikali kuzitumia taasisi zake za *GST* na *STAMICO* kufanya tafiti ambazo zitawezesha upatikanaji wa teknolojia mbadala ambayo itakuwa rahisi na ya gharama nafuu ili kuwasaidia wachimbaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza hapa kuwa watumiaji wa zebaki ni wale wachimbaji wadogo sana ambao pia uwezo wao wa mitaji ni mdogo sana na hawataweza kumudu hiyo teknolojia mbadala kama itakuwa ya gharama ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wapo tayari kutumia mbadala wa zebaki pindi utakapopatikana kwa kuwa lengo lao ni kuendelea na shughuli yao ya uchimbaji na kujipatia kipato ili waweze kuendesha maisha yao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati ni kuwa Serikali ijitahidi kuhakikisha inapatikana teknolojia rahisi na rafiki kwa wachimbaji wadogo tena kwa gharama nafuu na kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa teknolojia itakayopatikana iwe ya gharama inayolingana au ndogo zaidi ya zebaki, kwa kuwa itakuwa na gharama kubwa wachimbaji wadogo hawataweza kumudu na matokeo yake matumizi ya zebaki hayataisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo itasababisha kuitoa zebaki katika mfumo wa kuuzwa na kutumika kihalali na badala yake itaanza kuuzwa na kutumika kwa kujificha ukizingatia udhibiti wa wachimbaji wadogo ni changamoto kwa kuwa shughuli za uchenjuaji zinaweza kuendelea hata kwa kuficha majumbani kwao bila ya kukamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi wa hili unajidhihirisha pale ambapo kuna baadhi ya teknolojia kemikali ambazo walau zina unafuu, lakini kutokana na gharama yake kuwa juu zinatumiwa na wachimbaji wa kati na hawa wadogo wameendelea kutumia zebaki licha ya kutambua madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wa Kamati ni kuwa Serikali kupitia taasisi za *GST* na *STAMICO* iharakishe kupata mbadala wa kemikali ya zebaki ili kuepuka madhara ya kemikali hii hususan katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 ya mkataba inazitaka nchi zilizoridhia mkataba huu kutenga fedha za kugharamia shughuli mbalimbali zinazolenga kufanikisha malengo ya mkataba kulingana na mazingira, shughuli za

nchi husika, kwa kuwa tunaenda kuridhia Kamati inaishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili kuipatia uwezo kutekeleza shughuli mbalimbali zinazoendana na mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri, kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati, nimshukuru pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene; Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa ofisi hiyo muhimu kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kujadili azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na naomba majina yao yote yaingie kwenye *Hansard* kwa ushirikiano waliotoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yao juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Kamati Bwana Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi, Bwana Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi Zainab Mkamba, Bi Mwajuma Ramadhani pamoja na wasaidizi wake akiwemo Ndugu Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuwasilisha na naunga mkono azimio hili. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA MINAMATA KUHUSU ZEBAKIWA MWAKA 2013 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

**(***Minamata Convention on Mercury of 2013***)**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa Mwaka 2013 (Minamata Convention on Mercury of 2013).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyochini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusuAzimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa mwaka 2013 (Minamata Convention on Mercury of 2013)ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Bunge.Kamati ilijadili na kuichambua hoja hii na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao umelenga kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu.

## 2.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia hoja hii Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu;-

i) Semina ya kuijengea uelewa Kamati juu yaMkataba wa Minamata, ambapo tarehe 1 Septemba, 2019 Kamatiilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingirana kupatiwa semina hiyo. Semina hii iliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni kadiri ilivyoona inafaa.

ii) Kupokea maelezo ya Serikali juu ya pendekezo la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki (Minamata Convention on Mercury of 2013). Maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira siku ya tarehe 4 Septemba, 2019, yalifafanua kwa kina nia ya Serikali kutaka kutatua changamoto ya matumizi ya kemikali ya zebaki. Maelezo haya yalilenga kuishawishi Kamati na hatimaye Bunge kuridhia Mkataba huu.

iii) Kupokea maoni ya Wadau,katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati kuwaalika wadau ambapo wadau waliokuwa na maoni juu ya Mkataba huu wa Minamata walipata fursa ya kuyawasilisha. Kamati inawashukuru wadau wote waliofanikiwa kuwasilisha maoni yao kuhusu Mkataba huu, maoni yenu yalisaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu Mkataba huu na hatimaye kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

## 3.0 CHIMBUKO LA MKATABA

**Mheshimiwa Spika**, chimbuko na asili ya mkataba huu ni matokeo ya tafiti zilizofanywa kwa takribani miaka 50 iliyopita ambazo zilibaini kuongezeka kwa changamoto za Zebaki duniani, hali iliyolazimu Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira kupitia Azimio Na. GC 21/5 la mwaka 2001 kuelekeza kufanyika kwa tathmini ya hali ya uchafuzi wa mazingira duniani.

**Mheshimiwa Spika,** tathimini ilifanyika na matokeo yake yaliwasilishwa katika kikao cha 22 cha Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira ambacho kilifanyika Mwaka2003 na ilidhihirisha mambo yafuatayo.

i) Zebaki hudumu katika mazingira kwa muda mrefu (miaka 2-20) na husafiri masafa marefu kwa njia ya hewa, maji (mito, maziwa na bahari) na udongo.

ii) Zebaki husafiri angani umbali hadi kilomita 1,000 kutoka kwenye chanzo; na kuathiri afya ya binadamu, viumbe wengine na mazingira.

iii) Athari hizi zinajitokeza zaidi katika nchi zinazoendelea ukilinganisha na nchi zilizoendelea kutokana na nchi hizo kupunguza matumizi ya Zebaki.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto tajwa ilipendekezwa kuchukuliwa hatua za pamoja za jumuiya ya kimataifa ikiwemo kuanzishwa Mkataba wa Minamata unaohusu usimamizi wa Zebaki. Mkataba huu ulipitishwa tarehe 10 Oktoba 2013 na nchi wanachama 128. Nchi zinazohusika na Mkataba huu ni nchi Wanachama wa Jumuiya ya Kimataifa (United Nations) ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama pia.

## 4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyomezani leo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baadhi ya Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa.Sheria iliyozingatiwa zaidi ni Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ambapo ilibainika kuwa Mkataba huu haukuwa unakinzana na Sheria hiyona badala yake utaiongezea nguvu katika kusimamia uhifadhi wa mazingira. Kamati pia ilijiridhisha nafaidazinazoweza kupatikana kutokana na kuridhia kama ulivyo, faida hizo ni pamoja na;-
i) Kuboresha uwezo wa kitaifa katika kudhibiti na kusimamia Zebaki kwa lengo la kukabiliana na athari za uchafuzi unaotokana na zebaki

ii) Tafiti na program zitakazotekelezwa chini ya mkataba zitakuwa shirikishi baina ya nchi wanachama kama inavyoelezewa katika **Ibara ya 17** na **Ibara ya 19** jambo litakalosaidia nchi kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya athari za zebaki lakini pia itasaidia kuimarika kwa sekta ya uchumi ikiwemo kilimo, uvuvi, mifugo na maji hatimaye kukuza ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilijiridhisha juu ya maudhui ya mkataba ambapo **Ibara ya 1** ambayo inaelezea kuwa Mkataba unalenga kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na uchafuzi wa mazingira unaosabaishwa na Zebaki

**Nanukuu**: ***Article 31(1)*** *"The objective of thisConvention is to protect the human health and the environment from anthropogenic emissions and releases of mercury and mercury compounds"* **Mwisho wa kunukuu**.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Minamata unalenga kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya uchafuzi utokanao na Zebaki unaochangiwa na shughuli za binadamu.Zebaki ni miongoni mwa kemikali hatarishi na ina madhara ya afya ya jamii na mazingira kwa ujumla kutokana na kuwa na sifa ya kudumu kwa muda mrefu katika mazingira; uwezo mkubwa wa kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine; uchafuzi wa mfumo wa chakula (kutoka kwenye maji kwenda kwenye mmea na hatimaye kumfikia mlaji, kutoka kwenye maji kuingia kwenye viumbe vya majini na hatimaye kumfikia mlaji).

Kwa kuzingatia madhara ya zebaki Kamati inaona kuna umuhimu wa nchi kuridhia Mkataba huu kwa lengo la kushirikiana na nchi nyingine kutafuta suluhisho la zebaki bila kuathiri shughuli za binadamu hususani shughuli ya uchimbaji mdogo. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako kuridhia Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri huo wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo kamati imeona ni vyema yakazingatiwa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3** ya Mkataba inapiga marufuku kuanzishwa kwa migodi mipya ya Zebaki na kwa migodi iliyopo imepewa kipindi cha mpito cha miaka kumi na tano (15) tangia tarehe ya kuanza utekelezaji wa Mkataba ambayo ilikuwaAgosti, 2017, iwe imeacha uchimbaji. Hatua hii inaashiria kutoweka kwa Kemikali ya zebaki ambalo ni jambo jema lakini inaashiria kupotea kwa wachimbaji wadogopia kama jitihada za dhati hazitachukuliwa kupata mbadala wa Zebaki. Kamati inaishauri Serikali kuzitumia taasisi zake za GST na STAMICO kufanya tafiti ambazo zitawezesha upatikanaji wa teknolojia mbadala ambayo itakuwa rahisi na yagharama nafuu ili kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kusisitiza hapa kuwa watumiaji wa zebaki ni wale wachimbaji wadogo sana ambao pia uwezo wao (mtaji) ni mdogo sana na hawataweza kumudu hiyo teknolojia mbadala kama itakuwa ya gharama ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** wachimbaji wadogo wapo tayari kutumia mbadala wa zebaki pindi utakapopatikanakwa kuwa lengo lao ni kuendelea na shughuli yao ya uchimbaji na kujipatia kipato ili waweze kuendesha maisha yao na familia zao. Ushauri wa Kamati ni kuwa Serikali ijitahidi kuhakikisha inapatikanateknolojia rahisi na rafiki kwa wachimbaji wadogo tena ya gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kuwateknolojia itakayopatikana iwe ya gharamainayolingana au ndogo zaidi ya zebaki kwa kuwa kama itakuwa na gharama kubwa wachimbaji wadogo hawataweza mudu na matokeo yakematumizi ya zebaki hayataisha. Hali hiyo itasababisha kuitoa zebaki katika mfumo wa kuuzwa na kutumika kihalali na badala yake itaanza kuuzwa na kutumika kwa kujificha, ukizingatia udhibiti wa wachimbaji wa dogo ni changamoto

kwa kuwashughuli ya uchenjuajizinaweza kuendelea hata kwa kujificha majumbani kwao bila kukamatwa.
Mfano halisi wa hili unajidhihirisha hata sasa ambapo kuna baadhi ya teknolojia (kemikali) ambazo walau zinaunafuu lakini kutokana na gharama yake kuwa juu zinatumiwa na wachimbaji wa kati na hawa wadogo wameendelea kutumia zebaki licha ya kutambua madhara yake.

**Mheshimiwa Spika**, msisitizo wa Kamati ni kuwa Serikali kupitia taasisi za GST na STAMICO iharakishe kupata mbadala wa kemikali ya zebaki ili kuepuka madhara ya kemikali hii hususani katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika,Ibara ya 14** ya Mkataba Inazitaka nchi zilizoridhia mkataba huu kutenga fedha za kugharamia shughuli mbalimbali zinazolenga kufanikisha malengo ya Mkataba kulingana mazingira/shughuli za nchi husika. Kwa kuwa tanaenda kuridhia, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ili kuipatia uwezo kutekeleza shughuli mbalimbali zinazoendana na Mkataba huu.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwakunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru piaMheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Musa Ramadhani Sima (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hiyo muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya

Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yao juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapo chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge: -

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Machano Othamn Said, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**
10 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa wasilisho lako taarifa ya Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusiana na azimio hili.

Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Cecil Mwambe, muda usiozidi dakika 20.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika azimio la kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki *(Minamata Convention on Mercury)* yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni ya Bunge, toleo la mwaka 2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Mkataba huu wa Minamata ni kulinda afya za binadamu pamoja na mazingira yanayomzunguka kutokana na madini hatari ya zebaki. Japokuwa madini ya zebaki yana umuhimu mkubwa kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu, lakini madini haya pia yametajwa kuwa na athari nyingi za afya ya mwanadamu kwa miaka mingi pasipo wengi kufahamu athari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo baadhi ya machapisho ya wataalamu wa afya yanaonesha athari za zebaki ni pamoja na kuathiri ubongo, kubadili mfumo wa

kawaida wa vinasaba vya binadamu, kuharibu figo, kusababisha upungufu wa nguvu za kiume, magonjwa ya ngozi pamoja na kuharibu mimba kwa wamama wajawazito.

Pia inatajwa kusabaisha uchovu wa mwilini na kumfanya mtu ambaye ameathirika kuwa na usingizi wa mara kwa mara, hii ni pamoja na kupata kichefuchefu pamoja na kusababisha upofu huku kemikali hii ikiwekewa tahadhari kwamba inasababisha ulemavu wa kudumu kwenye viungo vya mwili na kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,zebaki ya aina yoyote ile inakuwa na kiwango cha hewa ya ukaa *(carbon monoxide)* na kwamba zebaki zamani ilikuwa ikitumika kama dawa ya kuua wadudu majumbani na nyingine ikitumiwa hospitalini kuziba meno na kupima joto la binadamu kwa njia ya *thermometer*. Zebaki inao uwezo wa kusababisha wanawake wajawazito kuzaa watoto wenye ulemavu. Vilevile anasema ikiwa mbegu za kiume na za kike zinakuwa zimeathiriwa na zebaki inawezekana kutokana na kutengeneza mtoto zinakuwa na mapungufu wa kimfumo katika vinasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaonyesha kuwa viwango vya zebaki duniani vinaendelea kuongezeka vikichochewa kila siku na shughuli za wanadamu zikiwemo uchomaji wa makaa ya mawe na uchimbaji wa madini ya dhahabu. Zebaki huingia kwenye vyanzo vya maji baada ya kutumika kuchenjulia madini aina ya dhahabu na hatimaye kuingia kwenye mwili wa binadamu kupitia ulaji wa samaki waliovuliwa kwenye maji hayo yenye madini ya zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kemikali hiyo hutumika kwa wingi katika maeneo yenye uchimbaji mdogo wa dhahabu wakati wa kuchenjua mchanga na kukamata dhahabu. Zebaki pia au *mercury* huwekwa kwenye karai lenye mchanga pamoja na maji kwa ajili ya kukorogwa na mikono ili kemikali hiyo iweze kuenea kwenye udongo huo. Pamoja na kemikali hiyo kuwa na muhimu katika kukamilisha zoezi zima la upatikanaji wa dhahabu katika migodi ya wachimbaji wadogo, lakini kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu, inaelezwa

kwamba zebaki ni kemikali hatari kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zebaki inapatikana kutokana na kemikali iliyopo kwenye chini ya mwamba ulioko chini ya ardhi unaofahamika kitaalamu kama *cinnabar ore.* Miamba ya *cinnabar ore* kuchimbwa na kusagwa kwenye mashine halafu unga wake huchemshwa kwenye maji na kwamba mvuke unaopatikana unakingwa kwenye kifaa maalumu ambacho hupoza mvuke huo hadi unageuka kuwa zebaki. Aidha, kemikali inayotokana na mwamba huo *(cinnabar ore)* ina uwezo wa kujitengeneza yenyewe ikiwa chini ya ardhi au ikichimbwa na kuzalishwa viwandani kwa njia za kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo aina nyingine ya zebaki inayoitwa *methyl mercury* hii ni kemikali hatari, hii mara nyingi hujitengeneza yenyewe chini ya ardhi, ina uwezo wa kuua haraka sana kwa sababu kiwango chake cha hewa ukaa *(carbon monoxide)* ni kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wachimbaji wadogo wengi hawana uelewa wa athari na madhara ya kiafya yatokanayo na matumizi ya zebaki na kuichukulia kawaida kama kitu kisicho na madhara, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili imeandaa mpango mkakati gani wa kutoa elimu juu ya athari za zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kutoa elimu ya madhara ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ambao wanatumia kemikali hiyo kwa ajili ya uchenjuaji. Hii ni kwa sababu baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaonekana wakichoma kwenye moto dhahabu iliyopatikana huku moshi uliochanganyika na mvuke wa zebaki ukifuka moja kwa moja kuelekea usoni mwao ilhali hawana kitu chochote cha kujikinga na mvuke huo unaotajwa kuwa hatari kwa afya zao, kwa sababu mvuke huo una hewa ya ukaa ndani yake ambayo ni hatari

zaidi, wanawake wakifua magunia yaliyotumika kuosha mchanga pamoja na nguo zao wanazovaa wakizifua karibu na vyanzo vya maji, hali inayoashiria mabaki ya zebaki huenda yakawa yanaingia katika vyanzo hivyo ambavyo hutegemewa kwa matumizi mbalimbali ya watu na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ambayo katika uridhiwaji wa itifaki hii ilitakiwa itoe suluhisho hasa kwa nchi zinazoendelea zenye wachimbaji wadogo wadogo wengi wa dhahabu huitumia zebaki katika uchenjuaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba hatuna mbadala wa matumizi ya zebaki kwa watu hawa na wachimbaji wadogo wa kiwango cha chini, zebaki ndiyo mkombozi wao, wao wanaona ni bora kuitumia kujipatia riziki hata kama itasababisha madhara ya kiafya katika miili yao. Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanyika kwenye migodi inayomilikiwa na kuendeshwa na wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu katika maeneno mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la itifaki; itifaki hii ya kimataifa chimbuko lake ni ugonjwa wa Minamata ambao ulipewa jina la mji mmoja huko nchini Japan kwenye ghuba inayofahamika kama Kyushu ulipozuka ugonjwa huo na hivyo ugonjwa ukapewa jina la mji wa Minamata. Ugonjwa huo uliua watu takriban 900 na kuacha wengine zaidi ya 2,265 wakiwa na ulemavu wa kudumu katika miili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa mwaka 1956 ambapo wananchi wa mji wa Minamata walishuhudia wagonjwa wanne wakipatwa na homa kali, naomba isomeke hivyo kwenye taarifa hiyo badala ya neno malaria, kifafa pamoja na kupoteza kumbukumbu kwa haraka hali iliyosababisha wagonjwa hao kupoteza maisha kwa muda mfupi. Ugonjwa huo pia uliwapata paka, ambao nao walikuwa wakipata vichaa hadi kufa kila walipokuwa wakila samaki waliovuliwa katika maji ya ghuba ya Kyushu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tukio hilo, ilibainika kuwa chanzo cha ugonjwa huo ni samaki waliokuwa wakivuliwa katika maji ya ghuba hiyo, kwani baada ya kula samaki hao wavuvi wengine 13 wa mji wa Minamata walikufa kwa dalili zilezile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wagonjwa wengine walizidi kuugua, baadaye uchunguzi uliofanyika na kubaini chanzo cha vifo hivyo, ilibainika kuwa zebaki aina ya *methyl mercury* iliyokuwa ikimwagwa katika maji ya ghuba hiyo kutoka kwenye kiwanda kilichokuwa kikizalisha kemikali zitokanazo na mimea ndizo zilileta athari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ulionesha kuwa zebaki iliyokuwa ikizalishwa kwenye kiwanda hicho baada ya kutupwa kwenye maji iliathiri samaki, ambapo watu wote waliokula samaki hao walipata madhara na wengine kufa. Taarifa mbalimbali zinazochambua tukio hilo zinaonyesha kuwa hata sasa athari hizo zipo na zinawakumba watu wa ghuba hiyo na kwamba tukio hilo limeacha alama inayoonesha madhara ya zebaki kwa dunia nzima. Kutokana na athari hizo, kemikali ya zebaki inapigwa vita duniani kote kutumiwa katika matumizi ya kawaida na ya kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na ukweli huo zebaki inaathari za kiafya za watu bila wao kujua madhara yake yanayoweza kudumu kizazi hadi kizazi, kwani baada ya kuingia mwilini hubadili vinasaba vya mwathirika na kuyageuza madhara yake kuwa ya kurithishana. Zebaki pia ina uwezo wa kuathiri mazingira na viumbe wengine wanaopatikana katika mazingira hayo kama ng’ombe, mbuzi na wanyama wengine. Binadamu akila nyama ya wanyama hao huweza kupata madhara ya zebaki inayowezakuwa ndani ya nyama ya wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya mkataba; matumizi makubwa ya zebaki katika nchi yetu yapo kwenye sekta ya uchimbaji wa dhahabu na kiasi kikubwa ni kwa wachimbaji wadogo na watu hao ni waathirika wakubwa na pia ndio chanzo cha kuingia zebaki kwenye vyanzo

vikubwa vya maji yanayotumiwa na jamii kubwa ya Watanzania, kama vile maziwa na mito mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2 inayohusu tafsiri; kuna maneno yaliyotumiwa ya *best available techniques*, kuwa ni mujarabu za kuzuia, kupunguza matumizi ya uzalishaji na utoaji wa zebaki kwenye hewa, maji na ardhi katika uhifadhi wa mazingira. Nchi wanachama zinahitaji kufikia kiwango kinachohitajika katika ulinzi wa mazingira kwa ujumla wake. Katika tafsiri hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, katika mazingira na hali ya uchumi kwa wananchi wetu, hizo zinazoitwa *the best available techniques* ni zipi ili watumiaji wakuu wa zebaki waweze kutumia njia hizo katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3 inazungumza vyanzo na biashara ya zebaki, ni ukweli kuwa Tanzania haizalishi wala kuchimba zebaki, lakini inaagiza zebaki nyingi na bidhaa ambazo zinatengenezwa na zebaki. Aidha, kuna vyanzo vikuu vya zebaki *(mercury compound sources)* hapa nchini na hivyo kuwa na uchafuzi wa hewa, vyanzo hivyo ni kama vile mitambo inayoendeshwa kwa kutumia makaa ya mawe, uzalishaji wa cement kwa kutumia *clinker* na kadhalika. Vyanzo hivi vimeelezewa katika kiambatanisho D cha Mkataba. Hoja ni je, kweli Tanzania tukisharidhia itifaki tutaweza kutimiza matakwa ya mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4 katika aya ya kwanza kinachosema kuwa kila nchi mwanachama haitaruhusu uzalishaji, uagizaji wa bidhaa zenye zebaki pale tarehe ya mwisho iliyowekwa katika mkataba huu kumalizika *(date after which the manufacture, import of the product shall not be allowed (phase out date)* na tarehe iliyowekwa ya mwisho wa matumizi ni mwaka 2020. Tanzania tunaridhia leo maana yake tumebakiza kipindi cha mwaka mmoja tu, na bidhaa zilizwekwa kwenye kiambatanisho A cha mkataba ni bidhaa nyingi zinazotumia umeme na visivyotumia umeme (vifaa vya elektroniki). Hoja ya msingi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ni je, tumejiandaaje kuwa na

mbadala wa bidhaa yenye zebaki na wafanyabiashara wameelimishwa vipi kuhusu jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba katika Ibara ya 7 imetambua matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo ambao uwekezaji wao katika uzalishaji wa dhahabu ni mdogo, lakini licha ya kuonesha madhara makubwa kiafya na wachimbaji wadogo kuwa ni chanzo kikuu cha *contamination* ya zebaki kwenye ardhi na maji, bado mkataba huu hautoi njia mbadala kwa hao watumiaji wakubwa wa zebaki, badala yake mkataba unatoa ushauri wa kujilinda tu kama kiambatanisho C kinavyoonesha, lakini matumizi yake yako pale pale. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu jambo hili la njia mbadala ili marufuku ya matumizi ya zebaki hapa nchini yawekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 32 inasema wazi kuwa hatutakuwa na stara *(reservations)* yoyote itakayofanyika katika mkataba huo. Kwa maana hiyo, kama unaridhia, unaridhia kila kifungu na kama unaacha kuridhia, unaacha mkataba mzima. Na kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani, masharti yaliyowekwa katika vifungu ukweli ni kwamba itakuwa ni ngumu kutekelezeka katika mazingira halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kama ambavyo tumeeleza hapo juu awali, zebaki ni madini ambayo yanakaa sana katika ardhi, mimea, viumbe hai na hivyo madhara yake kwa afya za binadamu na wanyama hawa kuwa rahisi kutoka sehemu kwenda nyingine. Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania na ambavyo kuna rasilimali ya dhahabu na matumizi makubwa ya dhahabu ni wachimbaji wadogo na hao hutumia zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu na kufanya matumizi ya zebaki kuwa ni jambo la kawaida sana kwao bila kuwa na ufahamu wa madhara yake kwenye mazingira ya afya zao itakuwa ni ngumu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa maeneo mengi yenye wachimbaji wadogo kunakuwa na mito midogo

ambayo wakati wa masika inaungana na mito mikubwa ambayo ni chanzo kikuu cha maji ya maeneo hayo. Hivyo, kwa kutokufahamu au kufahamu lakini kukosekana kwa utashi kunasababisha kuwepo na uwezekano mkubwa kwa idadi kubwa ya Watanzania katika maeneo mbalimbali wamekwishaathirika na madhara yatokanayo na zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halina ubishi kwa wakazi wanaotumia maji ya Mto Ruvu ambao unapita Morogoro Kusini, ambako kuna wachimbaji wadogo wa dhahabu na katika uchenjuaji wa dhahabu uwezekano ni mkubwa kutiririsha maji yenye zebaki kwenye Mto Ruvu. Ukienda Kanda ya Ziwa mambo ni yaleyale na ukienda Tanga, Wilaya ya Kilindi uwezekano ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa kwa mkataba huu itasaidia sana kuisaidia Serikali juu ya udhibiti wa matumizi ya zebaki hasa kwenye uchenjuaji wa dhahabu, lakini itakuwa ni busara pia kwa Serikali kutafuta kwa kushirikiana na Sekretarieti kwa mujibu wa kazi zake chini ya Ibara ya 24 ya Mkataba ili kutafuta kutumia kile kinachoitwa *the best available technique* katika kuhakikisha matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu yanaoneshwa na upungufu wake kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi inayochafuliwa na zebaki chochote kinachooteshwa hapo huota kwa kutumiwa na binadamu na mnyama au ndege, basi mimea itakayopeleka zebaki kwa binadamu au wanyama imetumika mimea hiyo na zebaki inabaki ardhini kwa kipindi kirefu sana, hii ni kuonesha jinsi ilivyokuwa na hatari sana kwa mazingira yanayozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haina pingamizi lolote juu ya uridhiwaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kurudia, Kambi Rasmi ya Upinzani haina pingamizi lolote juu ya uridhiwaji wa

mkataba huu kutokana na ukweli kwamba madhara ya zebaki kwa binadamu na wanyama na mimea ni hatari sana kulinganisha na magonjwa mengine ambayo yamezoeleka katika jamii yetu. Kwa muktadha huo, chochote kitakachotoa njia mujarabu za kudhibiti matumizi yake katika nchi yetu ni jambo muafaka kwa maendeleo ya Watanzania. Maendeleo kwa kiwango kikubwa yanaakisiwa na afya watu katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kurudia; kama inavyoelezwa hapo juu Kwa muktadha huo, chochote kitakachotoa njia mujarabu za kudhibiti matumizi yake katika nchi yetu ni jambo muafaka kwa maendeleo ya Watanzania. Maendeleo kwa kiwango kikubwa yanaakisiwa na afya za watu katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mimi Cecil David Mwambe ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KATIKA AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA MINAMATA KUHUSU ZEBAKI (*MINAMATA CONVENTION ON MERCURY)* - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni ya Bunge, toleo la mwaka 2016)"*

**1. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Mkataba huu wa Minamata ni kulinda afya za binadamu pamoja na mazingira yanayomzunguka kutokana na madini hatari ya zebaki. Japokuwa madini ya zebaki yana umuhimu mkubwa kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu, lakini madini haya pia yametajwa kuwa na athari nyingi za afya ya mwanadamu kwa miaka mingi pasipo wengi kufahamu athari zake.

2. **Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo baadhi ya machapisho ya wataalamu wa afya yanaonyesha athari za zebaki ni pamoja na kuathiri ubongo, kubadili mfumo wa kawaida wa vinasaba vya binadamu, kuharibu figo, kusababisha

upungufu wa nguvu za kiume, magonjwa ya ngozi pamoja na kuharibu mimba kwa wajawazito.

Pia inatajwa kusabaisha uchovu mwilini na kumfanya mtu ambaye ameathirika kuwa na usingizi wa mara kwa mara, kuwa na kichefuchefu pamoja na kusababisha upofu huku kemikali hii ikiwekewa tahadhari kwamba inasababisha ulemavu wa kudumu kwenye viungo vya mwili na kansa.

**3.** **Mheshimiwa Spika**, zebaki ya aina yoyote ile inakuwa na kiwango cha hewa ya ukaa (Carbon monoxide) na kwamba zebaki zamani ilikuwa ikitumika kama dawa ya kuua wadudu majumbani na nyingine ikitumiwa hospitalini kuziba meno na kupima joto la binadamu kwa njia ya *thermometer*. Zebaki inao uwezo wa kusababisha wanawake wajawazito kuzaa watoto vilema. Vilevile anasema ikiwa mbegu za kiume na za kike zitakuwa zimeathiriwa na zebaki zinapokutana na kutengeneza mtoto zinakuwa na upungufu wa kimfumo katika vinasaba.

**4.** **Mheshimiwa Spika**, utafiti unaonyesha kuwa viwango vya zebaki duniani vinaendelea kuongezeka vikichochewa kila siku za shughuli za mwanadamu zikiwemo uchomaji wa makaa ya mawe na uchimbaji wa madini ya dhahabu. Zebaki huingia kwenye vyanzo vya maji baada ya kutumika kuchenjulia madini aina ya dhahabu na hatikamaye kuingia kwenye mwili wa binadamu kupitia ulaji wa samaki waliovuliwa kwenye maji hayo yenye madini ya Zebaki.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, Kemikali hiyo hutumika kwa wingi katika maeneo yenye uchimbaji mdogo wa dhahabu wakati wa kuchenjua mchanga na kukamata dhahabu. Zebaki au Mercury huwekwa kwenye karai lenye mchanga pamoja na maji kwa ajili ya kukorogwa kwa mikono ili kemikali hiyo iweze kuenea kwenye udongo huo. Pamoja na kemikali hiyo kuwa muhimu katika kukamilisha zoezi zima la upatikanaji wa dhahabu katika migodi ya wachimbaji wadogo, lakini kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu; inaelezwa kwamba Zebaki ni kemikali hatari kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

6. **Mheshimiwa Spika**, Zebaki inapatikana kutokana na kemikali iliyopo kwenye mwamba ulioko chini ya ardhi unaofahamika kitaalamu kama 'Cinnabar Ore'. Miamba ya 'Cinnabar Ore' kuchimbwa na kusagwa kwenye mashine halafu unga wake kuchemshwa kwenye maji na kwamba mvuke unaopatikana unakingwa kwenye kifaa maalumu ambacho hupoza mvuke huo hadi unageuka kuwa zebaki. Aidha, Kemikali inayotokana na mwamba huo (Cinnabar Ore) ina uwezo wa kujitengeneza yenyewe ikiwa chini ya ardhi au ikachimbwa na kuzalishwa viwandani kwa njia za kitaalamu.

7. **Mheshimiwa Spika**, ipo aina nyingine ya zebaki inayoitwa 'Methylmercury' hii ni kemikali hatari, hii mara nyingi hujitengeneza yenyewe chini ya ardhi, ina uwezo wa kuua haraka sana kwa sababu kiwango chake cha hewa ukaa, Co (Carbon monoxide) ni kikubwa.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wachimbaji wadogo wengi hawana uelewa wa hatari na madhara ya kiafya yatokanayo na matumizi ya zebaki na kuichukulia kawaida kama kitu kisicho na madhara; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili imeandaa mpango mpango mkakati gani wa kutoa elimu juu ya athari za Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

9. **Mheshimiwa Spika,** ni muhimu sana kutoa elimu ya madhara ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ambao wanatumia kemilkali hiyo kwa ajili ya uchenjuaji**.** Hii ni kwa sababu baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wameonekana wakichoma kwenye moto dhahabu iliyopatikana huku moshi uliochanganyika na mvuke wa zebaki ukifuka moja kwa moja kuelekea usoni mwao, ilhali hawana kitu chochote cha kujikinga na mvuke huo unaotajwa kuwa hatari kwa afya zao, kwa sababu mvuke huo una hewa ya ukaa ndani yake ambayo ni hatari zaidi. Wanawake wakifua magunia yaliyotumika kuosha mchanga pamoja na nguo zao wanazovaa wakivifua karibu na vyanzo vya maji, hali inayoashiria mabaki ya zebaki huenda yakawa

yanaingia katika vyanzo hivyo ambavyo hutegemewa kwa matumizi mbalimbali ya watu na wanyama.

**10.** **Mheshimiwa Spika,** hoja ya msingi ambayo katika urudhiwaji wa Itifaki hii ilitakiwa itoe suluhisho hasa kwa nchi zinazoendelea ambazo zenye wachimbaji wadogo wadogo wengi wa dhahabu huitumia zebaki katika shughuli zao kwani hawawezi kuimudu teknolojia ya kutumia kemikali ya 'Cyanide' ambayo ni nzuri kwa uzalishaji wa dhahabu, mbadala wake ni nini?

**11.** **Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kwamba hatuna mbadala wa matumizi ya zebaki kwa watu au wachimbaji wadogo wa kiwango cha chini, zebaki ndiyo mkombozi wao, wao wanaona ni bora kuitumia kujipatia riziki hata kama itasababisha madhara ya kiafya katika miili yao. Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanyika kwenye migodi inayo milikiwa na kuendeshwa na wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu katika maeneno mbalimbali ya nchi yetu.

## 2. CHIMBUKO LA ITIFAKI

**12.** **Mheshimiwa Spika**, itifaki hii ya kimataifa chimbuko lake ni ugonjwa wa Minamata ambao ulipewa jina la mji mmoja huko Nchini Japan kwenye ghuba inayofahamika kama Kyushu ulipozuka ugonjwa huo, na hivyo ugonjwa ukapewa jina la mji wa *Minamata*. Ugonjwa huo uliua watu takriban 900 na kuacha wengine zaidi ya 2,265 wakiwa na ulemavu wa kudumu katika miili yao.

**13.** **Mheshimiwa Spika**, Ilikuwa mwaka 1956, ambapo wananchi wa mji wa Minamata walishuhudia wagonjwa wanne wakipatwa na malaria kali, kifafa pamoja na kupoteza kumbukumbu kwa haraka, hali iliyosababisha wagonjwa hao kupoteza maisha kwa muda mfupi. Ugonjwa huo pia uliwapata paka, ambao nao walikuwa wakipata vichaa hadi kufa kila walipokuwa wakila samaki waliovuliwa katika maji ya ghuba ya Kyushu.

Baada ya tukio hilo, ilibainika kuwa chanzo cha ugonjwa huo ni samaki waliokuwa wakivuliwa katika maji ya ghuba hiyo,

kwani baada ya kula samaki hao wavuvi wengine 13 wa mji wa Minamata walikufa kwa dalili zilezile.

Hata hivyo, wagonjwa wengine walizidi kuugua, baadaye uchunguzi ulipofanyika wa kubaini chanzo cha vifo hivyo, ilibainika kuwa zebaki aina ya 'Methylmercury' iliyokuwa ikimwagwa katika maji ya ghuba hiyo kutoka kwenye kiwanda kilichokuwa kikizalisha kemikali zitokanazo na mimea ndizo zilileta athari hiyo.

**14. Mheshimiwa Spika,** utafiti ulionyesha kuwa zebaki iliyokuwa ikizalishwa kwenye kiwanda hicho baada ya kutupwa kwenye maji iliathiri samaki, ambapo watu wote waliokula samaki hao walipata madhara na wengine kufa. taarifa mbalimbali zinazochambua tukio hilo zinaonyesha kuwa hadi sasa athari hizo bado zinawakumba watu wa ghuba hiyo na kwamba tukio hilo limeacha alama inayoonyesha madhara ya zebaki kwa dunia nzima. Kutokana na athari hizo, kemikali ya zebaki inapigwa vita duniani kote kutumiwa katika matumizi ya kawaida ya kibinadamu.

**15. Mheshimiwa Spika**, Ni kutokana na ukweli huo; Zebaki inaathiri afya za watu bila wao kujua madhara yake yanayoweza kudumu kizazi hadi kizazi, kwani baada ya kuingia mwilini hubadili vinasaba vya mwathirika na kuyageuza madhara yake kuwa ya kurithishana. Zebaki pia ina uwezo wa kuathiri mazingira na viumbe wengine wanayopatikana katika mazingira hayo kama ng'ombe, mbuzi na wanyama wengine. Binadamu akila nyama ya wanyama hao huweza kupata madhara ya zebaki inayokuwa ndani ya nyama ya wanyama hao.

## 3. MAPITIO YA MKATABA

**16. Mheshimiwa Spika,** matumizi makubwa ya zebaki katika nchi yetu yapo kwenye sekta ya uchimbaji wa dhahabu na kiasi kikubwa ni kwa wachimbaji wadogo wadogo, na watu hao ndio waathirika wakubwa na pia ndio chanzo cha kuingia zebaki kwenye vyanzo vikubwa vya maji

yanayotumiwa na jamii kubwa ya watanzania, kama vile maziwa na mito mikubwa.

**17. Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 2 inayohusu tafsiri, kuna maneno yaliyotumiwa ya "Best available techniques", kuwa ni mujarabu za kuzuia, kupunguza matumizi ya uzalishaji na utoaji wa zebaki kwenye hewa, maji na ardhi katika uhifadhi wa mazingira, nchi mwanachama zinahitaji kufikia kiwango kinachohitajika katika ulinzi wa mazingira kwa ujumla wake. Katika tafsiri hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, katika mazingira na hali ya uchumi kwa wananchi wetu, hizo zinazoitwa "the best available techniques" ni zipi ili watumiaji wakuu wa zebaki waweze kutumia njia hizo katika shughuli zao za kila siku.

**18. Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 3 inazungumzia vyanzo na biashara ya Zebaki, ni ukweli kuwa Tanzania haizalishi wa kuchimba Zebaki, lakini inaagiza Zebaki nyingi na bidhaa ambazo zinatengenezwa na Zebaki. Aidha kuna vyanzo vikuu vya Zebaki *Mercury Compound Sources* hapa nchini *na hivyo kuwa ni uchafuzi wa hewa, vyanzo hivyo ni* kama vile mitambo inayoendeshwa kwa kutumia makaa ya mawe, uzalishaji wa cement clinker n.k. Vyanzo hivi vimeelezewa katika kiambatanisho D cha Mkataba. Hoja ni je, kweli Tanzania tukisharidhia itifaki tutaweza kutimiza matakwa ya Mkataba?

**19. Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 katika aya ya 1 kinachosema kuwa kila nchi mwanachama haitaruhusu uzalishaji, uagizaji wa bidhaa zenye zebaki pale tarehe ya mwisho iliyowekwa katika Mkataba huu kumalizika ***(Date after which the manufacture, import of the product shall not be allowed (phase out date)),*** na tarehe iliyowekwa ya mwisho wa matumizi ni mwaka 2020. Tanzania tunaridhia leo maana yake tumebakiza kipindi cha mwaka mmoja tu, na bidhaa zilizwekwa kwenye kiambatanisho **A** cha mkataba ni bidhaa nyingi zinazotumia umeme na visivyotumia umeme (vifaa vya elektroniki).Hoja ya msingi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ni je tumejiandaaje kuwa na mbadala wa

bidhaa zenye Zebaki na wafanyabiashara wameelimishwa vipi kuhusu jambo hili.?

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Mkataba katika Ibara ya 7 imetambua matumizi makubwa ya Zebaki kwa Wachimbaji wadogo ambao uwekezaji wao katika uzalishaji wa dhahabu ni mdogo, lakini licha ya kuonesha madhara makubwa kiafya na wachimbaji wadogo kuwa ni chanzo kikuu cha "contamination" ya Zebaki kwenye ardhi na maji, bado Mkataba huu hautoi njia mbadala kwa hao watumiaji wakubwa wa Zebaki, Badala yake mkataba unatoa ushauri wa kujilinda tu kama Kiambatanisho **C** kinavyoonesha, lakini matumizi yako pale pale. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu jambo hili la njia mbadala ili marufuku ya matumizi ya zebaki hapa nchini yawekwe.

**21.** **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 32 inasema wazi kuwa hakutakuwa na stara(reservations) yoyote itakayofanyika katika Mkataba huu. Kwa maana hiyo kama unaridhia unaridhia kila kifungu na kama unaacha kuridhia unaacha mkataba mzima. Na kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani masharti yaliyowekwa katika vifungu, ukweli ni kwamba itakuwa ni ngumu kutekelezeka katika mazingira halisi ya nchi yetu.

## 4. HITIMISHO

**22.** **Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo tumeeleza hapo awali Zebaki ni madini ambayo yanakaa sana katika ardhi, katika mimea na katika viumbe hai na hivyo madhara yake kwa afya za binadamu na wanyama kuwa rahisi kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania na ambayo kuna rasilimali ya dhahabu na wagunduzi wakubwa wa dhahabu ni wachimbaji wadogo; na hao utumia Zebaki katika uchenjuaji wa dhahaba na kufanya matumizi ya Zebaki kuwa ni jambo la kawaida sana kwao, bila kuwa na ufahamu wa madhara yake kwenye mazingira na afya zao kwa ujumla.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kuwa maeneo mengi yenye wachimbaji wadogo kuna kuwa na mito ambayo midogo ambayo wakati wa masika inaunga na mito mikubwa ambayo ni chanzo kikubwa kwa maji yanayotumika mijini. Hivyo kwa kutokufahamu au kufahamu lakini kukosekana na utashi kunasababisha kuwepo na uwezekano mkubwa kwa idadi kubwa ya watanzania katika maeneo mbalimbali wamekwisha athirika na madhara yatokanayo na zebaki.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** jambo hili hailna ubishi kwa wakazi wanaotumia maji ya Mto Ruvu ambao unapitia Morogoro kusini ambako kuna wachimbaji wadogo wa dhahabu na katika uchenjuaji wa dhahabu uwezekano ni mkubwa wa kutiririsha maji yenye Zebaki kwenye mto Ruvu, ukienda kanda ya ziwa ni yale yale na ukienda huko Tanga, wilaya ya kilindi uwezekano ni mkubwa.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa; kwa Mkataba huu itasaidia sana kuiamsha Serikali juu ya udhibiti wa matumizi ya Zebaki hasa kwenye uchenjuaji wa dhahabu, lakini itakuwa ni busara pia kwa Serikali kutafuta kwa kushirikiana na Sekretariet kwa mujibu wa kazi zake chini ya Ibara ya 24 ya Mkataba, ili kutafuta na kutumia kile kinachoitwa ***" the Best Available Techniques"*** katika kuhakikisha matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu yanakomeshwa au yanapunguzwa kwa kiwango kikubwa sana.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** ardhi iliyochafuliwa na Zebaki, chochote kitakachooteshwa hapo na kuota na kutumiwa na binadamu au mnyama au ndege basi mimea hiyo itakuwa imepeleka Zebaki kwa binadamu au mnyama aliyetumia mimea hiyo, na ZEBAKI inabakia ardhini kwa kipindi kirefu sana. Hii ni kuonesha jinsi ilivyokuwa ni hatari sana kwa mazingira yanayotuzunguka.

**27.** **Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani haina pingamizi lolote juu ya uridhiwaji wa Mkataba huu, kutokana na ukweli kwamba madhara ya Zebaki kwa binadamu na

wanyama na mimea ni hatari sana kulinganisha na magonjwa mengine ambayo yamezoeleka katika jamii yetu. Kwa mkutadha huo chochote kitakachotoa njia mujarabu za kudhibiti matumizi yake katika nchi yetu ni jambo mwafaka kwa maendeleo watanzania, maendeleo kwa kiwango kikubwa yanaakisiwa na afya za watu katika maeneo mbalimbali.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** baada kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

..............................
Cecil David Mwambe (Mb)
**Kny: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI-OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA**
**10.9.2019**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumepokea taarifa zote sasa kwa hoja hizi tatu nazitoa kwenu mzijadili, lakini ni dakika tano/tano tu na hoja hapa ni kuridhia au kutokuridhia, hakuna mbwembwe za maneno mengi. Kwa hiyo, na majina ninayo hapa kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge ningependa tuzimalize hoja hizi asubuhi hii. Tunaanza, Mheshimiwa Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele na Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nianze tu na hoja iliyomalizika. Mimi ni mwanamazingira kwa kweli kama wenzetu hawa hoja za toka jana na leo wataendelea kuwa hivyo wa upande wa kushoto wanafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa ametoa mwelekeo mzuri sana wa mambo ya mazingira na kweli mimi nakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kusema ukweli hili tatizo lipo isipokuwa kwamba sumu ya zebaki ipo kila mahali, hata chakula chochote unachokula kuna kasumu ndani yake.

Tatizo la binadamu ni kiasi gani cha sumu kinachoweza kuathiri, lakini sumu kama sumu zipo tu kila siku zipo kila mahali, nikupongeze kwa kweli umefanya vizuri na mimi nadhani sina mjadala kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuja kwenye hoja ya pili, tunapokuwa tunapandisha haya Mapori ya Ugalla na Kigosi. Mapori haya tunachotaka kufanya ni kutengeneza *circuit*. Nataka nikukumbushe *circuit* maana yake nini, ukisema uende kutembelea Mikoa ya Kanda ya Ziwa maana yake unaenda kwenye Mikoa ya Mara, Kagera, Geita, Mwanza na Shinyanga, hapo umetengeneza *circuit* ya kutemebelea maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *tourism industry* kuna kitu tunaita *circuit*, kwa hiyo tukienda kwa mfano mgeni anataka kuja Kilimanjaro anatakiwa atoke Kilimanjaro aende *KIA*, akitoka *KIA* aende *Lake Manyara*, akitoka *Lake Manyara* aende Ngorongoro, akitoka Ngorongoro aende Serengeti; hapo umetengeneza *circuit* ya Serengeti na mafungu yake yanaweza kuwa yanaongezeka kutokana na hiyo *circuit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunapandisha Mapori ya Kigosi na Ugalla tuna maana kwamba kuna Burigi, Kigosi, Ugalla na Katavi, lakini katikati yake kuna Mapori ya Akiba Muyowosi, Ugalla na Kigosi. Kwa hiyo, tunatengeneza *circuit* ya Kusini ambayo mtu akitembea; mtu/mgeni ukimwambia atoke Dar es Salaam aende Katavi, atembee Mbuga ya Katavi arudi Dar es Salaam hawezi kwenda anaona kama hajatengeneza kitu. Kwa hiyo, tunataka atembee Katavi aende Ugalla, aende Kigosi na aende Burigi, kwa hiyo tunakuwa tumetengeneza hiyo *circuit* ya upande wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, hali iko sawa na maendeleo yanakuja kwa njia hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Augustine Masele, Mheshimiwa Peter Kafumu na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitumie muda huu kuweza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kuja na mpango mzuri huu wa kuyapandisha hadhi mapori haya ya Ugalla na Kigosi ili kuweza kuunganisha pamoja na Azimio la jana la *Mwalimu Nyerere National Park* ambayo ilikuwa ni Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda yetu ya Ziwa imekuwa ni sehemu ambayo kwa kweli ni chanzo cha uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kwa wananchi wetu kuweza kuwa wakataji wa misitu na uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, hatua ya Serikali ya kuyapandisha mapori haya hadhi na kuyaita Hifadhi za Taifa ni hatua muhimu kwa maendeleo ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maana hiyo mimi nitakuwa na mapendekezo tu machache juu ya jambo hili ya kwamba sasa kwa sababu tumeanza kuwa na *national parks* nyingi katika Kanda hii ya Ziwa, tukianza na zile za Burigi, Chato, Ibanda na Rumanyika na sasa tutakuwa na hii Hifadhi ya Kigosi pamoja na Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Wizara pamoja na Serikali zianzishe Vyuo vya Utalii pamoja na Vyuo vya Misitu pamoja na Mamlaka za Manyamapori na vyuo mbalimbali vya kuweza kufundisha watu juu ya elimu ya utalii kwa sababu vitu hivi ni vitu vigeni katika maeneo haya na kwa maana hiyo wananchi wetu watahitaji kupata elimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika upande wa Azimio la Kuridhia Mkataba wa Minamata na matumizi ya zebaki. Mimi niseme tu kwamba kwa kweli jambo hili naliunga mkono kwa sababu sisi pia ni waathirika wa masuala haya ya matumizi ya zebaki kwa sababu ni wazalishaji wa dhahabu na tuna wachimbaji wadogo wadogo ambao wanatumia mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maslahi ya muda, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masele kwa mchango wako na ushauri mzuri, Mheshimiwa Peter Kafumu, Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Koshuma.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,asante. Na mimi naomba nichangie kidogo juu ya mkataba huu ambao unataka kuhakikisha matumizi ya zebaki yanakuwa ya salama. Ulianza kutumika mwaka 2017 na sisi mwaka 2019 tunaridhia, kwa kweli tumewahi, Serikali naishukuru sana kwa kuamua kufanya hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu kama alivyoeleza Waziri una mambo kadhaa unaoelekeza. Mambo hayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba zebaki haichimbwi tena, migodi yote ya zebaki ifungwe na mingine ambayo ipo inaendelea ihakikishe kwamba haizalishi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matumizi ya zebaki au bidhaa zinazotumia zebaki na zenyewe zisitumike lakini zaidi sana ni matumizi ya zebaki katika kuzalisha dhahabu. Mkataba unaelekeza kuwe na matumizi yaliyoangaliwa, sio matumizi holela, mkataba hausemi kwamba tusichimbe dhahabu kwa uchimbaji mdogo, tusiunganishe dhahabu bila kutumia zebaki, lakini tuhakikishe matumizi haya hayafanyi mazingira yakaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba nilivyokuwa msimamizi wa sekta hiyo ya uchimbaji mdogo, wachimbaji wadogo wengi sana wameathirika na hata watu/watoto wanaozaliwa kwenye maeneo hayo wana hali mbaya sana; wanazaliwa wengine hawana macho na wengine vichwa vikubwa. Kwa hiyo, ni jambo la msingi sana Serikali tutakapomaliza kupitisha huu mkataba, tutengeneze sheria na kanuni ambazo zitahakikisha matumizi ya zebaki kwenye maeneo ya uchenjuaji wa madini yanakuwa ya

salama, tusiruhusu kama ilivyo sasa watu wanachenjua tu kwa kutumia zebaki bila *control. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; naomba niombe basi Serikali tu-*domesticate* huu mkataba kwa kutengeneza sheria, tusibakize zile sheria za zamani hazitoshi, tutunge sheria itakayoelekeza jambo hilo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Dkt. Kafumu kwa mchango wako na ushauri mzuri, Mheshimiwa Gekul Pauline, Mheshimiwa Kiteto Koshuma na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika maazimio haya mawili. Mimi naomba nijielekeze kwenye azimio hili la kupandisha hadhi mapori haya mawili ya Ugalla na Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze tu Serikali yetu kwa nia njema ya kukuza hii *circuit* ya Magharibi sasa kwa sekta ya utalii. Hili ni jambo jema sana kuona kwamba utalii katika nchi yetu unakuwa haubaki upande mmoja wa Kaskazini au Kusini lakini pia upande wa Magharibi wa nchi yetu unaangaliwa maana yake katika kukuza uchumi wa nchi yetu hili likipitishwa na Bunge letu tunakwenda kugusa uchumi wa wananchi wetu, lakini pia tunaongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu utalii katika nchi yetu unatuletea *forex* zaidi ya asilimia 25 mpaka 30 *forex* inatokana na sekta ya utalii. kwa hiyo, tunapopandisha hadhi mapori haya mawili maana yake tunaongeza kiasi na *circulation* ya *forex* katika nchi yetu kwa sababu haya mapori sasa yanakuwa *managed* na *TANAPA.* Kwa hiyo, ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; katika Taifa letu, utalii inachangia Pato la Taifa zaidi ya asilimia 17.2 na mantiki yake ni nini? *TANAPA* wanapokuwa wana-*manage* sasa haya mapori ambayo yameongezwa kwa upande wa Magharibi inasaidia kukuza na kuongeza mchango katika Pato la Taifa kutoka ile 17 tunaweza tukafika 20 au 25. Kwa hiyo, ni jambo jema sana Bunge hili kupitisha mapori haya yawe chini ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; utalii katika nchi yetu unachangia ajira kwa zaidi ya milioni mbili. Maana yake tutapata vijana wengi wa Magharibi na maeneo mengine ambao wataajiriwa katika sekta hii baada ya mapori haya mawili sasa kuwa chini ya *TANAPA* na kuwa *managed.* Kwa hiyo, ni jambo jema katika kuongeza pia ajira hili linaweza likawa linatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninafikiri ni la muhimu sana ni suala zima la kuboresha zile changamoto ambazo *TANAPA* wanapitia. Nafahamu mtu ambaye ana-*manage* kazi vizuri anaongezewa ndio maana *TANAPA* wameongezewa haya mapori mawili lakini nishauri sasa Serikali pia waangalie na zile tozo ambazo *TANAPA* wanakuwa wanazipitia kwa sababu tumewaongezea sasa hifadhi zinafika zaidi ya 20 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri zile tozo pia Mheshimiwa Waziri ukaziangalia zile ambazo *TANAPA* wanapokuwa wanatoa *dividend* kwa Serikali asilimia 15 wanakuwa-*charged* pia kodi ya asilimia 30 tena katika kile ambacho wanakichangia. Lakini wanapokuwa wanachangia miradi ya maendeleo ni vizuri pia Serikali iangalie na zile tozo zingine ambazo wamekuwa sasa wakizipitia kama changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* naunga mkono hoja, ni jambo jema sana na naamini kwamba hili litasaidia kukuza utalii katika Ukanda wa Magharibi na mwisho wa siku tuta-*share* keki ya Taifa kwa pamoja na vijana wetu pia watapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na Serikali wakati mmetuletea kwenye Kamati mlieleza kwamba wananchi wale hawataguswa na mipaka ile mlikuwa makini sana. Mimi niwapongeze sana, hili Serikali kuona kwamba wananchi wale wanakuwa hawaguswi, hawasumbuliwi na mkachora ramani kwa upya sasa ili wananchi wasisumbuliwe na naamini kwamba hili litafanyika kwa nia njema na wananchi wetu watafaidika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gekul kwa mchango wako, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Kiteto Koshuma na Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa pia na Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu tunapoelekea katika kuazimia azimio hili la *Minamata Convention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa bila kupoteza muda naipongeza Serikali kwa kuleta azimio hili ndani ya Bunge. Ukiangalia umuhimu mkubwa wa kuridhia Azimio la Minamata; Minamata kwanza yenyewe kama jina la *convention* yenyewe imetokana na madhara ambayo yaliwapata nchi ya Japan katika hilo eneo ambalo linaitwa Minamata. Madhara ambayo yalitokana na *disposal* ya hii sumu ya zebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa nchi kama Tanzania na sisi kuweza kuridhia mkataba huu kwa ajili ya kuweza kulinda afya za wananchi hususan wachimbaji wadogowadogo katika migodi ya dhahabu ambao ndio watumiaji wakubwa sana wa zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wananchi wengi sana hususan Kanda ya Ziwa ambako ndio kumezungukwa na migodi mingi wakipata athari za sumu inayotokana na zebaki kwa ajili ya kuchenjua dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Kanda ya Ziwa, kule kina mama wanajifungua watoto wenye vichwa vikubwa, kule ndio tunaongoza kwa tatizo hilo. Hatujaishia hapo, kule Kanda ya Ziwa wakina mama ndio wanaongoza kwa kupata watoto ambao wanakuwa na ulemavu wa viungo mbalimbali kwenye mwili. Kwa hiyo, ukiangalia ukubwa wa tatizo hili ni jambo zuri sana Serikali imeona kwamba ilete azimio hili ili sisi kama Bunge tuweze kuliridhia na hatimaye kupata faida mbalimbali katika kuridhia mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi Tanzania tutapata faida zipi, moja; tutapata faida ya kwamba tunaweza tukapata mbadala wa matumizi ya zebaki. Kama tumeona kwamba zebaki ina matatizo ambayo yanasababisha matatizo ya kiafya kwa wananchi hususan hawa wachimbaji wadogo wadogo, ina maana kama nchi tunaporidhia mkataba huu, tutapata faida ya kupata mbadala wa matumizi ya zebaki, kwanza kwa sababu katika nchi zote ambazo zimeridhia mkataba huu kutakuwa na mambo matatu ambayo yatafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, ni kuweza kupunguza matumizi ya zebaki katika kuchenjua dhahabu kwenye migodi. Lakini kitu kingine ni kwamba ni nchi zote ambazo zimeridhia mkataba huu zitazuiwa kuchimba hii zebaki. Sasa kama zile nchi ambazo zinachimba zebaki zitazuiliwa sisi kama Tanzania tusiporidhia mkataba huu tutajipanga vipi kupata matumizi mbadala ya zebaki kama zebaki itakuwa imezuiliwa. Kwa hiyo, utaona ni vizuri kama nchi tukaridhia mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina jambo moja la kushauri Serikali pamoja na kwamba tunaenda kuridhia mkataba huu ninaomba wazingatie *article 18* ambayo inazitaka nchi zilizoridhia Mkataba huu kutoa elimu kwa watumiaji wa zebaki, lakini pia kuhakikisha kwamba inawasaidia wananchi kufahamu ni madhara gani wanayapata katika utumiaji wa zebaki. Naomba Serikali

iweke mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba wanatoa elimu kwa wananchi ambao wanaathirika na zebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naiomba Serikali izingatie *article 16* ambayo inazitaka nchi ambazo zimeridhia huu mkataba kuhakikisha wanatoa huduma bora za kiafya kwa zile sehemu/yale maeneo ambayo wameathirika na matumizi ya zebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo naomba Serikali waweke mpango mkakati kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yameathirika kutokana na matumizi ya zebaki wanapata huduma bora za kiafya ili kuweza kuwasaidia wananchi ambao tayari wamekwisha kuathirika, lakini pia ninaiomba Serikali kuzingatia ushauri huu katika mkataba huu wa zebaki umeweka kipengele ambacho kipo katika *article 26* ambayo inazitaka nchi kuomba waweze kufanya *amendment* katika mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusijifunge, katika mkataba huu matumizi yamewekwa kwamba kuacha kutumia ndani ya miaka kumi na tano, kwa hiyo naomba Serikali izingatie *article 26* ili waweze kufanya *amendment* kupunguza muda wa matumizi ya zebaki ili kuweza kuwaokoa wananchi wetu. Ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Koshuma. Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kuipata hii nafasi, lakini ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja kwa vile huu mkataba au hili azimio itaisaidia kuifanya nchi iondokane na athari ambayo ilikuwa tayari inaangamia kutokana na *climatic change* au mabadiliko ya tabianchi ambayo Tanzania ilikuwa mojawapo ya nchi ambayo inaingia katika maangamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hizi Hifadhi ya Ugalla na Hifadhi ya Kigosi kuingia katika hifadhi sababu zake

kwanza Tanzania ilikuwa tayari misitu inatoweka, Tanzania wanyamapori walikuwa wanatoweka, hata uoto wa asili ulikuwa unatoweka, sasa kitendo cha kujikuta leo tunaazimia hili azimio ni imani yangu kuwa sasa hivi tunakwenda kubadilisha mazingira ambayo yalikuwa nchi inakwenda katika jangwa kuirudisha katika nchi ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, Mikoa ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Tabora kote huko ilikuwa tayari kumeshaingia jangwa kubwa sana kwa ajili ya watu walikuwa wanakata miti na ilikuwa sasa hivi mpaka Mikoa ya Lindi, Kusini kote misitu inatoweka, lakini sasa hivi *TANAPA* ina mbuga 20 wana matatizo makubwa ya kutozwa kodi nyingi ambazo zimeingizwa mle ndani. Je, mmewapangiaje kuwaondolea hizo kero ambazo itaifanya kuzitengeneza hifadhi zingine ambazo hazizalishi ili kuifanya hizi hifadhi zingine ziweze kuzitegemea zile hifadhi ambazo zinazalisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, leo hatuitegemei Ugalla katika muda mfupi huu kuweza kuzalisha wala Kigosi, Burigi na hizi hifadhi mpya hii ya Selous, lakini mkiwatengenezea mazingira ambayo itaifanya hii taasisi iweze kujiendesha mtakua mmefanya vizuri sana, lakini si hivyo tu, kuwaweka viongozi ambao wana uwezo. Tumezoea kuwaweka watu ambao hawana uwezo matokeo yake baada ya muda watu hawa watatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo, *Director General* wa *TANAPA* amepewa hifadhi 20 kwa kweli tumpigie makofi huyu baba amefanya kazi ya ziada sana, ameweza kuifanya *TANAPA* kuweza kupata mapato na nchi hii kujivunia *TANAPA* kama eneo la kujivunia. Je, mmempa hizi hifadhi, mmemwekeaje mazingira yake, anastaafu niliongea katika Bunge lililopita, kama anastaafu mmejipanga vipi hao wanaotaka kuja ili angalau awaachie watu ambao mfumo mzuri ambao aliuendeleza ili uweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yangu kuwa Serikali isiangalie watu kwa ajili ya uzee, angalia leo Malaysia watu wazee ndio wanaiongoza Malaysia, siyo lazima kila

mahali iwe kijana, hata mzee ukimuongezea muda akaisimamia hiyo kitu mtafikia mahali nchi hii tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia suala la zebaki, hili azimio ni zuri, kwa sababu wachimbaji wadogo wadogo wote wanafanya uchenjuaji wao kandokando ya mito na kandokando ya mito tunategemea binadamu wanakwenda kulima, tunategemea kwenda kuchota maji kandokando ya mito, tunategemea wanyama kandokando ya mito kwenda kunywa maji, sasa *contamination* hii ya madawa ambayo yanatumika ya zebaki inatufanya Watanzania wengi tunaathirika, tuchukue Mikao ambayo kuna wachimbaji wanahamahama kila siku, athari yake si ndogo, ina maana miti yetu, mito yote inaingia katika maji machafu lakini siyo sababu lazima tupange mpangilio ambao na hawa wachimbaji wadogo wadogo, kwa vile ndiyo maisha yao, tuwe tumewawekea mazingira gani, lazima tuwe na shughuli mbadala ya kuwakabidhi au kuna kitu mbadala cha kuwasaidia hawa watu ili na wao wasiendelee kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana katika masuala ya mazingira, Serikali tuisimamie, tulikuwa na asilimia 20….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea nilimtaja Dkt. Immaculate Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi, na mimi ninaridhia Azimio hili la Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki, namba moja kwa sababu ya madhara yaliyo makubwa sana kimazingira na kiafya katika jamii kutokana na matumizi haya

ya zebaki na namba mbili ni kwa sababu matumizi haya ya zebaki nchini yako makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *article* namba 3 ya mkataba huu unaongelea masuala ya ni nchi kutambua ni kiasi gani cha zebaki ilichonacho na nimepitia leo asubuhi ripoti ya mazingira kwa mwaka huu inaonesha kwamba Tanzania kwa sasa tumeweza kutengeneza au kusambaza zebaki katika mazingira tani 33.5 ambayo kwenye Mkataba wamesema kwamba nchi inaweza inatakiwa isi-*exceed* tani 10 katika ku-*generate* zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *article* namba 7 ya mkataba huu pia inaongelea kuhusu uchimbaji mdogo wa dhahabu ambao unatumia zebaki na hapa nchini kuna wachimbaji wadogo takribani milioni 1.5 na wengi wao wakiwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria, kwa hiyo idadi ni kubwa wanaofanya shughuli za kiuchumi, lakini pia wanajiweka katika *risk* ya *contamination* wao wenyewe kujiharibia afya na walio wazunguka na mazingira pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuwafatilia nini ambacho Mkataba huu unaelekeza ili kuwasaidia wananchi kiuchumi na kuwapa *alternative sources* katika shughuli zao za uchimbaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo *article* saba inasema kwamba nchi lazima itengeneze na kupitisha mpango kazi, au mpango mikakati, ni jinsi ya ku-*deal* na zebaki hususani katika wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *article* namba 12 katika mkataba huu, unaelezea kuhusu mkakati kwamba nchi iwe na mkakati mahsusi wa kurekebisha madhara ambayo yametokea kutokana na zebaki katika mazingira, sasa nilikuwa nataka nisisitizie kuwa nimesema asilimia kubwa ya wanaotumia zebaki ambayo inaathiri mazingira ni katika Ukanda wa Ziwa na tunajua kwamba karibu asilimia 90 ya uchimbaji wa dhahabu uko katika Ukanda wa Ziwa na

asilimia kubwa ya wachimbaji hao ni wale wadogo wadogo ambao wanatumia zebaki katika kuchenjua hiyo dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tatizo ni kubwa kuliko tunavyofikiria na lazima sasa tufate mwongozo wa huu mkataba kuangalia jinsi tunai-*save* vipi *Lake Victoria* yetu na wale ambao wanafanya shughuli za uchumi kuzunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisisitizie hapa *article* namba 13 inamuhusu Waziri husika ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wangu wa Bajeti kuhusu sasa hapo Mfuko wa Mazingira una kazi maalum na mahsusi, kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha wangekuwepo hapa waone kuwa tunaenda kuridhia mkataba huu sisi kama nchi, lakini mfuko wetu wa mazingira unasoma sifuri wakati tuna mambo mahsusi ya kimazingira ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *article* 13 katika mkataba huu unaongelea kuhusu rasilimali fedha na utaratibu wa jinsi ya kutumia hizo fedha katika kurekebisha madhara au kutoa elimu kuhusu zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa naomba niguse kwenye *article* 16 ya mkataba huu unaongelea masuala ya afya. Shida ya hii zebaki katika afya zetu zinaweza zisionekane papo kwa hapo na madhara yake ni makubwa sana kwa sababu yanaenda kubadili *DNA* yako (vinasaba vyako) na pia yanakaa kwenye mazingira kwa miaka elfu na maelfu, haviondoki hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna tayari ambayo wameshapata madhara ya kiafya kutoka kwenye zebaki basi naomba kuwe na mkakati mahsusi wa Kiserikali wa kuwa na vituo vya afya mahsusi na wanaotoa huduma mahsusi kwa wale ambao tayari wamepata madhara ya zebaki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Sware kwa mchango wako na ushauri wako. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kunipa nafasi niweze kuchangia na kwa ujumla mambo mengi yameshazungumzwa na Wabunge wengine waliochangia, lakini nitumie nafasi hii kwanza kabisa kusema naunga mkono maazimio yote yaliyoletwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono maazimio yaliyoletwa na Serikali, pia nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa watu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ulinzi mkubwa wa rasilimali zetu, hata ongezeko la tembo mpaka wanakuja kwenye makazi ya watu sasa hivi ni matokeo ya kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kazi kubwa mliyoifanya ya kuhifadhi na tembo wamekuwa wengi basi mtusaidie kwenye yale maeneo kama kule Korogwe tumeathiriwa sana na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaunga mkono, nichangie kwa upande wa maazimio haya mawili ya kubadilisha hadhi Mapori ya Akiba ya Ugalla na Kigosi kuwa Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ziko faida nyingi sana kupandisha hadhi mapori haya na tunajua kwamba Hifadhi ya Taifa ni hatua ya juu kabisa ya uhifadhi kwa maana kwenye Hifadhi ya Taifa haturuhusu shughuli nyingine za kibinadamu, kwa hiyo kwa mapori haya kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa tutakuwa tumeimarisha ulinzi wa rasilimali zetu, ikiwemo wanyama na baionuwai nyingine kwenye maeneo haya ya mapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaipongeza sana Wizara na tunaunga mkono azimio hili kwa sababu ni jitihada za kwenda kuongeza na kuimarisha ulinzi wa rasilimali zetu, lakini pia iko faida nyingine ya kupandisha hadhi mapori haya na kuwa Hifadhi ya Taifa. Faida nyingine kubwa ni kwenda kusaidia kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa, lakini pia kwenda kugusa maisha ya watu wetu, hasa kwenye maeneo ambayo yanapakana na hifadhi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma tulikuwa tunapiga kelele kidogo baadhi ya watu kwenye mambo kama ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Chato, sasa kwa kazi kubwa inayofanywa na Serikali sasa hivi ya kuimarisha miundombinu kama ujenzi wa viwanja wa ndege, kama reli ya *SGR,* kama ujenzi wa barabara, lakini pia kufufuliwa kwa shirika letu la ndege ni sehemu ya kutusaidia kwenda kuongeza pato kwa maana inakwenda kuchocheo utalii kwenye hifadhi hizi ambazo zitakwenda kuanzishwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono maazimio hayo, lakini naomba nishauri kwenye maeneo mawili, *TANAPA* ina hifadhi 19 na jambo hili limesemwa sana na tunaomba tuliweke msisitizo kidogo, tukichukua azimio tulilopitisha jana na haya mawili ya leo na yakienda kupita na hifadhi hizi zikianzishwa tutakuwa na jumla ya hifadhi 22 na hifadhi zinazoweza kujiendesha ni hifadhi tano. Kwa hiyo, unaweza ukaona huo mzigo wa kuendesha hifadhi nyingine ulivyokuwa mkubwa kwa *TANAPA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale majibu mazuri sana ya kitaalamu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili jana, lakini tunaomba tushauri vitu viwili, kitu cha kwanza, ni lazima Wizara iisimamie *TANAPA* vizuri na iwaelekeze waongeze Mkakati madhubuti wa kutangaza masoko ili kusaidia hifadhi hizi mpya zinazoanzishwa tusichukue muda mrefu sana zikaendelea kuwa tegemezi, ziweze kuanza kuingiza mapato vizuri na ziweze kuweza kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ni kwenye mzigo wa kodi, lilisemwa jana, lakini hata mama yangu Mheshimiwa Lulida amelizungumza hapa. *TANAPA* wanalipa kodi nyingi, *TANAPA* wanalipa asilimia 15 wanatoa asilimia 15 ya gawio kwenda Serikalini, malipo ya asilimia tatu kwenda kwenye *tourism development levy,* wanalipa *skills development levy,* lakini pia wanalipa *cooperate tax,* lakini hayo yote siyo shida ile miradi wanayofanya kwa ajili ya kusaidia jamii ambazo zinapakana na Hifadhi za Taifa na yenyewe inakuwa inatozwa kodi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tunaunga mkono azimio hili, ni azimio zuri litatusaidia kuimarisha maliasili zetu, litatusaidia kuongeza pato la Taifa lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** ...salama nipongeze mkakati wa kuweza kutangaza vivutio vyetu ili waongeze utalii kwenye maeneo yetu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo naongeza muda usiozidi dakika 30 tuweze, tumalize shughuli yetu. Namuita Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye maazimio yaliyoko mbele yetu na nita-*concentrate* sana kwenye maazimio mawili, Maazimio ya Maliasili ambayo ni lile la kupandisha mapori ya Akiba mawili kwenye maeneo ya Tabora kuweza kuwa *National Parks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira kubwa ya maazimio haya natambua kabisa kwamba ni ya kuimarisha ulinzi wa maliasili zetu, lakini pia kufungua fursa za utalii kwenye maeneo ya Kanda ya Magharibi jinsi ambavyo

tumekuwa na mkakati huo kuweza kupanua wigo wa utalii zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mapori mengi ya Mkoa wa Tabora yakiwepo haya ambayo yanaenda kuwa *National Parks* ikiwepo pia na mapori ya misitu mengi sana kutokana na kukosa ulinzi kwa miaka mingi iliyopita yalivamiwa na watu na baadaye baadhi ya maeneo vijiji vilisajiliwa kisheria na watu wakaendelea kuishi kule kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano eneo linaenda kuwa *Ugalla National Park* ambalo kilometa 2065 ambazo zitaungana na zile kilometa 1800 kuweza kuwa *National Park* hizi kilometa 2065 zinatoka kwenye Msitu wa *Ugalla North* na kwenye huu msitu wa *Ugalla North* ndiyo eneo ambalo Kaliua wananchi vijiji vitatu vimo mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kijiji cha Zugimlole ambacho kuna vitongoji vyake, Kijiji cha Uyumbu na Kijiji cha Igombe na mwaka 2017 hapa Bunge liliagiza Wizara kuweka mipaka ya maeneo ya hifadhi na wakaanza ule utaratibu wa kuanza kuweka mipaka, lakini hawakushirikisha wananchi, nilivyolalamika Bungeni hapa wananchi wenyewe, Wabunge wengi wanalalamika Bunge likaagiza zoezi lile lisitishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ile ilikuwa imewekwa kwenye miji ya watu na hivi tunavyoongea sasa hivi yaani zile *beacon* ziko kwenye miji ya watu, kwa hiyo tunakwenda kupitisha azimio hili lakini kuna baadhi ya maeneo kwenye *Ugalla North* ambapo bado wananchi wapo mle ndani, lakini ukiangalia pia hata maeneo ya Kigosi kuna watu walikuwa wanafuga misitu huku nyuki, kitu ambacho ni *friendly* na mazingira na kwa taarifa za Mheshimiwa Waziri peke yake ni kwamba kuna watu wamefuga kwa muda mrefu na kwa mwaka jana tu kuna watu waliosajiliwa mle ndani, watu wameweza kuvuna tani 701 ambazo zina thamani ya shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo langu ni kwamba maeneo haya tunakwenda kuyapitisha kuwa *National Park* lakini bado kuna agizo la Rais pia ambalo aliagiza maeneo yote ambayo wananchi walikuwa wanabughudhiwa kwanza tutulie na akaunda Tume yake kuweza kuhakikisha kwamba maeneo haya yanapitiwa tuweze kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo langu naomba, pamoja na kuwa inaenda kupita, lakini lazima Wizara ituambie namna gani watu hawa ambao bado wako mle ndani watahakikisha kwamba waondolewa kiutaratibu ili wasibughudhiwe, kiukweli hatupendi maumivu haya yaendelee, hatupendi kabisa maumivu haya yaendelee kwa sababu ni kilio chetu cha muda mrefu na mpaka Mheshimiwa Rais amefikia hatua ya kuweza kuunda Tume anajua watu kabisa wako ndani ya Hifadhi, lakini waliingia baada ya kuwa mipaka ile ilikuwa *pollars* ilikuwa pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mimi naomba sana kwamba hilo liangaliwe, lengo letu ni kwamba kweli tuihifadhi kwa kupanua wigo wa utalii lakini pia wananchi wetu wasije wakateswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda kuwapa pia *TANAPA* mzigo mkubwa sana kwa sababu tukianza....

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Ahsante. Mheshimiwa Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na wa mwisho Mheshimiwa Chumi.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hakuna mtu anayeweza kupinga maendeleo ya Kitaifa ikiwepo kutunza hifadhi zetu na kuweza kutambua maeneo mbalimbali yakafanyika kuwa hifadhi, mimi mwenyewe mmoja wapo ninapongeza Wizara ikiendelea kufanya hivyo, lakini ikifuata kanuni na sheria za Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyepita ametoka kuzungumza mahali hapa kwamba watu wa lile Pori la Ugalla walikuwepo siku zote na Serikali hii ilikuwepo, wananchi wale wakapewa huduma mbalimbali, huduma za umeme, maji wameendelea kuishi kwa miaka na kufanya mifugo yao mahali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka Serikali itoe taarifa kwa wananchi, wakaweza kutoa na elimu na kuwaelimisha wananchi ili waweze kujua maendeleo yao, maana yake mwisho wa siku walinzi wa hifadhi wa hizi ni hao hao wananchi wanaoishi maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa wamezaliwa katika maeneo hayo, leo hii tukiwafanya wakimbizi katika nchi yao tunakuwa hatuwatendei haki. Mpaka sasa Serikali inaleta hoja hii mezani kwako hata Kamati yenyewe haijafika kwenda kukagua maeneo husika na kuona ni jinsi gani wananchi wameathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu juu ya *TANAPA*, *TANAPA* tumeipatia mzigo mkubwa na ndiyo kazi yetu *offcourse* lakini je, bajeti tunazopanga kwa Mheshimiwa kiongozi huyu wa *TANAPA*, je, pesa hizi zinamfikia ili aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi na kazi akafanya kwa uweledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vibaya zaidi kuongeza kazi zaidi wakati pesa Serikali haitoi kwa *TANAPA* wala haitoi msaada wa kuisaidia *TANAPA* kuweza kufanya kazi yake vizuri, hata tunapoingia kwenye ushindani wa utalii ni lazima mapori haya yawekwe kimpango mzuri hata kuweza kuvutia hawa watalii, lakini kama hawana pesa wanajipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wananchi katika hizi hifadhi zimekuwa za muda mrefu, tunaomba Wizara hata kama leo mnapitisha kwa kura nyingi...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:**...mbazo ziko upande wa pili, tunaomba Mheshimiwa Waziri Kigwangalla uende ukahakikishe hiyo migogoro kwa ukaribu sasa, japokuwa tumetangulia mbele wewe utakuwa unarudi nyuma, wananchi wakaweze kutatuliwa matatizo ya kwao, tunakuomba ufanyie hivyo bwana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri tunataka tujue katika vijiji kwa mfano kwa upande wa hili Pori la Ugalla kuna watu wa Sikonge na Kaliua mmekataje? Ni kiasi gani ambacho kitaenda kwenye hifadhi mtuambie na kiasi gani ambacho kitabaki kwa wananchi, kilio changu mimi bado ni wananchi, kwa sababu tunajua mwisho wa siku wananchi hawa mmeshawawekea mawe, kuna wakati Mbunge wa Kaliua aliwahi kuzungumza hapa kwamba mnaweka mawe mpaka kwenye vitanda vya wananchi.

Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri kama Mtanzania, naomba urudi tena ukaangalie uhalisia wa Mheshimiwa Mbunge aliyezungmza katika Bunge hili, kama ni kweli vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaunga maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia. Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kukubaliana na hili azimio la kuridhia hifadhi mapori ya akiba kuwa hifadhi pori la Ugalla pamoja na Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia natokea huko Tabora na ninafahamu ni kwa namna gani wananchi wengi waliweza kuvamia haya mapori, hivyo ningeiomba sana Serikali pamoja na dhamira na nia nzuri ya kwenda kuweka Hifadhi za Taifa katika maeneo haya, lakini hawa wananchi ambao wako maeneo yale watafutiwe utaratibu mzuri wa kutafutiwa maeneo ya kwenda ya kukaa na waondolewe pale bila bughuza yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Tabora tunasema tunashukuru kwa sababu tunakwenda na sisi kuwa na Hifadhi za Taifa katika Mkoa wetu mapori katika Mkoa wa Tabora yamekuwa mengi sana hivyo yamepelekea migogoro mikubwa baina ya wakulima, baina ya wafugaji, baadhi ya wafanyakazi wa hifadhi hizi. Kwa hiyo, ningeomba sana kwamba tunapokwenda sasa kutengeneza hifadhi katika maeneo haya ya Ugalla na Kigosi basi tuangalie hata zile changamoto zilizokuwa zinakabili maeneo yale zitatuliwe kwa haraka ili hawa watu waweze kujua sasa wanapopelekwa ndio yatakuwa maeneo yao ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika azimio hili la Mkataba wa Minamata, mimi nilikuwa nataka kushauri Serikali kidogo kwamba pamoja na kwamba azimio hili mimi silipingi kabisa, lakini cha ajabu toka mwaka 2013 tulipotia saini mkataba huu, leo mwaka 2019 ndio tunakuja kupitisha azimio hili, nini kimetukimbiza na kinachopelekea kupitsha azimio hili leo mwaka 2019. Kwa sababu madhara ya zebaki yanajulikana na mimi nimejionea mwenyewe kwa macho yangu kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mazingira, nimejionea mwenyewe kwa macho yangu ni kwa namna gani athari za zebaki zinavyoweza kuwakabili watu hasa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi wanayotumia wachimbaji wadogo ni mabaya sana, lakini ukiangalia hapa tumepewa miaka 15 kwenda kumaliza kabisa matumizi ya zebaki, lakini hii miaka mingine ya nyuma kuanzia 14 kwenda huku mpaka huu mwaka mmoja nini kitafanyika kuhakikisha

kwamba wananchi wetu hawaendelei kuumizwa na matumii ya zebaki. *(Makofi)*

Mimi ningeomba sana Serikali Mheshimiwa Waziri mje na mpango madhubuti wa kuona kwamba ni kwa namna gani mnakwenda kulimaliza kabisa suala la matumizi ya zebaki yalivyo hivi sasa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kupata nafasi na kama wenzangu walivyosema na mimi naunga mkono maazimio haya ya Bunge ya kuridhia ubadilishaji na kuongeza hadhi haya mapori kama ilivyokuwa imetajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nipende kusema mambo machache. La kwanza kama ambavyo pia Kamati imesema sasa hivi tunaenda na kitu kinaitwa *conservation with sustainable development*, maana yake ni nini kwamba kwa kuyapa hadhi hii mapori haya moja itaimarisha ulinzi, lakini pili itajenga mazingira bora ya kuendeleza utalii. Sasa ili hayo yaweze kufanyika na kufanikiwa kuna kitu sisi katika nchi yetu tunasema ni ya pili kwa vivutio vya utalii baada ya Brazil, maana yake tukizungumza katika ile tunaita *comparative advantage* sisi tuko vizuri katika dunia baada ya Brazil, lakini tukizungumzia *competitive advantage* bado kuna mambo ya kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nijielekezee katika kutoa ushauri sasa kwa Serikali pamoja na kupongeza jitihada hizi basi kuongeza nguvu ili tuweze kuwa *competitive* katika suala zima la utalii kusudi kuongeza mapato kutoka asilimia 17 iliyoko sasa hivi na kuendelea.

Sasa ili tuwe competitive maana yake ni nini, lazima tuboreshe mazingira ya kuwekeza katika shughuli za utalii, lakini pili kuiongezea ngu *TANAPA* na *TTB* katika kujitangaza. Lakini la tatu pia kupunguza vikwazo ambavyo kwa namna

moja au nyingine vimekuwa kizuizi katika kuhakikisha kwamba sekta hii ya utalii pamoja na kuongeza hadhi hizo hatufikii malengo ambayo yanaweza kutufanya tukawa *competitive* katika masuala mazima ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine na la muhimu ambalo Mheshimiwa Masele alilisema pale ni kujengea uwezo vyuo vyetu vya mafunzo ya utalii ikiwa ni pamoja na kuviongezea nguvu katika mafunzo ya lugha, kwa sababu tunatarajia watalii waje kutoka maeneo mbalimbali pamoja na lugha yetu ya Kiswahili pamoja na lugha ya Kiingereza, lakini vyuo hivi vipewe msisitizo wa kuongeza mafunzo ya lugha nyingine za ziada ili watalii wanapokuja basi kunakuwa na mawasiliano ambayo ni mepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho napenda kuipongeza Serikali na hasa Mheshimiwa Kigwangalla na timu yake na Naibu wake na watendaji wake kwa kweli kama ambavyo niliwahi kusema wakati fulani mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, wanafanya kazi nzuri, katika utendaji wao kazi nzuri basi wasisite pia kutazama na kutupia jicho katika suala zima la *historical sites.* Nimewahi kutoa mfano pale Kihesa Mgagao ambayo ilikuwa ni kambi ya wapigania uhuru....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** ...tungeitazama na tungeweza kuongeza mapato zaidi. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi kwa mchango wako na ushauri. Sasa naanza kuwatambua watoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Kigwangalla, *not more than 10 minutes*.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii ya kufafanua maeneo machache ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa

Wabunge wenzangu na pili niwashukuru wachangiaji wote na kimsingi niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kiasi kikubwa wameunga mkono hoja ambayo imewekwa mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia zaidi niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa waliotupa wakati tulipokuwa tukifanyia kazi azimio hili, lakini pia niwapongeze sana na niwashukuru Kambi ya Upinzani Bungeni pia kwa kuunga mkono hoja hii kwa kiasi kikubwa na niwahakikishie tu kwamba mashaka yaliyopo, wasiwasi mdogo uliopo tutaushughulikia kwa uungwana na ustaarabu wa hali ya juu tukizingatia mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamechangia hapa Bungeni, tunafahamu Mheshimiwa Magdalena Sakaya amezungumzia uwezekano wa uwepo wa watu katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu kwamba Mheshimiwa Rais anawapenda sana Watanzania, anajali maslahi yao na anayahudumia kwa karibu sana mahitaji ya Watanzania wote ikiwemo hawa Watanzania ambao kipindi ambapo ulinzi ulilega kwenye maeneo haya ya hifadhi walivamia na ndio maana mwezi Januari 15 Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alitupa maelekezo mimi pamoja na Mawaziri wengine saba tukafanya kazi kubwa sana ya uchambuzi wa maeneo yenye migogoro na maeneo yote haya tuna mapendekezo mahususi ambayo tumeyafikisha kwake na wakati atakapotupa mwongozo namna ya kuyamaliza basi tutarudi kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa wananchi kuwapa mrejesho, lakini pia kufanyia kazi maelekezo ambayo tutakuwa tumepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuko makini na nia ni njema na migogoro yote iliyopo katika maeneo yanayohifahiwa kwa kweli tutaishughulikia kiuungwana sana na sote ni mashahidi maeneo ya hifadhi kwa sasa yametulia kwa kiasi kikubwa, wananchi wanaishi vizuri na maeneo ya

hifadhi na askari wetu, hakuna tena ile pigapiga, kamata kamata haipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu pia kufafanua kwamba changamoto ambazo zimetolewa katika eneo la mzigo ambao anabebeshwa *TANAPA* tunazifahamu na Serikali imekwishaanza kuzifanyia kazi, mwaka huu tulifanya kazi kidogo bahati mbaya haikukamilika kama ambavyo tunatarajia, kwa hiyo tutaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Fedha ili tuweze kuona walau kuna namna ambayo tunaisaidia *TANAPA* na uhifadhi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho kabisa nisema tu kwamba baada ya mchakato wa kupandisha/kubadilisha hadhi maeneo haya matatu kwa maana ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na Hifadhi ya Taifa ya Kigosi Tanzania itafikisha Hifadhi za Taifa 22. Pia tukichanganya na *marine parks* mbili ile ya *Mafia Ruvuma Estoary Marine Park* pamoja na ile ya Mafia kule tukichanganya na hii ya Mnazibay tutakuwa nazo jumla *parks* zipatazo 24 na hivyo Tanzania itakuwa ndio nchi yenye hifadhi nyingi zaidi hapa Barani Afrika. Kwa sasa kuna nchi ya Kenya ambayo ina hifadhi 23 ukichanganya hifadhi za nchi kavu na hifadhi za kwenye maji, lakini Tanzania tulikuwa nazo hizo 16, baada ya kupandisha na kubadilisha hadhi maeneo yote haya sasa Tanzania tutakuwa tuna hifadhi 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambe anauliza hizi zina maana gani? Maana yake kubwa ni kwamba hii itakuwa ni *selling point* ya muhimu sana kwamba sisi ni nchi yenye hifadhi nyingi, kwa hiyo, kiuhifadhi itatupa *credit,* lakini pia kibiashara itatupa *credit* kwa sababu ni *selling point* kwenye *marketing* kuna *punch line*. Kwa hiyo, tukisema kwamba sisi tuna nyingi zaidi kuliko wengine tunaonekana sisi ni vinara na hivyo ni bora zaidi kuliko wengine na hivyo itatusaidia kuuza kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nukta yangu ya mwisho nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa mwongozo ambao amekuwa akiutoa

kutuwezezesha kufikia hatua hii. Kwetu sisi wahifadhi hii ni hatua kubwa na nyeti na hizi Hifadhi za Taifa sio tu zitasaidia kupata mapato lakini zinaweka mustabali wa maisha ya watu wetu. Nchi yetu imekuwa *degraded* kwa kiasi kikubwa, eneo la malisho ya mifugo limeharibika kwa zaidi ya asilimia 31, kiasi cha mvua kimepungua sana na sababu ni hii *encroachment* ya wananchi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na hii ilikuwa inatishia kuleta njaa miongoni mwa watu wetu ambao sisi Waheshimiwa Wabunge tunawatetea hapa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatua hizi anazochukua Mheshimiwa Rais za kumaliza migogoro, lakini pia kubadilisha hadhi baadhi ya maeneo ili kuyahifadhi vizuri zaidi ili kuyapa ulinzi mkubwa zaidi, ili kuweza kuyatumia kibiashara zaidi kwa kweli ni hatua ambazo zitaandika jina la Mheshimiwa Rais Magufuli kwa wino wa dhahabu kwa vizazi na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa maazimio yote mawili naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, naanza na hoja kuhusu Pori la Akiba la Kigosi.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi Lilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nakuja kwenye Azimio la pili linalohusu Pori la Akiba la Ugalla.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Ugalla Lilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Bunge limeridhia mapendekezo ya kubadilisha hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi. Pili, Bunge limeridhia rasmi mapendekezo ya kubadilisha hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla. Kwa hiyo, niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo na Mheshimiwa Waziri na timu yako ahsanteni sana.

Tunaendelea Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kuhitimisha hoja yako kwa muda usiozidi dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kuwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Sadiki Muradi pamoja na Makamu Mwenyekiti Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa umoja wao na kwa ushirikiano pamoja kuwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba azimio hili linafikia hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa kutoa maoni mazuri ambayo kimsingi kwa pande zote mbili Kamati pamoja na Upinzani wameunga mkono hoja hii. Pia niwashukuru wachangiaji wengine wote waliozungumza na wale walioandika kimsingi hakuna hata mmoja aliyepinga azimio la matumizi ya zebaki yaani *The Minamata Convention on Mercury*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa pongezi hizi na na kwa kuwa hakuna aliyepinga nataka nisema kwa ujumla wake tu kwamba mengi yaliyosemwa yamelenga zaidi katika kuonesha namna gani sasa kama tumeshakubaliana kwamba zebaki ni kitu kibaya, kina madhara kwa binadamu kwa afya ya binadamu na mazingira. Pia yako madhara ambayo yanaonekana na yanatokea na tunayafahamu na mifano tunaijua. Lakini pia

liko kundi la wachimbaji wadogo ambao wao wanaathirika moja kwa moja kwa sababu wanaichezea zebaki kwa kuishika kwa mikono hapa tuna kazi ya kufanya na ndio maana Jumuiya ya Kimataifa na dunia imeona ikae na kuja na mapendekezo ya makubaliano haya ambayo leo tumeyaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi suala la zebaki ni suala gumu kwa sababu viko vitu ambavyo hatuna namna bado tunahitajika kutumika kutumia zebaki kwa sababu ya aina ya teknolojia ambazo bado tunazihitaji kwa ajili ya huduma, kwa ajili ya matibabu, kwa ajili ya mila na kwa ajili ya baadhi ya utengenezaji wa vitu vingine ambavyo tunavihitaji. Na teknolojia mbadala wa vitu hivyo haujapatikana, kwa hiyo itatutuchukua muda kidogo na ndio maana hata katika kuridhia na hata azimio lenyewe linazungumzia juu ya kuondokana na matumizi ya *mercury* kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ifikapo kwa 2030 kusudia la mkataba huu ni kuhakikisha kwamba tuwe tumeondoka kabisa, sasa haya ni malengo na kimsingi *the legal status* ya *convention* hizi za Kimataifa huwa sio kwamba unapokuwa haujafikia *level* unaadhibiwa, lakini kutoingia na kukubali na kuridhia mikataba kama hii unaweza ukakosa faida za kushirikiana na wenzako duniani katika kuondokana na jambo ambalo si zuri kama ilivyo zebaki.

Kwa hiyo, kimsingi mimi nikubaliane na Wabunge wote na niseme tu kwamba Serikali imejipanga chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba tunakuwa na mpango mkakati wa kutekeleza azimio hili na tumekwishaanza maandalizi ya mpango mkakati huo na ifikapo mwezi ujao tutakuwa tayari tumeukamilisha mpango mkakati ambao utakuwa na majibu ya hoja nyingi sana zilizoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe namna ambavyo tutaweza kuondokana na matumizi ya zebaki kwa sababu ya ubaya ambao wote tumedhihirisha hapa kwamba ni kitu kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuomba na kusihi Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na maoni haya yaliyotolewa na watu wote pia msimamo wa Serikali katika kuamua kuridhia azimio hili ili tuwe pamoja na dunia tusiweze kukosa fursa nyingine za ushirikiano wa kusaidia na wenzetu duniani katika kuondokana na matumizi ya zebaki ambayo ni mbaya kwa afya ya binadamu lakini pia kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mussa kwa kushirikiana na mimi na kunisaidia na hata tumeweza kulifikisha azimio hili mahala hapa na kwa kumalizia nichukue nafasi hii kukuomba wasihi Waheshimiwa Wajumbe na Wabunge wote waweze kuridhia azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki yaani The Minamata Convention on Mercury Lilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Bunge limeridhia rasmi Azimio la Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki yaani *The Minamata Convention on Mercury.*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumefikia tamati kwa shughulizi zetu za leo, niwashukuruni sana kwa ushirikiano wenu tumeweza kuyafanya haya kwa tija.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kuna Mheshimiwa Kakoso kama mtu ameokota funguo za gari ndani au maeneo mengine katika *premises* za Bunge

Mheshimiwa Kakoso jaribuni kumpata nadhani ni za kwake. Sina lingine la ziada kwa maana hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 11 Septemba, saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 7:20 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 11 Septemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*